SUPA JACKPOT
TZS. 1,059,844,733
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



**Anayedaiwa** kuua mkewe akiwa na hawara aendelea kushikiliwa polisi

UKURASA 7


Nipashe TESA
Jumanne Desemba 27, 2022
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI
Gari linalopaa, kuendeshwa barabarani laja, litaanza kupatikana sokoni 2025
Nyama ya maabara sasa ruksa kuliwa
ELIMU
KWAHERI 2022
NA PANCRAS LUOGA
Uwe kijijini au mjini wakinge watoto na athari za kuangamia

UKURASA 13


# Nipashe

MWANGA WA JAMII

Jumanne Desemba 27, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581172

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper LIKE & FOLLOW US


## POMBE KALI

# Kauli ya Askofu Dk. Shoo yaibua gumzo



**Wadau**, madaktari bingwa Muhimbili, wanasaikolojia wanena... *uk. 2*



Moja ya ajali mbaya zilizotokea mwaka huu ambayo iligharimu maisha ya watu.

# Ajali barabarani zilivyogharimu maisha ya wengi mwaka unaoisha

UKURASA 3

# Tanzania yahimili uchumi licha ya UVIKO-19 na vita vya Ukraine

UKURASA 5




Waziri wa Elimu, Prof. Adolf Mkenda akifurahia jambo wakati wa uzinduzi wa mbio za 'Rombo Marathon' zilizofanyika Desemba 23, mwaka huu, wilayani Rombo zenye lengo la kufungua fursa mbalimbali katika kukuza utalii nchini, zilizoenda sambamba na kaulimbiu ya 'For People, For Better', Benki ya KCB imekua mdhamini wa mbio hizo zilizokuwa na umbali wa kilometa 21, 10 na tano. Kushoto ni Naibu Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Pauline Gekul na wafanyakazi wa benki hiyo. Kulia ni Meneja Masoko, Shose Kombe na wafanyakazi wenzake. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

**MICHEZO** NTIBAZONKIZA KUZIBWA NA WAWILI GEITA UK.28 | **KABWELA** UK.7



Abiria wanaosafiri kutoka Songe makao makuu ya wilaya ya Kilindi kuelekea Tanga na Arusha wakiwa wamekwama eneo la Msente mpakani mwa Kilindi na Handeni jana baada ya mabasi kushindwa kuendelea na safari kutokana na mvua zinazoendelea kunyesha kuharibu barabara hiyo. **PICHA: DEGE MASOLI**

# Kauli ya Dk. Shoo matumizi ya pombe kali yaibua gumzo

**Na Christina Mwakangale**

KARIPIO la ulevi kupindukia lililotolewa na Askofu Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dk. Frederick Shoo (pichani), limeibua mjadala huku wanasaikolojia na madaktari wakieleza sababu za kukithiri kwa unywaji pombe na madhara yake.

Katika mahubiri yake kwenye ibada ya Krismasi juzi, Askofu Shoo ambaye pia ni Mkuu wa Dayosisi ya Kaskazini, alikemea kunywa pombe kali kunakofanywa na vijana wa umri mdogo, akionya kuwa wanaharibu afya zao wakiwa na umri mdogo.

Baadhi ya wadau wa afya na saikolojia, wameiambia Nipashe kuwa vijana wenye umri mdogo kuanza unywaji pombe kali, kutawakwamisha kufanikiwa, wakiyataja mabadiliko ya soko huria, uchumi wenye ushindani na ushawishi kuwa sababu ya kundi hilo kujiingiza kwenye ulevi.

Vilevile, wamesema baadhi ya maudhui ya nyimbo nyingi za wasanii yanahamasisha ulevi, hali inayowafanya vijana kupenda kunywa kwa kuwa ni jambo linalohalalishwa.

Akizungumza na Nipashe jana, Daktari Bingwa Mwandamizi wa Afya na Magonjwa ya Akili wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Dk. Saidi Kuganda alisema pombe kali zimo kwenye orodha ya kundi la dawa ambazo zinaathiri akili mara tu zitumiwapo.

Alisema yapo makundi sita ya pombe za aina hizo, zikiwamo ambazo zinachangamsha akili (stimulants) na zinazolaza akili (depresants), pia zinazompatia mtumiaji maruweruwe.

"Zipo aina sita au zaidi. Lakini tabia yao kubwa ambayo ni common (kawaida) ni kwamba zinaanza kukupatia steam (raha au starehe) ambayo akili haraka inarekodi kuwa dawa hii ni kitu kizuri na kinanipatia raha ambayo huipati kwingine.

"Nguvu hii ni kubwa zaidi kuliko hata madhara au maudhi madogo madogo ya hiyo dawa. Mfano, pombe nyingi ni chungu lakini kwa 'steam' unayoipata ukinywa pombe, inakufanya ukubali uchungu ule mradi upate ile steam," alisema bingwa huyo wa afya ya akili.

Bingwa huyo alitaja sababu ya vijana wengi kunywa pombe hizo ni pamoja na kutaka kupata starehe, akisema itafikia mahala watahitaji kiwango cha juu. Pia alionya kuwa pombe husababisha kuzoeleka kimapokezi mwilini na kupoteza uwezo wa kuleta starehe.

"Hivyo, mnywaji inabidi aongeze kiwango, kwa vijana ndiyo mbaya zaidi, maana wao wana vishawishi vingi, inaharibu kabisa uwezo wake wa kufanya uamuzi sahihi, anakuwa tegemezi wa pombe na huchukua nafasi ya mwanzo kabla ya jambo lingine.

"Na hii ni taratibu mno inavyoingia, wala huwezi jua na ndiyo maana vijana wengi hubisha na kusema siyo kweli," alitahadharisha Dk. Kuganda ambaye pia ni Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Wataalamu wa Afya Tanzania (MEHATA).

Bingwa wa Magonjwa ya Ajali na Mifupa kutoka Taasisi ya Tiba ya Mifupa, Upasuaji wa Ubongo na Mishipa ya Fahamu Muhimbili (MOI), Dk. Kennedy Nchimbi alisema pombe zina madhara na wanywaji walio wengi hushindwa kutimiza malengo yao ikiwamo kujiingiza kwenye ushawishi mbaya.

"Unaweza kutekwa na mambo yasiyofaa kama umalaya, ugomvi, wizi na kuwa na uzembe, akili huondoka katika hali yake ya kawaida," alifafanua bingwa huyo.

USHAURI

Mtaalamu wa Ustawi wa Jamii na Mshauri wa Masuala ya Familia, Malezi na Makuzi ya Watoto na Malezi ya Vijana, Joseph Kayinga alisema kwamba katika kila jamii kuna tabia za asili zilizozoeleka ikiwamo kabila fulani kuwa wafanyabiashara, wacheza ngoma na nyinginezo na kwamba zingine zinaathiriwa na mabadiliko ya kiuchumi.

"Kila jamii ina utambulisho wake kutokana na mila na desturi. Inapofika suala la starehe, jadi ilikuwa kukutana sehemu ama nyumbani kwa mtu fulani, lakini sasa uchumi wa baa, hoteli, huko unatumia fedha ukiwa huru, mradi uwe nazo.

"Lakini zamani ukiwa nyumbani na mababu, yaani wazee, ukinywa pombe wakiona zinakuzidi wanakwambia 'inatosha' au 'nenda nyumbani'.

"Unapokwenda baa unakuwa huna nidhamu ya kwamba unywe kiasi gani, utakunywa utakavyo na kuonekana unakwenda na wakati wa kisasa, hii ni baada ya ukoloni kuja, yaani mfumo mpya wa ustaarabu wa unywaji ulibadilika kutokana na wageni na nguvu ya fedha kutawala.

"Lakini sasa ukiwa baa, ukanywa na wenzio unajenga heshima. Kisaikolojia kila binadamu anataka aonekane bora, imara na anaweza, na hii inafanya vijana watekeleze hilo kujiongezea sifa baa.

"Pia sasa kuna uhamasishaji wa unywaji pombe, zipo nyimbo zinaipamba kabisa pombe na ulevi ni sifa, 'kulewa na marafiki', ila jamii inaathirika kisaikolojia kutokana na hili," alionya Kayinga.

**WADAU WANENA**

Wakitoa maoni kwenye kurasa zao za mitandao ya kijamii kwa nyakati tofauti kuhusu karipio hilo la Askofu Dk. Shoo, baadhi ya wadau walikuwa na mtazamo tofauti, wakiwamo wanaomuunga mkono na wanaopingana naye.

Albert Mushi, mmoja wa wadau hao, alisema vijana wanapaswa kuacha pombe kabisa, akitamka: "Siyo pombe kali tu, pombe siyo nzuri kwa afya na hata kiimani mtu hawezi kuishi maisha yanayompendeza Mungu kama ataishi maisha ya kilevi".

Kwenye ukurasa wa mmjoa wa wachangiaji hoja hiyo ya askofu, anayejiita Mrusi alisema: "Askofu yupo sahihi, halafu hizo kali za bukubukum (Sh. 1,000), una akili timamu uelewe kwa buku kweli! Kulewa kwa buku ni upungufu wa akili au kulewa chini ya Sh. 700 wanakunywa vikali 'spirit' mno."



Mwingine aliyejiita Massawe alisema: "Dukani wanauza chakula, maji, dawa, sumu, ni wazazi pekee wawaelekeze vijana, kipi watumie na kipi wasitumie, idadi kubwa sana vijana hawana afya njema."

Mchangiaji mwingine kwenye ukurasa wa mtandao kijamii aliyejiita Whisky alisema: "Iimewaua kushinda mbege na komoni au kangala, watu wamevimba matumbo, 'soon liver disorder' itakuwa common (itakuwa kawaida).

Francis Msemwa, mchangiaji mwingine wa mjadala huo, alisema: "Jamani kaongea jambo jema, acheni pombe kali, maana yake vijana mmeshindakana."

Mdau mwingine anayejiita Denis Bongole katika ukurasa wake, alisema: "Unajua Askofu Shoo tunakuheshimu sana na tunajua wewe ni mtaalamu wa Theology, Haya ya pombe tupunguzieni masimango, tupeni akili tupate hela, msituzodoe. Huenda ndiyo kinachotupa amani zaidi ya misuto yenu. Na uzuri tukiwa baa, hatuwasemi kama mnavyotusema mkiwa huko kwenye nyumba zenu."

HABARI KITAIFA

# Ajali zilivyogharimu maisha ya watu 880

**Na Christina Mwakangale**

MWAKA 2022 umebakiza siku nne kufikia ukomo, ukiacha kumbukumbu nyingi. Kati ya mengi ya kukumbukwa, ni ajali zilizoacha huzuni miongoni mwa wanafamilia na jamii kupoteza ndugu na watu mashuhuri ambao walitegemewa na taifa.

Pia, ajali hizo zimeacha majeruhi wengi ambao hadi sasa wamelazwa hospitalini, na wengine wanauguzwa nyumbani na wamegeuka kuwa wategemezi huku familia zao zikipoteza mali na mwelekeo wa maisha kwa sababu waliowategemea wamefariki dunia.

Kwa mujibu wa Kikosi cha Usalama Barabarani nchini, Watanzania 886 wamepoteza maisha kati ya Januari na Novemba, mwaka huu, kutokana na ajali za barabarani huku 573 wakijeruhiwa kwenye ajali 1,422 zilizotokea.

Idadi hiyo ni ongezeko la ajali 11 zilizotokea katika kipindi cha mwaka 2021 ambazo zilikuwa 1,411.

Wakati ajali hizo zikitokea mzigo unakwenda kwenye matibabu, Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Profesa Abel Makubi, alisema asilimia 60 ya wagonjwa wa ajali, hawana bima ya afya na hushindwa kulipia huduma walizopata na serikali kubeba mzigo wa matibabu kulipia gharama.

Aidha, serikali wiki hii imebainisha kuwapo ongezeko la majeruhi watokanao na ajali wanaohitaji upasuaji katika vituo vya afya nchini, ikitoa tahadhari kwa watumiaji wa barabara kwa kufuata sheria ili kuondoa ajali zinazoweza kuepukika katika sikukuu za mwishoni mwa mwaka.

Hivi karibuni, Msemaji wa Jeshi la Polisi nchini, David Misime, alisema asilimia 75 ya ajali za barabarani zinatokana na uzembe wa madereva kutokana na ulevi wakiwa safarini na kwamba kuanzia sasa watakaopata ajali na kukutwa wamelewa moja kwa moja watapelekwa mahakamani.



Moja ya ajali mbaya zilizotokea mwaka huu ambayo iligharimu maisha ya watu.

**ZILIZOTIKISA**

Moja ya ajali zilizotikisa kwenye vyombo vya habari ndani na nje ya nchi, ni ya ndege ya Precision Air, iliyotokea Novemba 6, mwaka huu, mjini Bukoba mkoani Kagera, huku watu 19 wakifariki dunia, kwa mujibu wa mamlaka husika.

Mkaguzi Mkuu wa Ajali za Ndege kutoka Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, David Nyamwihura, alisema ripoti ya ajali za ndege nchini tangu mwaka 1920 hadi 2013 zinaonesha zimewahi kutokea 52 zilizosababisha vifo vya watu 196.

Idadi kubwa ya ajali hizo hutokea maeneo ya milimani. Ingawa ajali Precision iliyotokea Bukoba, ilikuwa katika Ziwa Victoria, mita chache kutoka Uwanja wa Ndege wa Bukoba, wakati ndege hiyo nambari PW 494 ikijiandaa kutua ikitokea Dar es Salaam kupitia Mwanza, inaweza kuingia kwenye rekodi mpya.

**VIFO WANANDOA**

Pia, wiki iliyopita watu watatu walifariki dunia wakiwamo wanandoa, ambao ni askari polisi, kutoka mkoani Arusha, Noah Semfukwe (30) na Agnes Kiyeyeu (27), katika ajali ya gari iliyotokea eneo la Tanangozi, nje kidogo ya Manispaa ya Iringa, ambayo imeingia kwenye kumbukumbu ya mwaka huu.

Kamanda wa Polisi, Mkoa wa Iringa, Allan Bukumbi aliwataja waliofariki katika ajali hiyo ni watatu wakiwamo wanandoa hao, askari wa Jeshi la Polisi, Semfukwe, aliyekuwa dereva pamoja na mkewe, Agnes.

**MAMA, WATOTO WAFARIKI**

Kadhalika, huzuni ilitawala katika familia ya Byemerwa, baada ya watoto watatu pamoja na mama yao, kufariki dunia Desemba Mosi na 3, mwaka huu, baada ya ajali, wakati wakitoka kwenye sherehe ya mahafali ya mmoja wa watoto wa familia hiyo ambaye naye alifariki dunia.

Ajali hiyo ilitokea Jumamosi iliyopita Desemba mosi, mwaka huu, maeneo ya Kibamba, waliofariki ni Immaculata Byemerwa (mama), Janeth Byemerwa (20) na Jollister Byemerwa (17) na mtoto Albert Mrema, aliyekuwa amelazwa Hospitali ya Mloganzila aliyefariki siku iliyofuata.

**WAANDISHI AJALINI**

Tukio lingine ni waandishi wa habari watano kutoka vyombo mbalimbali vya habari kufariki dunia baada ya gari walilokuwa wakisafiria, kupata ajali eneo la Busega mkoani Mwanza.

Waandishi hao ni Abel Ngapemba, Ofisa Habari Mkoa wa Mwanza; Johari Shani kutoka Uhuru Media Group; Husna Mlanzi na Athony Chuwa wa kituo cha ITV pamoja na Steven, Ofisa Habari Wilaya ya Ukerewe.

**BASI LAUA**

Mkoani Morogoro, watu 23 walipoteza maisha na wengine 34 kujeruhiwa kutokana na ajali iliyohusisha gari la abiria la kampuni ya Ahmeed, aina ya lori, katika eneo la Maleki, Kibaoni, Barabara ya Morogoro kwenda Dodoma, Machi 19, mwaka huu.

Polisi walitaja sababu ni mwendokasi wa dereva wa lori ambaye alijaribu kumkwepa mwendesha pikipiki na kujikuta akilivaa basi lililokuwa linatoka Mbeya kuelekea Dar es Salaam.

**BALOZI AJALI**

Balozi wa Tanzania nchini Austria, Celestine Mushi alifariki dunia Desemba 15, mwaka huu, baada ya gari yake kuteketea kwa moto eneo la Mkata, wilayani Handeni, mkoani Tanga akielekea Moshi kwenye sikukuu za mwisho wa mwaka.

**MWELE MALECELA, NGOWI**

Februari 10, mwaka huu, aliyekuwa Mkurugenzi wa magonjwa yasiyopewa kipaumbele katika Shirika la Afya Duniani (WHO), Dk. Mwele Malecela, alifariki baada ya kuugua kwa muda mrefu saratani ya kichwa, pia aliwahi kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu (NIMRI) kabla ya kuvuliwa wadhifa huo Desemba 17, 2026.

Dk. Mwele aliitangaza Tanzania duniani akiwa ni miongoni mwa wasomi wachache kutoka nchini kufanyakazi WHO, huku akikumbukwa kwa msimamo wake wa kile anachokiamini.

Machi 28, mwaka huu, kilitokea kifo cha Profesa wa Chuo Kikuu cha Mzumbe, Prof. Honest Ngowi, aliyefariki dunia kwa ajali ya gari iliyohusisha lori lenye kontena na gari alilokuwamo, alilokuwa anasafiria kwenda mkoani Morogoro.

Ajali hiyo ilitokea Mlandizi mkoani Pwani, ikihusisha magari matatu, yakiwamo aina ya Noah, Land Cruiser alilokuwa anasafiria na lori lililobeba kontena ambalo ndilo chanzo cha ajali, baada ya kuhama njia na kuiangukia Noah ubavuni, kisha kulalia gari alilokuwamo mchumi huyo.

Profesa Ngowi alikuwa mchumi mbobevu ambaye alitumia taaluma yake kutafsiri uchumi kwa maisha ya wananchi wa kawaida, alianzisha Ngowi TV ambayo ilikuwa na vipindi vya kuelimsha wananchi namna ya kutumia mazingira yake kukuza uchumi wake.

**KIFO DED TABORA**

Septemba 14, mwaka huu, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Igunga mkoani Tabora, Fatuma Omary na dereva wake pamoja na mwingine mmoja, walifariki dunia baada ya ajali iliyohusisha magari matatu, katika mteremko wa Inyala, mkoani Mbeya.

Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, alithibitisha kutokea kwa ajali hiyo na chanzo akidai ni uzembe wa dereva wa gari la Mkurugenzi aliyekaidi amri ya Jeshi la Polisi kusimama ili kupisha msafara wa malori.

Eneo hilo la Inyala, ambalo lilitajwa kuwa hatari, kabla ya barabara kupanuliwa huku viongozi wa dini mkoani humo wakiliombea, ilitokea ajali ilihusisha pia magari mawili, likiwamo lori la kubeba mafuta.

Idadi ya vifo katika ajali hiyo iliyotokea Agosti 16, mwaka huu, ilifikia watu 19 huku majeruhi wawili kati ya 10 hali zao zikiwa mbaya.

Taarifa ya ajali hiyo iliyohusisha lori lililobeba mchanga na kufeli breki, liliyagonga magari matatu katika eneo la Shamwengo, Kata ya Inyala mkoani humo.

Kamanda wa Jeshi la Polisi Mkoa wa Mbeya, Urlich Matei alithibitisha idadi hiyo ya vifo 19.

**KIFO CHA MREMA**

Pia mwaka huu, nyanja ya siasa iliingia huzuni baada ya kumpoteza aliyekuwa Mwenyekiti wa chama cha TLP, Augustino Mrema, aliyefarikI dunia Agosti 21, katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), alikokuwa akipatiwa matibabu.

Mrema (77), aliwahi kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani na kuwa mgombea urais kupitia NCCR-Mageuzi, ikiwa ni uchaguzi wa kwanza wa mfumo wa vyama vingi katika uchaguzi mkuu wa mwaka 1995, akitokea Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Mrema, aliwahi kuwa Mbunge wa Moshi Vijijini (CCM), Temeke (NCCR-Mageuzi) na Vunjo kupitia TLP na hadi alipofikwa na mauti alikuwa ni Mwenyekiti wa Bodi ya Parole.

**AJALI MTWARA**

Juni 26, mwaka huu, watu 10 wakiwamo wanafunzi wanane wa shule ya msingi ya King David, mkoani Mtwara, walifariki dunia wakati wakiwa njiani kuelekea shuleni, baada ya gari la shule kutumbukia shimoni katika eneo la Mjimwema.


Ajali hiyo ilihusisha gari aina ya Toyota Hiace yenye namba za usajili wa T 207 CTS ambayo ni mali ya shule hiyo.

RIPOTI MAALUM -2

# Mizizi ya moto hifadhini Kilimanjaro na yanayokwamisha vita vya kuukabili

**Na Mwandishi Wetu, aliyekuwa** MOSHI

**SEHEMU ya kwanza ya ripoti hii jana ilikuwa na ufafanuzi wa wakazi wa Mkoa wa Kilimanjaro na Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) kuhusu matukio ya moto kwenye Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro (KINAPA). Endelea na sehemu ya mwisho kujua hatua zinazochukuliwa.**




Nipashe

MKUU wa Mkoa wa Kilimanjaro, Nurdin Babu anabainisha mikakati yao ya kukabiliana na matukio ya moto kwenye hifadhi hiyo, akiwaonya wafugaji wanaoingiza mifugo yao KINAPA kwa lengo la kupata malisho, akiwa na angalizo kwamba wajiandae kupoteza mifugo hiyo kwa kuwa itauzwa kwa mnada.

"Kuanzia sasa tutataifisha mali zote, ikiwamo mifugo inayoingizwa kwenye hifadhi hii kinyume cha sheria kwa kisingizio cha kutafuta malisho.

"Pia hivi karibuni uliibuka moto kwenye Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro. Wapo wanaoingia hifadhini na kuua wanyama wadogo na kuvuna asali. Ninaonya kwa mara ya mwisho, baadaye asiwapo wa kunilaumu," anasisitiza.

**JICHO LA CAG**

Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) hayuko mbali na kinachoendelea KINAPA. Kwenye ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka 2020/21 iliyowasilishwa bungeni jijini Dodoma Aprili 12 mwaka huu, CAG Charles Kichere ameyamulika kwa kina matukio ya moto hifadhini Kilimanjaro, akipendekeza hatua nne za kuchukuliwa kuyadhibiti.

Anabainisha kuwa TANAPA haina uwezo wa vifaa na hata maandalizi kukabiliana na majanga ya aina hiyo, akifafanua kuwa kujitayarisha kwa majanga kunajumuisha hatua mbalimbali zinazochukuliwa na serikali, mashirika, jumuiya au watu binafsi ili kukabiliana vyema na athari za mara moja za majanga ya kibinadamu au ya asili.

"Mapitio yangu ya ripoti ya matukio ya moto iliyotolewa tarehe 23 Desemba 2020, iliyohusu uchunguzi wa chanzo cha moto kwenye Hifadhi ya Mlima Kilimanjaro, yalibaini hifadhi hiyo ilitumia siku sita kuanzia tarehe 11 hadi 16 Oktoba 2020 kuzuia na kuzima moto huo, ambapo kilomita za mraba 96.07 za eneo la hifadhi ziliteketea.

"Hali kadhalika, moto huo uliharibu mandhari ya uoto wa asili wa eneo la Moorland na uliua viumbe hai na kuharibu miundombinu ya mbuga ikiwa pamoja na vibanda 10 vya kitalii vyenye uwezo wa kubeba wageni 80," CAG Kichere anafafanua kwenye ripoti yake hiyo.

Anaendelea kubainisha kuwa moto huo ulisababisha upotevu wa mali zenye thamani ya Sh. milioni 993 na wakati huohuo KINAPA ilitumia Sh. milioni 221.51 kukabiliana na moto huo, hivyo serikali kupata hasara ya jumla Sh. bilioni 1.214.

"Vilevile, nilibaini kuwa mlipuko ule wa moto haukuwa wa kwanza kwenye eneo la hifadhi hiyo kwani kuliwahi kutokea matukio mengine ya moto katika vipindi tofauti miaka ya 2002, 2004, 2008, 2013 na 2016, ambapo jumla ya hekta 357,565 ziliteketea.

"Licha ya hifadhi hiyo kupata somo kutokana na mfululizo wa matukio hayo ya moto, nilibaini kuwa bado haikuwa na vifaa vya kisasa vya kuzimia moto kama vile ndege za kuzima moto.

"Pia, maofisa wake hawakuwahi kupewa mafunzo sahihi ya zimamoto ili kuwaweka sawa kwa ajili ya kukabiliana na kudhibiti majanga ya moto. Kutokuwa na vifaa vya kutosha na vya kisasa kunaifanya hifadhi ikose ufanisi wakati wa kukabiliana na majanga ya moto," CAG anatoa hadhari.

**NINI KIFANYIKE?**

Kutokana na hatari hiyo inayoikabili KINAPA na hifadhi zingine nchini, CAG Kichere anapendekeza serikali na TANAPA wachukue hatua nne, ikiwamo kufanya tathmini ya athari za milipuko ya moto na kurejesha miundombinu na uoto wa asili kwenye maeneo yaliyoathiriwa na moto.

Hatua zingine tatu kwa mujibu wa CAG Kichere ni: Kutumia satelaiti katika kubaini matukio ya moto; kuanzisha kikosi kazi cha kupambana na majanga ya asili; na kutenga bajeti na kununua vifaa vya kisasa vya kuzima moto ikiwa pamoja na helikopta kwa ajili ya kukabiliana na milipuko ya moto na ambayo itatumika kwa shughuli za doria na uokoaji hifadhini.

**TABIA HATARISHI**

Katika ufuatiliaji wake kubaini vyanzo vya matukio ya moto hifadhini, CAG Kichere anasema kuna tatizo la uvamizi pamoja na shughuli za kibinadamu ndani ya hifadhi hiyo, husuani kwenye eneo la 'Half-mile', ambalo ni eneo halali la KINAPA ililokabidhiwa kupitia Tangazo la Serikali Na. 278 la Septemba 16, 2005.

"Ninapendekeza serikali itafute njia mbadala za maendeleo ya binadamu kwenye maeneo yanayopakana au kuingiliana na maeneo ya hifadhi ili kuboresha programu za uhifadhi kwa jamii ndani na nje ya maeneo ya utalii. Serikali pia ibainishe mipaka yote ya hifadhi za taifa iliyoingiliwa na iwaondoe wavamizi," anawasilisha hoja yake.

Kwa mujibu wa CAG Kichere, kutokuwapo mitambo ya utambuzi kwenye milango ya kuingilia watalii na kuwapo kamera mbovu za usalama KINAPA, ni shida nyingine ya ziada inayochangia hujuma dhidi ya hifadhi hiyo.

"Wakati wa ziara yangu Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro mwezi Julai 2021, kwenye Mageti ya Machame, Rongai, Londolosi, Lemosho na Marangu nilishuhudia watalii wakiingia hifadhini bila mabegi yao wala wao wenyewe kukaguliwa na kuchunguzwa kwa kutumia mitambo ya utambuzi.

"Pia niliona kati ya mageti manane yaliyoko kwenye hifadhi hiyo, ni mageti mawili tu ya Machame na Marangu ndiyo yalikuwa na kamera za usalama. Zaidi ya hayo, nilibaini kuwa hata kamera zingine kwenye Geti la Machame hazikuwa zinafanya kazi.

"Ninapendekeza Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro iweke vifaa vya usalama kama vile mitambo ya utambuzi pamoja na kamera za usalama zinazofanya kazi vizuri kwenye mageti," CAG Kichere anatoa hoja.

Wizara ya Maliasili na Utalii katika hotuba yake ya makadirio na mapato na matumizi kwa mwaka huu wa fedha, inabainisha kuwa ili kukabiliana na matukio ya moto kwenye maeneo ya hifadhi, imeandaa mipango ya usimamizi na udhibiti wa moto na kuendelea kutoa elimu kwa jamii inayopakana na maeneo yaliyohifadhiwa.

Wakati TANAPA na KINAPA wakikosa vifaa vya kisasa vya kuzima moto hifadhini, Taasisi ya WAJIBU imefanya uchambuzi wa Ripoti ya CAG kwa Mwaka 2020/21 na kubaini Sh. trilioni 4.591 zimetumika serikalini katika mazingira yenye viashiria vya rushwa na pasipo kupata tija yoyote (nugatory expenditure) kwa mwaka huo wa fedha.

Kiasi hicho ambacho ni sawa na asilimia 15 ya fedha zote zilizotumika serikalini mwaka wa fedha 2020/21 zilizofikia Sh. trilioni 31.373, kingetosha kununua helikopta na vifaa vya kisasa vya kuzima moto hifadhini, pia kutoa mafunzo kwa watumishi wa KINAPA na TANAPA kukabiliana na majanga ya moto.

**USULI NA HISTORIA**

Mlima Kilimanjaro ni moja kati ya milima ambayo kilele chake hufikiwa kwa urahisi na hivyo kuwa kivutio kikubwa kwa wapanda milima kutoka kila pande za dunia. Safari ya kupanda mlima huo humpitisha mpandaji kwenye kanda za hali ya hewa tofauti kuanzia ile ya nchi za tropiki hadi aktiki.

Kwa mujibu wa tovuti rasmi ya KINAPA, hifadhi hiyo ina ukubwa wa kilometa za mraba 755 na iko umbali wa kilometa 45 kutoka mjini Moshi. Ni hifadhi inayojumuisha Mlima Kilimanjaro unaozungukwa na ukanda wa msitu wa mlimani.

Zaidi ya watalii 20,000 hupanda mlima huo kila mwaka wakiwamo wageni kutoka nje ya Tanzania. Hifadhi hiyo ilianzishwa mwaka 1973, yaani miaka 49 iliyopita.

## Watanzania watakiwa kulinda amani, upendo

**Na Steven William,**

MUHEZA

WATANZANIA wametakiwa kudumisha amani, umoja na upendo kwa kuwa ni jambo muhimu kwa maisha ya duniani yenye kuhitaji kumcha Mungu nyakati zote.

Hayo yalisemwa na Padri wa Kanisa la Katoliki, Parokia ya Kristo Mfufuka wilayani Muheza, Martine Kihiyo katika ibada ya Krismasi.

Aidha, aliwaomba waumini hao kusherehekea sikukuu za mwisho wa mwaka kwa upendo na amani.

Alisema Mungu amewapenda watu wake na ndio maana amewafikisha kufunga wakati huu wa kumaliza mwaka 2022, wanapaswa kutenda mema nyakati zote.

Alisema kwa niaba ya waumini wa kanisa hilo wanaombea amani nchi ya Tanzania kusitokee machafuko yoyote ya kuvunja amani.

Mchungaji Kiongozi wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Usharika wa Muheza, John Ndimbo katika ibada ya Sikukuu ya Krismasi alisema kuwa amani, umoja na upendo ndio jambo muhimu.

Mchungaji wa Kanisa la Anglikana Mtaa wa Madaba, Wilaya ya Muheza mkoani humo, Paul Luhinga, alisema Watanzania wana wajibu mkubwa kuombea viongozi wa nchi kwa ujumla.



Diwani wa Kata ya Orkesumet, wilayani Simanjiro mkoani Manyara, Sensei Laizer (katikati) akizungumza na wananchi wa eneo hilo juu ya kuchangia maendeleo ikiwemo madawati ya Shule ya Sekondari Simanjiro na umaliziaji wa vyoo Shule ya Msingi Orkesumet, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Tanzania yahimili uchumi licha ya UVIKO-19 na vita Ukraine

**Na Elizabeth Zaya**

TANZANIA ni miongoni mwa nchi zinazotajwa kuendelea kufanya vizuri katika kuimarisha uchumi wake kwa kipindi ambacho dunia inapitia kwenye msukosuko wa uchumi uliosababishwa na vita vya Ukraine na Russia, mlipuko wa virusi vya corona, maarufu UVIKO-19 na mabadiliko ya tabianchi.

Kila nchi kwa uwezo wake ilikuwa ikipambana kujinasua kiuchumi mwaka huu kulingana na uwezo wake na namna inavyojipanga, Tanzania nayo ilijipanga kwa namna yake katika kupambana na mtikisiko huo.

Takwimu zinaonyesha Tanzania ni miongoni mwa nchi zilizofanya vizuri katika kunusuru uchumi wake katika kipindi hiki ambacho dunia inahangaika na majanga hayo matatu ambayo yametikisa uchumi wa kila nchi.

Ripoti ya Benki Kuu ya Tanzania (BoT) iliyotolewa Novemba mwaka huu na Kamati ya Sera na Fedha, ilibainisha kuwa uchumi wa dunia umeendelea kutoridhisha na kusababisha Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) kushusha makadirio ya ukuaji wake kwa mwaka 2022 na 2023 kulinganishwa na makadirio ya awali.

Pia ilitaja mfumuko wa bei kuendelea kuwa juu ya malengo katika nchi nyingi kutokana na ongezeko la bei za bidhaa na mabadiliko ya hali ya hewa na kusababisha BoT kuchukua hatua ya kupunguza ukwasi ili kukabiliana na kadhia hiyo.

Kamati hiyo ilibainisha kuridhishwa na mwenendo wa uchumi wa Tanzania, ikieleza kuwa hadi nusu ya kwanza ya mwaka huu, uliendelea kukua na hivyo kuonyesha uwezekano wa kufikiwa kwa makadirio ya ukuaji wa asilimia 4.7 hadi mwisho wa mwaka huu.

Kwa mujibu wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), Pato la Taifa katika robo ya pili kuanzia Aprili hadi Juni mwaka huu liliongezeka hadi Sh. trilioni 45.2 kutoka Sh. trilioni 39.9 kipindi kama hicho mwaka jana.

### NENO LA REPOA

Dk. Donald Mmari ni Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Utafiti na Kupunguza Umaskini Tanzania (REPOA) ambayo miongoni mwa kazi zake kubwa ni kufanya utafiti unaolenga kuleta mbadiliko ya kiuchumi na kijamii ili kuimarisha uchumi, kutatua shida katika sekta za kilimo, viwanda, biashara, na ukuaji jumuishi unaoleta mageuzi kimaisha.

Anasema ukilinganisha na nchi za Afrika Mashariki, Tanzania imefanya vizuri kukabiliana na kutetereka kwa uchumi kulikochangiwa na UVIKO-19, vita vya Ukraine na Russia pamoja na mabadiliko ya tabianchi.

"Mfano, hata ukiangalia mfumuko wa bei, Tanzania ndiyo yenye mfumuko mdogo wa bei kuliko nchi hizo, na hata athari za UVIKO-19 siyo kubwa sana kulinganisha na nchi za Afrika Magharibi, Afrika ya Kati au nyingine, na hii ni kwa sababu uchumi wa Tanzania haukutegemea sekta moja peke yake" anasema Dk. Mmari.

Mkurugenzi huyo anabainisha kuwa mikopo ambayo nchi imechukua nayo imesaidia kwenye mzunguko wa fedha katika kukuza biashara na watu kuanza kufanya uzalishaji, ikiwamo kupanua masoko na serikali kuchukua dhamana ya kupunguza gharama ya nishati kwa kuweka ruzuku.

"Siyo kitu kidogo hicho na kuna maeneo imekopa ili kulinda uchumi, hii imesaidia sana na ndiyo maana Tanzania imeendelea kufanya vizuri katika kuimarisha uchumi wake tofauti na nchi zingine hasa za Afrika.

"Serikali imejaribu kwa kupitia BoT kushusha riba ili mikopo kwa sekta binafsi iongezeke kwa sababu sekta binafsi inapokua ndipo kunapokuwa na uwezekano mkubwa kwa wananchi kupata ajira.

"Mabadiliko ya tabianchi yameleta athari kubwa sana na kuchangia kupanda bei za chakula, tumeona serikali imejitahidi kuweka sera za kupunguza mfumuko wa bei, kuweka ruzuku kusaidia wakulima na mipango mbalimbali ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi," anasema.

### MIKAKATI SERIKALINI

Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba anasema Deni la Taifa sasa limefikia Sh. trilioni 90. Kati yake, Deni la Serikali ni Sh. trilioni 73 na lililobaki la Sekta Binafsi.

Dk. Nchemba pia amenukuliwa kwenye majukwaa mbalimbali akisema kuwa Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazosifika kufanya vizuri kwa namna inavyoshughulikia masuala ya uchumi.

"Kwa mfano kunapofanyika mikutano nje ya nchi, kati ya marais wanaoombwa kuonwa zaidi mpaka maombi yanajaa ni Rais Samia Suluhu Hassan, na hii ni kwa sababu nchi yake imefanikiwa vizuri katika masuala ya uchumi," alisema Dk. Nchemba katika mahojiano na moja ya vituo vya televisheni nchini hivi karibuni.

Alisema hakuna nchi yoyote duniani inayoweza kujenga miradi mikubwa pasi na kukopa, akisisitiza kuwa wanakopa ili kujenga uchumi imara na kwa haraka.

"Kwa mfano, ukisema uendeshe miradi mikubwa kwa fedha ya kukusanya mwenyewe, labda utumie miaka sijui mingapi huko ndipo umalize, na wakati huo watu wanataka maendeleo.

"Kuna baadhi ya mikoa watu walikuwa wanatumia siku nyingi mpaka kufika wanakokwenda, lakini mikopo imesaidia watu wamejengewa barabara, usafiri umerahisishwa, watu wamesambaziwa umeme kupitia REA (Wakala wa Nishati Vijijini), miradi ya maji, miradi imefanyika kwenye kilimo na maeneo mengine mengi.

"Zipo faida nyingi zinazotokana na mikopo hii na ninataka kuwaambia wananchi kwamba hakuna deni la siku moja. Kwa mfano, mimi nimeingia kwenye wizara hii, kuna deni la serikali ya awamu ya kwanza nimekuja kulilipa, na sisi mpaka hapa tulipo deni letu ni himilivu na hatuwezi kufika hata siku moja tukakwama," alisisitiza waziri huyo.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kuporomoka kwa maadili wazazi wasijisahau malezi

**VIONGOZI** wa dini katika nyakati tofauti za ibada ya Sikukuu ya Krismasi, wamekemea kuporomoka kwa maadili nchini na kuwataka wazazi kukumbuka wajibu wao wa malezi badala ya kuangalia shughuli ya kutafuta pesa pekee.

Wakihubiri katika mkesha na siku ya Krismasi, walilalamika kuporomoka kwa maadili kwa watoto ambao wengi wanafanya mambo kinyume na mafundisho ya dini.

Wazazi wametupiwa lawama kwa kuwaacha watoto wao wakiiga mambo ambayo ni kunyume na utamaduni na utaratibu wa kitanzania.

Matukio ya ukatili wa kijinsia yameshamiri kutokana na kuibuka kwa wingi vitendo vya watoto kufanyiwa unyama na watu wakubwa tena wengine kutoka ndani ya familia.

Wengine ni watoto wenyewe kwa wenyewe kufanyiana kwa kuiga kutoka kwenye mitandao ya kijamii au kwenye picha za ngono zinazoonyeshwa kwenye vibanda umiza.

Hali hii imeendelea kushamiri siku hadi siku na matukio hayo kuripotiwa kwenye vyombo vya habari.

Pamoja na kuwapo kwa adhabu kali kwa wale wanaowafanyia wenzao ukatili wa aina hiyo, lakini vitendo hivyo vinaendelea kuibuka na kujiuliza ni nini hasa kinachosababisha hali hiyo kuendelea.

Kama walivyoshauri viongozi wa dini, wazazi wanajukumu kubwa la kulea watoto kwa kuwafuatilia nyendo zao na kuwachunguza kila siku ili kujua kama wako sawa au kuna tofauti.

Lakini baadhi ya wazazi kutokana na kuwa na shughuli nyingi za kazi, wanajisahau na kuwaachia jukumu hilo wasaidizi wao wa kazi kuwalelea watoto wao kuanzia kuangalia kazi zao za shule, kuwaogesha na kuwapikia na hatimaye mtoto anaiga tabia anazofundishwa na mlezi wake.

Mama anaweza kuwa nyumbani amepumzika, lakini badala ya siku hiyo aonyeshe upendo kwa watoto kwa kuwa nao karibu, kuwapikia au hata kuzungumza nao kujua kama wana tatizo, hilo halifanyiki badala yake msaidizi wa kazi anayefanya kazi hiyo kila siku ndiye anayeachiwa jukumu.

Jambo hili linasikitisha na baadhi ya watoto wanapitia mateso makubwa kutoka kwa baadhi ya wasaidizi wao lakini wanaogopa kusema kwa sababu wazazi hawako karibu nao.

Watoto hao wanapofanyiwa vitu vibaya wanatishwa wasiseme na kama wakisema wataambulia kipigo na wengine kubaki na makovu mwilini mpaka mzazi akija kugundua mtoto ameshaathirika kimwili na kisaikolojia.

Baadhi ya wazazi pia wanashindwa kufuatilia nyendo za watoto wao kwa kuwaachia huru bila kuwauliza wanakwenda wapi wakati mwingine wanarudi usiku mwingi bila kuulizwa.


Malezi kwa watoto ni jambo la msingi, kama hawatalelewa kwa maadili mazuri tangu wakiwa wadogo, wakikua ni shida kurekebishwa ndio maana wazazi wengine hulalamika wameshindwa tabia za watoto wao.

Watoto wanatakiwa wafundishwe kushika imani za dini zao kwa kufundishwa kusoma vitabu vitakavyowaongoza kutenda matendo mema.

Mtoto yeyote asiyejua misingi ya dini hawezi kuwa na tabia njema na matokeo yake hujiingiza kwenye matendo mabaya ya wizi, ujambazi na pia unyama wa ukatili wa kijinsia.

Wazazi kumbukeni jukumu la kulea watoto ni lenu si la wasaidizi wenu wa nyumbani.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

Na Mwandishi Wetu

# Mwaka unakwisha jiepushe na ajali

**KUNA** imani na fikra kuwa mwishoni mwa mwaka kuna visababishi vingi vinavyoweza kuleta vifo, hata bila kutegemewa. Tena ipo imani kuwa ni kipindi cha ajali zinazotokea kitatanishi.

Kama kuna ukweli kwanini usiwe makini barabarani na maeneo yanayoweza kukatisha maisha yako kuelekea 2023.

Shirika la Afya Duniani (WHO) linakadiria watu takribani milioni 1.35 hufariki kila mwaka kutokana na ajali barabarani zinazotokea zaidi kwenye nchi za uchumi mdogo.

Aidha, hugharimu nchi hizo karibu asilimia tatu ya mapato yake na asilimia 93 ya ajali hizo hutokea mataifa maskini ikiwamo Tanzania.

Ajali huua, kuleta ulemavu, kuharibu magari, miundombinu na madaraja kwa ujumla huambatana na hasara nyingi lakini cha kutia moyo ni kwamba ajali za barabarani zinaweza kupungua na hata kuzuilika kama watu watatii sheria, kuacha ulevi, kuchati na kufanya yanayokatazwa barabarani.

Kikubwa ni kuzingatia sheria za barabarani kwa madereva ambao wanaendesha vyombo mbalimbali, raia na watumia barabara wengine wote.

Kwa mfano dereva anaendesha gari huku anaongea na simu au anachati, anafungulia mziki mkubwa lakini pia ana foni masikioni.

Kwenye bodaboda madereva wanavunja sheria kwa kupenya bila kujali taa wala trafiki anayeongoza magari.

Lakini pia wapo wafanyabiashara wanajitumbukiza na kupanga bidhaa barabarani wapendavyo. Si hivyo pia wapo wanaoziona barabara kama sehemu ya mchezo wakiegesha magari kila wanapojisikia, kutumia magari mabovu yakiwamo yasiyo na taa, vioo wala breki.

Wapo wazazi wasiowajali watoto huwaacha wazurure barabarani bila msaada na wakati mwingine hawajui nini cha kufanya. Chungeni watoto wenu wazazi na walezi hasa wakati huu wa sikukuu za mwisho wa mwaka.

Walevi nao ni chanzo cha ajali ikiwa umetumia pombe yako na hujiwezi barabara siyo sehemu salama kwako na wasafiri wengine na magari au vyombo vya moto, wanaokunywa sana jihadharini pia.

Ni vyema kukumbusha madereva kuepuka vilevi kama vile pombe, sigara , dawa za kulevya wakiendesha vyombo vya usafiri kwa sababu pia ulevi ni chanzo cha ajali, hili jambo likitekelezwa na kuzingatiwa ajali za barabarani mwishoni mwa mwaka zinaweza kupunguzwa.

Vile vile madereva wanatakiwa kuepuka matumizi ya simu wanapoendesha kwa sababu kunawapunguzia umakini na kusababisha ajali za barabarani, kwa hiyo inatakiwa tupige vita jambo hili ili ajali za barabarani zipungue hasa wakati wa sikukuu.

Wamiliki wa vyombo vya usafiri sambamba na madereva wanatakiwa kuhakikisha kuwa vyombo vyao vya usafiri vinapelekwa gereji kwa ajili ya matengenezo na uchunguzi juu ya vyombo hivyo, angalau kila wiki, huenda hili litasaidia kuwa na Tanzania isiyo na ajali za barabarani zinazoweza kuepukwa.

Lakini wauza mafuta nao wawe makini hakuna sababu ya kumwaga mafuta barabarani kwani huongeza utelezi na kutishia usalama.

Mamlaka zinazohusika na barabara kama vile TANROADS, Jeshi la Polisi na Kikosi cha Usalama Barabarani ni muhimu kuhakikisha miundombinu mibovu inarekebishwa na barabara zinakuwa imara ili kupunguza ajali za barabrani hasa maeneo ya vijijini na mijini.

Wekeni vizuizi vya kutumbukia ndani ya mito hasa kwenye madaraja na kuweka alama za utambulisho kuwa kuna daraja , kona au mteremko na zinazong'aa ili kuwaamsha madereva wasioona kikamilifu.

Madereva wazingatie alama za barabarani kama zinazowaeleza kuhusu mteremko mkali wajali na wapunguze mwendo kasi au spidi kubwa wakiwa barabarani. Wawajali wanaovuka na wanaoendesha pikipiki, baiskeli na wengine wanaoegesha magari kiholela.

'Wazee' wa pikipiki wasisahau kuvaa kofia ngumu kwa sababu usalama wa dereva na abiria kwa kiasi kikubwa upo kwenye kofia ngumu na kuzuia kifo au majeraha makubwa, hili likizingatiwa ajali za barabarani zinaweza kupungua.

Madereva waepuke kubeba mizigo kupita kiasi kwa sababu mzigo ukizidi gari linaweza kuanguka, kuangusha shehena, kuyumba na hata kuleta usumbufu barabarani.

Kuegesha magari kiholela kwenye kona, miteremko mikali, au popote dereva anapojisikia ni hatari, lakini pia kuendesha magari bila taa ni hatari zaidi kuweni makini ili mwaka 2022 usiwe wa ajali bali wenye matukio machache ya ajali za barabarani.

# Lema akumbusha kujadili mazingira

**Na Mwandishi Wetu**

ALIYEKUWA Mbunge wa Arusha Mjini, Godbless Lema amewataka Watanzania wanapokutana vijijini kwenye sikukuu za mwisho wa mwaka kujadili athari za mabadiliko ya tabianchi na kuweka mikakati ya kutunza mazingira.

Katika ujumbe wake wa Krismasi na Mwaka Mpya, Lema anayeishi Canada tangu mwaka 2020, alisema ni muhimu kwenye vikao vya familia na vijiji kujadili jambo hilo kwa kina.

"Ninashauri kwenye kikao cha kijiji tujaribu kuongea suala la mazingira. Kwani wingi wetu unapaswa kuwa na maarifa juu ya jambo hili, idadi ya watu inaongezeka sana na wakazi na ndugu wanapenda sana kuja au kurudi kuishi nyumbani.

"Hivyo maendeleo ya ujenzi wa nyumba mpya kila siku litakuwa ni jambo la kawaida katika ardhi yenye ukubwa uleule. Ni muhimu sasa kukawapo wazo la uratibu katika msingi wa kutazama mazingira. Vijiji vya Kilimanjaro milimani vinazidi kuwa vidogo kulinganisha na mahitaji ya kizazi kilicho ongezeka sana."

"Kwahiyo uratibu wa ujenzi wa nyumba unaozingatia mazingira na upandaji miti unapaswa kupewa kipaumbele kikubwa, ili kuendelea kutunza uoto wa asili tulio nao vijijini ambao pia ni silaha muhimu katika kulinda vyanzo vya maji na Mlima Kilimanjaro."

"Nilitamani kuwapo, lakini nitakaporudi nitakuwa mtu mwenye bidii hii sana katika suala la mazingira kwa maarifa na ushauri mwingi na wajibu katika kutunza mazingira na ujenzi ambao utaendelea kuweka suala hili kuwa kipaumbele. Hivyo tusisahau kabisa kuanza kuongea sasa masuala ya upandaji miti kwa vitendo," alisisitiza.

Alisema miradi hiyo inaweza kufikiriwa na kuanza sasa, wako vijana wengi vijijini hilo linaweza kufanywa kuwa ajira zao kwa uratibu.

Ikifanywa hivyo bila shaka sasa na wajukuu wataendelea kufurahia hali bora ziku zote.



John Samwel (kulia) mmoja wa wahitimu wa mafunzo ya kuwajengea uwezo wa kusimamia miradi mikubwa yaliyotolewa na kampuni ya ujenzi ya Group six International na Chongqing Vocational Institute of Engineering akisoma risala kwa niaba ya wanafunzi wenzake kwenye sherehe za kufunga mafunzo hayo yaliyofanyika jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Anayedaiwa kuua mkewe akiwa na hawara aendelea kushikiliwa polisi

**Na Neema Hussein,** MPANDA

JESHI la Polisi mkoani Katavi, linaendelea kumshikilia mtuhumiwa wa mauaji ya mke aliyetengana naye na kumfukia kwenye shimo la choo miezi sita iliyopita na mabaki yake kufukuliwa wiki iliyopita.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Katavi, Ali Makame, aliiambia Nipashe jana kuwa hatua hiyo inatokana kuendelea na uchunguzi na kuwakamata wahusika wengine wa tukio hilo, ikiamini wako wengi zaidi.

"Bado hatujamfikisha mahakamani, tunaendelea na upelelezi wetu ili kubaini mtandao mzima wa watu waliohusika, tukio kubwa kama hilo haliwezi kufanywa na watu wawili tu lazima kutakuwa na wengine wanaohusika," alisema.

Polisi pia inaendelea kumsaka mwanamke mwingine ambaye jina lake halikutajwa, aliyekuwa anaishi na mtuhumiwa wa mauaji hayo, Augustino Joseph (31), anayedaiwa kutoweka baada ya mwenza wake kukamatwa. Jeniviva Athanas (30), mama wa watoto wawili, anadaiwa kuuawa miezi sita iliyopita katika kijiji cha Kaseganyama, Wilaya ya Tanganyika, mkoani Katavi, alipoenda nyumbani kwa mumewe kupeleka watoto kumuona baba yao.

Kamanda Makame alisema, mwanamke huyo aliripotiwa kupotea miezi sita iliyopita katika mazingira tata na familia yake ilipofuatilia, ikashuku mume kuhusika na mauaji na alipohojiwa zaidi alikiri na kuiongoza Polisi kuonyesha alikoufukia mwili huo.

"Tulipokwenda kufukua, tulikuta kuna mifupa kwa sababu kipindi ni kirefu palibakia mabaki hayo ya mifupa na tukajiridhisha kuwa ni kweli, hilo tukio limetendeka na sio tu kupotea bali aliuliwa," alisema Kamanda Makame.

Wakizungumza na Nipashe kwenye maziko, Manispaa ya Mpanda, ndugu wa marehemu waliiambia Nipashe kuwa, chanzo cha mgogoro baina ya wanandoa hao ni kutokana na tukio la mke kumfumania mumewe na mwamamke aliyekuwa akiishi naye baada ya kutengana.

Alisema uchunguzi wa awali unaonyesha kuwa mwanamke (hawara) aliyekuwa akiishi na mume wa marehemu walishirikiana kumuua na mwili kuufukia kwenye shimo la choo na kuchoma nguo zake na simu ili kupoteza ushahidi.

Jeshi la Polisi linaendelea kumtafuta mwanamke huyo ambaye alikimbia na mpaka sasa hajulikani alipo pamoja na wengine ambao wanahisiwa kushiriki kufanya ukatili huo ili kuwafikisha mahakamani kujibu tuhuma zinazowakabili.

"Mimi na mwanangu tuliishi vizuri nilimuoza kwa mtu anayeishi huku Katavi, lakini baada ya miezi sita hatukuwa na mawasiliano naye nimekuja kugundua baada ya usaidizi wa polisi mtuhumiwa kutaja kuwa alimuua na kwenda kutuonyesha alipomuulia na baadaye alifukuliwa na kuonyesha viungo vyake," alisema baba wa marehemu, Ndikumwami Ndihabwa.

**KABWELA** **Na Fadhili Mohammed**





Katibu Mkuu wa kanisa la KKKT Dayosisi ya Kaskazini Mashariki, Julius Madiga (mwenye suti) akizungumza na waumini katika ibada iliyofanyika katika kanisa la KKKT Usharika wa Muheza Tanga iliyoambatana na shughuli ya watoto 47 kupata Kipaimara katika kanisa hilo, ikiwa ni sherehe ya pili ya Krismasi jana. **PICHA:STEVEN WILLIAM**

# TTCF yalia danadana marekebisho ya sheria na sera kudhibiti tumbaku

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha Kudhibiti Tumbaku Tanzania (TTCF) kimesema kuna danadana nyingi katika kurekebisha sheria na sera ya kudhibiti tumbaku nchini huku wananchi wanaotumia na wasiotumia wakiendelea kuathirika.

Mkurugenzi Mtendaji wa TTCF, Lotgard Kagaruki, akizungumza na waandishi wa habari hivi karibuni, alidai jitihada zao za kupinga matumizi ya tumbaku na matangazo ya kuhamasisha nchini zimezimwa kutokana na nguvu ya wazalishaji wa bidhaa hizo.

"Tumeshawahi kwenda kwa mawaziri tofauti na wote wanatuhakikishia sheria itakwenda bungeni, lakini zinatokea danadana, hatujui kinachoendelea na haifiki bungeni, athari ya tumbaku ni kubwa, tumeridhia mkataba wa kimataifa wa kupinga tumbaku, lakini hakuna utekelezaji.

"Kwa sasa tunaona matangazo ya kuhamasisha na kwenye baa zetu uvutaji wa shisha unashamiri kila siku na hakuna hatua zinazochukuliwa," alisema.

Msemaji wa Wizara ya Kilimo, Hudson Kamoga alipotafutwa na Nipashe kwa simu jana kuzungumzia mchakato wa kurekebisha sheria na sera ya tumbaku, alisema:

"Hao wenye malalamiko wasiishie kulalamika kwenye vyombo vya habari, milango ya wizara iko wazi, waje waonane na waziri au katibu mkuu, kama wana jambo lao litawekwa mezani na kutatuliwa."

Kwa mujibu wa Kagaruki, jitihada za kupunguza matumizi ya tumbaku zimerudi nyuma na kwamba magonjwa yasiyoambukiza yanalitesa taifa, lakini ni ngumu kusikia kiongozi anasema sababu ni tumbaku, bali watu wanaambiwa wafanye mazoezi na lishe.

"Asilimia kubwa ya wavutishwaji (wanaovuta moshi wa wanaovuta) ni kubwa sana, wako hatarini zaidi, sheria yetu inahitaji marekebisho lakini kila kiongozi anakwepa, duniani tunaonekana tofauti kutokana na kutotekeleza Mkataba wa Kimataifa wa Kudhibiti Tumbaku wenye kanuni 38 ambao tumeuridhia," alisema.

Kagaruki alisema nchi zilizoendelea zinatumia mbinu ya kupandisha bei ya bidhaa hiyo ili wanunuaji wawe wachache na ikiwa bei juu, vijana hawatamudu, lakini nchini inauzwa bei rahisi na ndiyo maana shisha inatumika kila mahali na kwa uwazi licha ya kuwa na madhara makubwa.

Alisema watumiaji wengi wa bidhaa hizo ni vijana ambao ndiyo nguvu kazi ya taifa.

"Kwa miaka mitatu bei ya sigara haijapanda, kuna madai wakipandisha wataruhusu magendo lakini ukifuatilia kwa kina siyo sababu yenye mashiko.

"Wakulima wamekuwa wavutaji bila kupenda tangu analima zao hilo hadi kuvuna na kulichoma, hakuna mtanzania ambaye hajavuta tumbaku na hasa wale wanaokwenda nyumba za starehe," alibainisha.

Alisema ni muhimu nchi ikaheshimu mkataba wa kimataifa wa kupinga tumbaku kwa kusitisha matangazo na ufadhili wa masuala ya tumbaku.

"Tuache uhusiano usio wa lazima na kampuni za tumbaku, kuwapo mwongozo wa maadili kwa viongozi wanapohusiana na kampuni hizo.

"Kilio chetu kwa serikali tunasema tunaomba uzalendo, tuweke afya mbele, tujali afya ya jamii na mazingira na tuunge mkataba mkono kwa kupitisha sheria," alisema.

Kiongozi huyo alisema wananchi wamekuwa waathirika wa tumbaku kuanzia wanaolima, wanaovuna na kuitumia ndiyo maana wamekuwa mstari wa mbele kupinga.

Mkurugenzi huyo alimkumbuka Dk. Reginald Mengi kwa kumnukuu rafiki yake Mzee Filex Mosha ambaye alieleza waombolezaji kuwa walimfuata Mengi anunue kiwanda cha tumbaku lakini alisema "hicho kiwanda kinaua watu, siwezi kuwa kwenye sigara kwa sababu ya faida hata wakinipa mabilioni". "Mimi ninasema Mungu aendelee kumlaza pema pale alipo, tungekuwa na viongozi wawili watatu kama huyu tungeshapiga hatua kubwa.

"Kama wenzetu wameweza kupiga hatua, kwanini tushindwe? Wakenya wanapenda biashara kuliko sisi kama ingekuwa na faida, wasingeiacha lakini wamefanikiwa kudhibiti na kuheshimu mkataba wa kimataifa," alisema Kagaruki.

Mkurugenzi huyo alisema walikwenda Namtumbo wakawatoa wakulima asilimia 90 kwenye kilimo cha tumbaku wameanza kupanda mazao mbadala ya mahindi, mpunga, ufuta na alizeti.

Alisema kuwa waliwakuta na nyumba zao za nyasi lakini maisha yamebadilika,wamejenga nyumba za bati na afya za watoto zinaimarika.

## Madereva, makondakta walia na mikataba inayowanyonya

**Na Christina Mwakangale**

MADEREVA na makondakta wa daladala wameeleza kwamba makubaliano ya maneno wanayofanya na wamiliki wa vyombo vya moto yanawaumiza inapotokea pande mbili hazijaelewana kwa kuwa mwenye nguvu anachukua mali yake na kumpa mwingine bila kuzingatia taratibu, jambo linalowafanya waishi kwa wasiwasi.

Wadau hao wa usafirishaji walibainisha hayo juzi walipohudhuria uzinduzi wa ripoti ya utafiti wa miaka minne uliofanywa na Chuo Kikuu Mzumbe na kuwafikia waliojiajiri kwenye sekta hiyo takribani 3,000 kwenye mikoa ya Dodoma na Dar es Salaam, kubaini iwapo wamejiunga na mifuko ya kijamii, bima na huduma za kifedha.

Ahmed Hamisi ni dereva wa daladala, akifanya safari zake kati ya Ubungo na Gongo la Mboto mkoani Dar es Salaam, alisema kwamba shughuli anayofanya haina uhakika wa kesho yake, hivyo kuwa na ugumu kujiunga na mifuko ya hifadhi ya jamii na bima na hata kuweka akiba ya fedha.

"Shughuli zetu zina changamoto na utafiti huu unabainisha namna asilimia zaidi ya 90 tuna mkataba na chombo, yaani kama ni daladala basi ndio mkataba (makubaliano) wako, kesho halipo, huna mkataba.

"Badala ya sisi kuingia mkataba na kampuni au bosi na kusainishiana karatasi, wewe kila siku unafika kwa bosi 'chombo hiki basi', na unaweza siku ukaenda asubuhi chombo hakipo kapewa mtu mwingine," anasema dereva huyo.

Aloyce Gervas, mmoja wa watafiti, alisema utafiti huo ulioanza mwaka 2017 hadi 2021, umebaini zaidi ya asilimia 90 ya vijana waliojiriwa katika sekta ya hiyo, hawana mikataba inayotambua haki zao huku waliyonayo huingia mkataba na chombo badala ya mtu.

Alisema utafiti huo ulibaini kwamba walioajiriwa kwenye kundi hilo, kwa asilimia 66 wana elimu ya msingi, huku 30 pekee wakiwa wamefikia kiwango cha sekondari na asilimia 25 wana ujuzi wa vyuo vya ufundi.

Aloyce alibainisha kwamba, kati ya waliohojiwa waliojiajiri kwenye ajira hiyo kwa asilimia 99 ni wanaume na wengi wao wana umri ulio kati ya miaka 30 hadi 32.

Ofisa Habari wa Shirikisho la Vyama vya Waendesha Pikipiki Mkoa wa Dar es Salaam, Said Msisiri alisema Mkoa wa Dar es Salaam kitakwimu una madereva wa pikipiki na bajaj wapatao 360,000.

## Waziri asherehekea Krismasi na wagonjwa

**Na Hassan Mabuye,** DODOMA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula amesherehekea sikukuu ya Krisimasi na wagonjwa kwa kula nao chakula na kukabidhi zawadi kwa kundi hilo kwenye Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma.

Alikabidhi zawadi hizo juzi kwa wagonjwa kwenye wodi ya watoto walio na changamoto ya lishe na watoto walio na changamoto mbalimbali za kiafya, wakiwamo waliopata ajali za moto na majanga mbalimbali.

"Nimeamua kuja kusherehekea sikukuu na wagonjwa kwa kuleta chakula nilichopika nyumbani kwangu, vinywaji na matunda kwa sababu ninajua leo ni sikukuu ya Krisimasi na ushiriki wa watoto ni muhimu lakini kuna ambao wameshindwa kusherehekea wakiwa nyumbani kutokana na changamoto mbalimbali za kiafya," alisema Dk. Mabula.

Waziri huyo alisema Rais Samia Suluhu Hassan ameonyesha njia kwa viongozi kusherehekea sikukuu pamoja na wananchi wenye uhitaji ambapo ametoa huduma ya vyakula kwa mikoa yote nchini kwa ajili ya Krismasi na Mwaka Mpya ili watu wote wapike na kusherehekea hata kama hawana uwezo kiuchumi.

"Na mimi ninamshukuru sana Mheshimiwa Rais kwa sababu ameonyesha njia toka jana mikoa yote amegawa vyakula kwenye vituo vya kulelea watoto kwa ajili ya sikukuu hizi za Krisimasi na Mwaka Mpya.

"Na sisi kama wawakilishi wake ni wajibu wetu kuwatembelea wahitaji, hasa watoto ndiyo maana nimeamua kuja hapa hospitalini kula nao sikukuu,' alifafanua.

Katika ziara hiyo, Dk. Mabula aliongozana na Dk. Ibenzi Ernest, Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani Mkoa wa Dodoma ambaye alimshukuru waziri huyo kwa sadaka yake hiyo ambayo alisema ina mchango mkubwa kwa mgonjwa kufarijika pale ambapo anaona watu wanamjali.

Dk. Ibenzi alitumia fursa hiyo kumwomba Waziri Mabula kufikisha shukrani zake kwa Rais kwa mafanikio makubwa ya kuboresha huduma za afya hasa katika upatikanaji wa vifaa tiba na maboresho ya majengo ya utoaji huduma za afya kwenye maeneo mbalimbali nchini. "Kwa kweli sisi watoa huduma za afya tunaipongeza sana serikali kwa maboresho mengi yaliyofanyika kuanzia ukarabati majengo, upatikanaji wa vifaa tiba vya kutosha na hata usafi katika wodi zetu, kwani zamani ilikuwa hospitali zinatoa harufu kwa kutofanyiwa ukarabati kwa muda mrefu," Dk. Ibenzi alipongeza.




Watoto yatima wanaolelewa katika kituo cha Angel House kilichopo Tarime wakifurahia zawadi ya Krismasi iliyotolewa na Mgodi wa North Mara jana (Kushoto) ni Mkurugenzi wa kituo hicho, James Masero ( wa pili kulia mwenye shati la bluu) ni Ofisa Mahusiano wa Barrick North Mara, Zachayo Makobero. Mgodi huo pia ulitoa zawadi ya Krismasi kwenye kituo cha City of Hope. **PICHA: MPIGAPICHA WETU.**

## Wanakijiji wafurahia kuvua samaki mwenye uzito Kg 200

**Na Boniface Gideon,** TANGA

WAKAZI wa Kata ya Moa wilayani Mkinga mkoani Tanga wamesherehekea sikukuu ya Krismasi kwa furaha baada ya wavuvi wa eneo hilo kumvua samaki mkubwa zaidi katika historia ya Mkoa wa Tanga.

Samaki huyo aina ya papa alivuliwa juzi mchana akiwa na uzito wa kilo 195 na kuvunja rekodi ya samaki waliowahi kuvuliwa kwenye eneo hilo. Mwaka jana walivua mwenye uzito wa kilo 160.

Mwenyekiti wa Jumuiya za Usimamizi wa Rasilimali Bahari (BMU) wa kata hiyo, Kassim Alfani, akizungumza na waandishi wa habari alisema historia imeandikwa kwa kuwa hawakuwahi kuvua samaki mwenye uzito na ukubwa wa aina hiyo.

"Tulipomvua samaki huyu na kumfanyia vipimo, tuliwasiliana na wenzetu wa wilaya zingine zenye bahari ikiwamo Tanga Mjini na Pangani ili tufahamu historia ya uvuvi wao, tunashukuru kupitia BMU wametuelezea historia yao kwa miaka ya hivi karibuni ya 2000 hakujawahi kuvuliwa samaki mkubwa mwenye zaidi ya kilo 100," alisema.

Kassim aliwataka wavuvi wa kijiji hicho kuendelea kufuata sheria na taratibu za uvuvi ili kuendelea kuvua samaki wakubwa zaidi ya huyo.

"Samaki huyu ni sehemu ya mikakati yetu BMU pamoja na wavuvi wetu ya kutunza rasilimali bahari ikiwamo kuzuia uvuvi haramu na kuzuia shughuli haramu baharini kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama wakiwamo askari wa KMKM ambao wametusaidia sana kuhakikisha bahari yetu inakuwa tulivu.

"Hali hii inawavutia samaki wakubwa kusogea karibu, hivyo tutaendelea kusimamia rasirimali bahari kwa manufaa ya jamii yetu," alisisitiza Kassim.

Diwani wa Moa, Sitaruki Bwago alisema kuvuliwa samaki huyo ni matokeo makubwa ya elimu ya utunzaji rasilimali bahari ambayo wameiwekeza kwa miaka mitano iliyopita.

"Haya ni matokeo ya uwekezaji wa elimu ya utunzaji rasilimali bahari, elimu hiyo tumeiwekeza kwa miaka kadhaa sasa hivi ingawa awali tulipata shida kutokana na kwamba wavuvi na wananchi walikuwa hawataki, waliamini tunawazuia kufanya shughuli zao lakini kwa sasa wamekuwa mstari wa mbele kuhakikisha bahari inakuwa tulivu muda wote na wanatusaidia ulinzi dhidi ya wanaofanya uharamia,"alifafanua.

Bwago alisema kwa siku za hivi karibuni wavuvi wamekuwa wakivua samaki wengi ambao walikuwa wadogo na wengi ni dagaa maarufu kama uwono, lakini baada ya kuimarishwa kwa vyombo vya ulinzi na usalama pamoja na wavuvi, hali imebadilika na sasa samaki wakubwa wanapatikana kwa wingi.

"Ujio wa KMKM umetusaidia sana kuleta matokeo makubwa ya uvuvi, mfano zamani dagaa maarufu kama uwono ndiyo walikuwa wakivuliwa zaidi, lakini hivi sasa samaki aina ya bangala ambao ni wakubwa wanavuliwa wengi zaidi, lakini pia wanauzwa kwa bei kubwa na kiukweli imechangia kuongeza kodi kwenye wilaya yetu na kata yetu ndiyo inaongoza kwa mapato mengi ya halmashauri na chanzo kikuu ni shughuli za uvuvi na utalii wa fukwe," alifafanua.

Aliwataka wananchi na wavuvi kuendelea kutunza rasilimali bahari ili kupata matokeo makubwa zaidi ya hayo.

"Kama tumefanikiwa kuweka ulinzi kwa zaidi ya asilimia 90 na leo hii kata yetu inavunja rekodi, basi ninaamini tuna uwezo wa kuwa matajiri kupitia shughuli hizi kwa kutunza rasilimali bahari.

"Niwaombe wavuvi, wananchi tutunze rasilimali hizi ili vizazi vyetu vipande matunda haya lakini pia maisha ya wananchi yabadilishwe kupitia shughuli hizi za uvuvi," alisisitiza Bwago.

## Mkuu wa Wilaya ataka marekebisho gati

**Na Julieth Mkireri, MAFIA**

MKUU wa Wilaya ya Mafia mkoani Pwani, Martin Ntemo ameitaka Mamlaka ya Bandari (TPA) kulifanyia marekebisho gati la kupitisha abiria wilayani humo kutokana na uchakavu unaotishia maisha ya watumiaji wake. Amebainisha kuwa gati hilo kwa sasa mbao zake zimechakaa kiasi cha kupoteza ubora wa kuhimili abiria wanaopita pamoja na vyombo vya moto.

Ntemo alitoa maelekezo hayo juzi baada ya kutembelea na kukagua gati hilo, akisisitiza mamlaka hiyo kutoa kipaumbele cha marekebisho, ili kuepusha madhara yanayoweza kutokea endapo hatua za haraka hazitachukuliwa kurekebisha dosari zinazoendelea kujitokeza.

Alibainisha kuwa mbao kwenye njia ya gati la kupitisha abiria na magari wanapokwenda kupanda vyombo vya usafiri kisiwani Mafia, zimechaa kiasi cha kuhatarisha usalama wa watumiaji wake.

"Nimetumia mapumziko ya sikukuu ya Krismasi kukagua gati hili ambalo ni kiungo muhimu cha kusafirishia abiria kwenye vyombo vya usafiri wa baharini hasa pale maji yanapokuwa yamekupwa na kufanya vyombo vya usafiri kulazimika kuegeshwa mbali na fukwe. Nimejionea hali halisi, daraja linahitaji matengenezo ya haraka," alisema Ntemo.

Aliongeza kuwa ni muhimu kuzingatia matumizi ya teknolojia mbadala kwa matengenezo ya sehemu ya kupitisha magari kwa kuondoa mfumo wa kutumia mbao ambazo ni ghali na siyo rafiki wa mazingira badala yake yatumike mabati maalum ya madaraja ambayo hupunguza kelele pale magari au pikipiki zinapopita juu yake.

Gati hilo lenye urefu wa kilomita moja, lilifunguliwa rasmi na Rais wa Awamu ya Nne, Jakaya Kikwete mwaka 2013 likigharimu zaidi ya Sh. bilioni 20.

# 'Maofisa waharibifu vyanzo vya maji wachukuliwe hatua'

**Na Elizabeth Zaya**

KITUO cha Wanahabari Watetezi wa Rasilimali na Taarifa (MECIRA) na Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), wameiomba serikali kuwachukulia hatua maofisa wa serikali wanaokodisha maeneo ya vyanzo vya maji na uhifadhi wa mazingira kwa ajili ya masilahi yao binafsi.

Alisema baadhi ya viongozi wamekodisha maeneo ya hifadhi za mazingira na kutoa hatimiliki za watu kuendesha shughuli zao katika maeneo hayo na kwamba ni vyema serikali ikaangalia namna ya kuchukua hatua ikiwamo kuwaondoa ili kunusuru vyanzo hivyo vya maji na uhifadhi wa mazingira.

"Na wanawaingiza 'mkenge' hata viongozi wakubwa kwa kuwapatia maeneo hayo kinyume cha sheria huku wakifahamu kwamba sio sahihi, nchi hii ina maeneo mengi ni vyema serikali ikafanyia kazi na hili kama ambavyo imeamua kulishughulikia ili tusipate matatizo makubwa kama tulivyoshuhudia tatizo la maji na umeme," alisema Mwenyekiti wa TEF, Balile.

"Baadhi yao waliopewa kwenye maeneo hayo wanafanya shughuli hizo tofauti na vibali vyao walivyopewa, baadhi wanalima badala ya kufuga na wanaingiza mifugo ya wafugaji. Kwa mfano mto wa Kilombero, wanaofanya shughuli zao mle ni watu wakubwa, tunaendelea kusema haya ili serikali ifanye uchunguzi na ichukue hatua kwa sababu bila kufanya hivyo, hawa vigogo wataendelea kuendesha shughuli zao na kuharibu mazingira."

Alitoa mfano kwa waliopewa vibali kujenga matuta Mbarali mkoani Mbeya na Kilombero mkoani Morogoro na kuzuia maji kupita kwenye mkondo wake kwa kuelekeza kwenye mashamba yao bila kujali inaleta athari kwa idadi kubwa ya wananchi wanaotegemea vyanzo hivyo vya maji na hata kuchangia upungufu wa maji katika Mto Ruaha Mkuu.

Balile alipongeza hatua ya serikali kuanza kuchukua hatua ya kuagiza wote wanaoshiriki katika uharibifu huo kwenye vyanzo mbalimbali vya maji na uhifadhi wa mazingira nchini.

"Wiki iliyopita sisi wanahabari tulikuwa na kongamano kubwa lililofanyika mkoani Iringa la kujadili suala hili, tunaipongeza sana serikali kupitia kwa Rais Samia Suluhu Hassan kwa hatua ya haraka aliyoichukua ya kudhibiti suala hilo na kutilia mkazo kwa kauli aliyoitoa Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango ambaye alikuwa mgeni rasmi katika kongamano hilo, hii inatia moyo sana na tunaahidi kuendelea kushirikiana na serikali katika hili," alisema Balile.

"Hatuwezi kuacha hifadhi za mazingira na vyanzo vya maji vikiendelea kuharibiwa wakati athari zake zinapokuja zinamgusa kila mtu, kama ni shida ya maji wote ilitukumba haikuchagua mtu."

Mwenyekiti wa MECIRA, Habib Mchange, alisema wanahabari wameamua kutobaki nyuma na kuwa kama watazamaji kuona vyanzo hivyo vinaharibiwa.

"Kwa hiyo tutatumia kalamu zetu kuelimisha, kuonyesha serikali wapi pana tatizo ili ichukue hatua stahiki kwa sababu tukisema na sisi tuache athari katika miaka ijayo itazidi kuwa kubwa".



Mkuu wa Wilaya ya Mafia, Mhandisi Martin Ntemo (katikati aliyevaa kofia) akiangalia moja ya maeneo ambayo mbao zimepasuka katika gati la Mafia. **PICHA: MARGARET MKIRERI**

# Askofu atabiri neema 2023

**Na Francis Godwin,** IRINGA

ASKOFU wa Kanisa la Kiinjilila Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Iringa, Dk. Blaston Gavile amesema kuwa mwaka 2023 una dalili za mafaniko mengi ya mwili na rohoni, huku akihimiza watu kuweka akiba na kuwa na tahadhari kwenye matumizi.

Kiongozi huyo aliyasema hayo juzi wakati akitoa salamu za Krismasi katika ibada iliyofanyika Usharika wa Iringa Mjini.

Alisema mwaka ujao utakuwa wa neema kubwa, lakini ni muhimu wananchi kutumia vyema mvua zinazoendelea kunyesha kupanda mazao badala ya kuandaa mashamba.

"Kama wachungaji, ninaweka angalizo mwaka ukiwa na neema, wengi tunajisahau na kuona ni haki yetu kupata mema, bado ninasisitiza tuweke akiba tutunze, sisi kwa sisi tuombeane uzima kama familia," alihimiza.

Pia alitaka kila mmoja kuweka akiba ya chakula atakachokipata ili kuwa na akiba endelevu ya chakula, akifafanua kuwa chakula kikitunzwa vizuri, mvua ikichelewa wananchi watakuwa na akiba ya chakula na kuondoa hofu.

Dk. Gavile alisema maandalizi mema ya familia yanapaswa kwenda sambamba na maandalizi mazuri ya kuwaandaa watoto vizuri kwa ajili ya shule ili wapate elimu sahihi na wasome katika kujiandalia maisha ya baadaye.

Aliwataka watanzania kuendelea kuombea taifa na Rais Samia Suluhu Hassan pamoja na watendaji kazi wenzake ili nchi iendelee kuwa na amani na mshikamano.

Pia aliitaka jamii kukemea na kupinga ukatili wa kijinsia ambao umeshika kasi mkoani humo na maeneo mengine nchini, ukiwaathiri zaidi watoto na wanawake.

Alionya kuwa bila jamii kulishughulikia tatizo hilo, hali itazidi kuwa mbaya na kuwa na kizazi chenye ukatili.

## Wakulima wa pamba waingia makubaliano kuchangia pembejeo

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAKULIMA wa zao la pamba nchini wameingia makubaliano ya kila mmoja kuchangia kiasi cha Sh. tano kwa kila kilo moja ya pamba wanayozalisha, ili kutunisha mfuko wa pembejeo utakaotumika kununua pembejeo wakati zitakapochelewa zinazotolewa na vyama vya ushirika.

Mwenyekiti wa Mradi wa Pamoja wa Vyama Vikuu vya Pamba (TANCCOOPS), Zainabu Mahenge aliyabainisha hayo jana wakati akitoa taarifa ya hali ya kilimo cha zao hilo kwenye Mkutano Mkuu wa 27 wa Chama Kikuu cha Ushirika Kahama (KACU) uliohudhuriwa na viongozi mbalimbali akiwamo Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Festo Kiswaga.

Alisema ili zao hilo lisiendelee kushuka kila msimu kutokana na ukosefu wa pembejeo na viuatilifu, wameona kuna haja kila mkulima anayelima zao hilo kuchangia Sh. tano kwa kila kilo moja ambazo zitatumika kununua pembejeo na kuwagawia wakulima.

Mahenge alisema zao hilo linalimwa kila mwaka mwezi Novemba, hivyo kupitia mfuko huo watanunua pembejeo mwezi Septemba na kuzifikisha katika vyama vya msingi 14 vilivyopo nchi nzima na wakulima watachukua kwa kadri ya mahitaji yao.

"Kinachosababisha kushuka kwa zao hili kila msimu ni ucheleweshaji wa pembejeo za kupandia, kukuzia na viuatilifu. Sisi kupitia mfuko huu tutanunua pembejeo zote mwezi Septemba na kuzifikisha kwenye AMCOS zote," alisema Mahenge.

Mwenyekiti wa KACU, Hamisi Majogoro alisema amefurahishwa na uanzishaji wa mfuko huo, akiamini utasaidia kukidhi haja ya pembejeo za zao hilo hususani pale zitakapochelewa zile zinazotolewa na vyama vya ushirika na kuwataka wakulima kuchangia kiasi hicho.

Alisema anasubiria maelekezo kutoka kwa wasimamizi wa zao hilo kwa maandishi na atakapoyapata na kuyapitia atayapitisha, ili wakulima wake wa pamba wachangie kiasi hicho kwa lengo la kukuza zao hilo na kuhakikisha linawanufaisha wote kwa pamoja. Mmoja wa wakulima wa zao hilo, Ahmed Nambo alisema wanalima mashamba makubwa ya pamba na wanapata pembejeo za kukuzia na kupandia, lakini viwatilifu vinakosekana na kusababisha mimea kushambuliwa na wadudu na kukosa mavuno ya kutosha.

Mkulima Simon Nzengo alisema wako tayari kuchangia kiasi hicho kwa kuwa pembejeo na viwatilifu vitakavyonunuliwa kupitia mfuko huo vitasaidia mazao yao kustawi huku akiwashauri wakulima wenzake kuchangia na kulima zaidi kwa sababu hitaji lao litakuwa limeshatatuliwa.





## Zaidi ya wanafunzi 7000 kupangiwa kidato cha kwanza

**Na Allan Isack,** ARUMERU

MKUU wa Wilaya ya Arumeru, Richard Ruyango, amesema serikali itahakikisha wanafunzi 7,856 waliofaulu mtihani wa darasa la saba mwaka huu, wanapangiwa shule za sekondari kwa ajili ya kujiunga na kidato cha kwanza mwakani.

Ruyango, aliyasema hayo jana katika Halmashauri ya Arusha, wilayani humo, wakati wa hafla ya makabidhiano ya vyumba 38 vya madarasa, vilivyojengwa kwa ajili ya kupokea wanafunzi wa kidato cha kwanza Januari 2023.

Alisema kutokana na uwapo wa vyumba vya madarasa 134, ambavyo serikali imejenga kwa miaka miwili mfululizo vitawezesha idadi hiyo ya wanafunzi kuanza masomo kwa wakati. "Mwishoni mwa mwaka 2021 tulipokea Shilingi bilioni mbili tukajenga vyumba 96 vya madarasa na mwaka huu, tumepokea Sh. milioni 769 kujenga vyumba 38 kwenye shule 18 zilizokuwa na upungufu na madarasa yatatumika kwa wanafunzi wa kidato cha kwanza wa mwaka 2023," alisema Ruyango.

Hata hivyo, amewataka viongozi wote kusimamia na kuhakikisha wanafunzi waliopangiwa kujiunga na elimu ya sekondari, wanaanza masomo ifikapo Januari 9, mwaka 2023.

Aliwataka walezi na wazazi wa wanafunzi kuwapatia mahitaji yao ya msingi ya shule kama yalivyoorodheshwa kwenye fomu za kujiunga na shule hizo.

Naye Mwenyekiti wa Halmashauri ya Arusha, Ojungu Salekwa, alisema serikali imejitahidi kutekeleza majukumu yake na iliyobaki ni kuhakikisha wanafunzi waliopangiwa kujiunga na kidato cha kwanza wanakwenda shule kama walivyochaguliwa. "Serikali imeshafanya kazi kubwa ya kutekeleza majukumu yake ya msingi, kilichobakia ni sisi viongozi kuhakikisha wanafunzi waliopangiwa wanajiunga na shule na kuanza masomo kwa wakati, lakini kwa wazazi na walezi tunapaswa kuwapa watoto wetu mahitaji yote ya shule," alisema Ojung'u.

Joshua Augustino, mwanafunzi anayeingia kidato cha pili, katika Shule ya Sekondari ya Mringa, ameishukuru serikali kwa kuwajengea madarasa mazuri na aliahidi kuwa atasoma kwa bidii ili kufikia malengo na kuja kulitumikia taifa lake la Tanzania.

Mwenyekiti wa Bodi ya Shule ya Sekondari ya Mringa, Jackson Mollel, alisema kazi iliyofanywa na serikali ni kubwa na inathamani kwa watoto na vizazi vya sasa na vijavyo kwa kuwa imewapunguzia wananchi mzigo wa kuchangia ujenzi wa madarasa kutokana na michango hiyo kusuasua na kushindwa kukamilisha darasa hata moja kwa wakati.

# Operesheni hifadhi Mlima Bokwa yahusishwa na rushwa

**Na Dege Masoli,** KILINDI

OPERESHENI ya kuzuia shughuli za kilimo katika Hifadhi ya Mlima Bokwa, Wilaya ya Kilindi, mkoani Tanga, imechukua sura mpya baada ya baadhi ya wakulima kuihusisha na rushwa.

Zaidi ya ekari 400 za hifadhi hiyo zilizoko Kata za Songe na Bokwa, ndizo zilizoathiriwa na shughuli za binadamu.

Haji Ramadhan, mkazi wa Kijiji cha Kwamba alisema, "Hatukatai kuhamishwa, lakini kinachotukwaza ni baadhi ya wenzetu kupendelewa kwa sababu ya rushwa."

"Hili agizo la Mkuu wa Wilaya la kuzuia watu wasilime katika mlima huo ni kama limegeuzwa dili na baadhi ya viongozi ambao wanachukua pesa."

Kutokana na tuhuma hizo, wananchi hao wamemuomba Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Omar Mgumba, kuingilia kati.

Baadhi ya wakulima katika Kijiji cha Vilindwa, tofauti na wenzao wa Kijiji cha Songe wameendelea kufanyakazi bila ya kuchukuliwa hatua zozote.

"Tupo zaidi ya watu 600 wakazi wa vijiji vya Kwamba, Songe, Vilindwa na Bokwa tuliokuwa tukilima mlimani wote tulishushwa, lakini baadaye wenzetu wa Vilindwa walikaidi na kwenda kupanda mazao, lakini hakuna hatua zozote dhidi yao, je? na sisi tukapande," alihoji Fatuma Idd, mkazi wa Songe. "Hapa kuna harufu ya rushwa, haiwezekani eneo hilohilo wengine walime na wengine wasilime kuna nini hapa kama sio rushwa? Kama si hivyo basi uongozi wa kata umeshindwa kuisimamia operesheni hii," alisema Bimsekwa Omar, mkazi wa Bokwa.

Akizungumzia tuhuma hizo, Mwenyekiti wa Serikali ya Kijiji cha Kwamba, Abdi Makinda, alikiri kupokea malalamiko hayo na kuutupia lawama uongozi wa kata hiyo kwa kushindwa kufika kwenye mkutano wa hadhara aliouitisha kwa ajili ya kupata majibu ya madai ya wananchi hao.

Diwani wa Kata ya Songe, Abubakari Makengwa, alidai kuwa inawezekana kuwapo kwa wakaidi hao ambao alisema hawajabainika kutokana na ukubwa wa eneo hilo.

Akijibu tuhuma hizo, Ofisa Mtendaji wa kata hiyo, Ramadhan Dhahabu, alisema walishafanya ziara maeneo ya mlima huo na kueleza kuwa zaidi ya ekari 400 zilizolimwa hazijapandwa kutokana na agizo hilo.

Ingawa alikiri kuwapo kwa maeneo yaliyopandwa katika kijiji cha Vilindwa, kwa madai kuwa serikali ya kijiji hicho ndiyo iliwapotosha wananchi hao baada ya kuweka vibao vya mipaka katika maeneo yasio sahihi.

"Awali viongozi wa Kijiji cha Vilindwa waliweka vibao vya mipaka ndani ya hifadhi hiyo na kuwaaminisha waliokuwa wakilima kuwa wapo nje ya ramani, na sisi tulilibaini hilo tulipofanya ziara ya uhakiki na Mkuu wa wilaya na kukuta watu wanapalilia mahindi ndani ya hifadhi," alisisitiza Dhahabu.



Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, Kiria Laizer (kushoto) akimkabidhi Mwenyekiti wa CCM Kata ya Terrat, Soipey Koromo, kadi mpya za kielektroniki kwenye ziara yake ya kushukuru kuchaguliwa na kukagua uhai wa chama juzi.
**PICHA: GIFT THADEY**

# Wananchi watengua uamuzi wa kuhamia Korogwe

**Na Oscar Assenga,** KOROGWE

WANANCHI wa Kijiji cha Kwemasimba, Wilaya ya Korogwe, wametengua azimio lao la kutaka kuhama kutoka halmashauri hiyo kwenda Halmashauri ya Mji Korogwe, baada ya serikali kutatua tatizo la uhaba wa maji lililokuwa likiwakabili kwa muda mrefu.

Kwa zaidi ya miaka 10, wananchi hao walikuwa wanataka kuhamishwa kiutawala kwenda Kata ya Mtonga, Halmashauri ya Mji Korogwe ili kupata huduma za kijamii ikiwamo maji, umeme, barabara na zahanati.

Akitangaza kutengua azimio hilo juzi, Mwenyekiti wa Kitongoji cha Mbaramo, Suleiman Mshihiri, alisema wananchi wake wamefurahishwa na utekelezaji wa mradi wa maji uliotekelezwa na Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA), kwa kuwa sasa hawaendi kuhemea maji nyakati za usiku.


Mshihiri alitoa hakikisho hilo mbele ya Meneja wa RUWASA, Mkoa wa Tanga, Upendo Lugongo, aliyekwenda kijijini hapo kukagua mradi wa maji, ambao baadhi ya vituo ya maji (vilula) vimeanza kutoa maji.

Alisema kwamba hivi sasa wameondoa tishio la kutaka kuondoka Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe kwenda Halmashauri ya Mji Korogwe, kwa sababu serikali imeanza kuwapelekea huduma za jamii, baada ya kuanza kupata maji ya bomba. Mjumbe wa Kamati ya Mazingira ya Kijiji cha Kwemasimba, Godfrey Kidudu, alisema kwa sasa wanachotaka kwenye kijiji chao ni huduma za jamii na sio ahadi zisizo na majibu. Akizungumza na wananchi wa kijiji hicho, Meneja huyo wa RUWASA, Upendo Lugongo, aliwataka wananchi kutunza vyanzo vya maji, kwa kuwa miradi hiyo ya maji inayojengwa itakuwa haina faida kama vyanzo vya maji vitakuwa vimekauka, hivyo viongozi wa vijiji washirikiane na wananchi kutunza vyanzo hivyo.

"Nimefurahi hapa kuona kuna viongozi wa mazingira. Tunaomba viongozi wa mazingira kuwahamasisha wanafunzi kuanza kupenda kutunza mazingira kwa kupanda miti. Mtu ana watoto watano, kila mtoto unampa mti wa kupanda kuzunguka nyumbani kwao, hiyo itasaidia kurudisha uoto wa asili," alisema Mhandisi Lugongo.

"Mradi huu hadi kukamilika kwake, utagharimu Sh. milioni 481. Utakuwa na tangi lenye ujazo wa lita 75,000 na vituo vya kuchota maji vipatavyo 10.

"Kwa sasa wananchi 2,731 watanufaika na mradi huu, lakini uwezo wa mradi huo ni kuhudumia wananchi 4,313, hivyo utakuwa na uwezo wa kuhudumia wananchi hadi mwaka 2041," alisema.



# Wimbi wadudu waharibifu wa mazao laibuka Babati

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

WAKULIMA wa kata ya Kiru na vijiji vya jirani katika Halmashauri ya Wilaya ya Babati, mkoani Manyara wamesema limeibuka wimbi kubwa la wadudu waharibifu wa mazao maarufu kama Mbilizi ambao wanatishia uhai wa mazao.

Hali hiyo ilielezwa jana na baadhi ya wakulima kwa nyakati tofauti walipozungumza na Nipashe.

Aliyekuwa Mbunge wa Babati Vijijini awamu iliyopita, Vrajil Jituson, alisema wadudu hao ni wengi Bonde la Kiru.

"Hii kitu ikianza kwenye mahindi na mazao mengine italeta njaa na hawa wadudu tumeanza kuwaona hii ni siku ya tatu," alisema Jituson.

Aidha, alisema wakulima wakubwa wameshaanza kupiga dawa za visumbufu hivyo vya mimea ili kuepusha madhara.

Alisema wadudu hao wakipita mahali majani yanaanza kunyauka kama vile walikuwa wanapita ng'ombe.

Kadhalika, alisema tayari wameanza kupiga dawa hawaisubiri serikali na kuna haja ya kutoa taarifa kwa mamlaka za serikali zikajua na kuanza kutafuta mbinu za kuwatokomeza wadudu hao.

Mkazi wa Kijiji cha Daghailoy, Janeth Isaya akizungumzia wadudu hao alisema, sio mara ya kwanza kujitokeza hasa mvua inapoanza kunyesha.

Alisema Mbilizi wanaingia kwa makundi makubwa na kushambulia mimea ya aina zote bila kujali ni aina gani.

Alisema adudu hao wakijitokeza mwaka unaofuata wakulima wanapata mazao ya kutosha kitu ambacho anadai huwashangaza wengi.

Naye Kaimu Ofisa Kilimo wa Mkoa wa Manyara, Samwel Dahaye akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu alikiri wadudu hao kuwapo maeneo mengi ya Kiru na Kijiji cha Daghailoy na kudai wanaitwa viwavijeshi vamizi, lakini wakulima wamezoea kuwaita Mbilizi.

Dahaye alisema wadudu hao ni wengi wanajazana kwenye mashamba kama inzi.

Mtaalamu huyo wa kilimo alisema wadudu hao wanajificha kwenye udongo na mvua ikinyesha wanatoka na waliingia miaka mitatu iliyopita.

"Viwavijeshi vamizi vilipoingia mwaka wa kwanza heka heka za kuvidhibiti zilikuwa nyingi sana," alisema Dahaye.

Ofisa kilimo huyo alisema njia pekee ya kuondoa wadudu hao ni wakulima kuchukua hatua za haraka kupiga dawa ambazo watashauriwa na wataalamu kutoka maduka ya pembejeo.

"Wadudu hawa wanaishi kipindi kifupi baada ya mvua kunyesha na mvua ikipungua wanajifukia kwenye udongo,"alieleza

Vile vile alisema njia nyingine ya kuwadhibiti ni wakulima kuwa wanakagua mashamba yao mara kwa mara na kupiga dawa kwenye kiini cha mche ili uweze kuendelea kustawi.

Awali, wadudu hawa wakati wanaanza kuingia nchini ilielezwa na Wizara ya kilimo kuwa wanakula mimea zaidi ya 80 na wanaharibu zaidi mimea jamii ya nafaka ingawa kama hayapo wanaharibu pamba.



Waumini wa Kanisa la KKKT Usharika wa Muheza mkoani Tanga wakitoka katika ibada ya Krismasi ya pili jana kuelekea nyumbani ambapo ibada hiyo iliambatana na shughuli ya watoto 47 kupata Kipaimara katika kanisa hilo. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Sita wazaliwa Sikukuu ya Krismasi Arusha, Manyara

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

WATOTO sita wameripotiwa kuzaliwa katika Hospitali mbili wakati wa mkesha wa kumbukumbu ya kuzaliwa Yesu Kristo ambapo watoto wanne wamezaliwa Hospitali ya Mission Dareda na wawili wamezaliwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Manyara.

Akizungumza na Nipashe, Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Mission Dareda Dk. Joseph Lori alisema katika hospitali hiyo walizaliwa watoto wanne.

Dk. Lori alisema watoto wawili walikuwa wakiume na wengine wawili wa kike ambapo mtoto aliyezaliwa na uzito mkubwa kati ya hao alikuwa ni wa kike na uzito wake ulikuwa kilogramu nne na aliyekuwa na uzito wa chini kati ya hao ni wa kiume aliyekuwa na kilogramu 2.8.

Aidha, Dk. Lori alisema uzito wa kilo 2.8 unafaa kwa kuwa unaotakiwa kitaalamu ni kuanzia kilogramu 2.5.

Alisema watoto wanaozaliwa na uzito pungufu shida kubwa wanakuwa wanazaliwa kabla ya kufikisha siku zao.

"Shida nyingine inakuwa kondo la nyuma la mama anakopata chakula mtoto hapati cha kutosha," alisema Dk. Lori.

Vile vile, alisema mtoto kuzaliwa akiwa na uzito pungufu unaweza kuwa unasababishwa na wanawake wanaokunywa pombe au wanaovuta sigara wakati wakiwa wajawazito.

Dk. Lori alisema mjamzito anayeishi kwenye mazingira ya moshi wa sigara ni hatari kwa kuwa naye anakuwa sehemu ya uvutaji wa sigara.

Alisema ili mjamzito aepushe madhara hayo kwa mtoto ni vizuri aanze mapema kuhudhuria kliniki ili apate ushauri wa kitaalamu.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Manyara, Dk. Catherine Magali, alisema watoto waliozaliwa usiku wa kuamkia Noeli walizaliwa wawili wa kiume mmoja ambaye alikuwa na uzito mkubwa wa kilogramu 3.7 na wa kike aliyekuwa na uzito wa kilogramu 3.4. Kwa mujibu wa taarifa za madaktari hao, afya za watoto na wazazi wao zinaendelea vizuri.

Sera ya Afya ya mwaka 2007 inaeleza kuwa serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi inayotoa huduma bila faida na mashirika ya kimataifa itaendelea kutoa huduma bila malipo kwa wajawazito, watumiaji wa huduma za uzazi wa mpango na watoto wenye umri chini ya miaka mitano.

# Wananchi vijiji vinne kunufaika mradi wa maji

**Na Hamida Kamchalla,** LUSHOTO

ZAIDI ya wananchi 6,239 katika vijiji vya Irente, Yoghoi, Ngulwi na Bombo wilayani Lushoto wanatarajiwa kunufaika na mradi wa maji na kuondokana na kero ya upatikanaji wa huduma hiyo kwa muda mrefu katika maeneo hayo.

Kauli hiyo ilitolewa na Meneja wa Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira (RUWASA), Wilaya ya Lushoto Mhandisi Erwin Kayetan juzi kuwa mradi huo utagarimu zaidi ya Sh. milioni 578 hadi kukamilika. Aliyasema hayo baada ya Meneja wa RUWASA, Mkoa wa Tanga Mhandisi Upendo Lugongo kufanya ziara ya kukagua miradi ya maji wilayani humo.

Kayetan alisema mradi huo unahusisha vilula (vituo vya kuchotea maji) 17, ukarabati wa matangi mawili yenye ujazo wa lita 175,000 kila moja na jingine la lita 50. Pia ujenzi wa chanzo kipya na ulazaji wa bomba mita 13,500.

"Mradi wa Maji wa Irente-Yoghoi-Ngulwi-Bombo utanufaisha wananchi 6,239 ambapo hadi kukamilika kwake utagharimu Sh. 578,175,639, na utakuwa na vilula 17, ukarabati wa matangi mawili ya lita 175,000 kwa kila moja na tangi lingine la lita 50," alisema.

"Pia ujenzi wa chanzo kipya, na ulazaji wa bomba umbali wa mita 13,500 chini ya Mkandarasi Buzubona & Sons Company Ltd wa Karagwe, Kagera. Mkataba unaisha mwishoni mwa mwezi Januari, 2023,"alisema Kayetan.

Kayetan alisema kwenye mradi wa maji wa Funta katika halmashauri ya Bumbuli wilayani Lushoto utakuwa na vilula 23, na wakazi 4,782 watanufaika, na utagharimu Sh. 832,655,200 hadi kukamilika. Pia, alisema utahusisha ujenzi wa tangi lenye ujazo wa lita 90,000 ujenzi wa chanzo kipya na ulazaji wa bomba mita 9,900, huku Mkandarasi akiwa ni KOBERG Construction ltd, mkataba unaisha mwishoni mwa Mei, 2023.

Mhandisi Lugongo alisema RUWASA ipo tayari kuendelea kuongeza mahitaji ya matangi kwenye Kata ya Ngulwi ili wananchi wawe na ari ya kuchangia gharama ya huduma ya maji na kufanya miradi iwe endelevu.

"RUWASA ipo tayari kuongeza mahitaji ya matangi kwenye kata hii ili mradi wananchi wachangie gharama ya maji na miradi iwe endelevu na wao kuendelea kupata huduma ya maji na miradi iendelee," alisema.

Hata hivyo, Lugongo alisisitiza utunzaji wa mazingira na kulinda vyanzo vya maji hasa katika kata ya Funta kutokana na maeneo yake mengi kuharibiwa na uchimbaji wa madini.

"Nimeona katika kata hii maeneo mengi yameharibiwa kutokana na uchimbaji madini, naamini viongozi wa vitongoji, vijiji, kata na wilaya watakaa kuweka mikakati ya kulinda vyanzo vya maji na mtiririko wa maji yanakopita," alisema Lugongo.

Nipashe
# TESA
Jumanne Desemba 27, 2022
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI

## Gari linalopaa, kuendeshwa barabarani laja, litaanza kupatikana sokoni 2025





Ukurasa 17

Ukurasa 14

## Nyama ya maabara sasa ruksa kuliwa

ELIMU

**KWAHERI 2022**
**NA PANCRAS LUOGA**

# Uwe kijijini au mjini wakinge watoto na athari za kuangamia

WASOMAJI wa TESA tunawatakia mwaka mpya mwema na ari zaidi ya kusoma, kujifunza na kufurahia mambo yote yanayohusu elimu kwenu na jamii nzima.

Kazi inaendelea na sikukuu ya Noeli imemalizika ikikaribisha ujio wa mwaka mpya 2023, wakati shangwe za Happy New, zikiendelea kurindima jamii isisahau kuwa matendo ya unyanyasaji na udhalilishaji watoto yalitikisa 2022 hivyo isiruhusu yajirudie na kuimarika mwakani kwa kila mwanajamii kuwalinda vyema Watoto walio kwenye likizo.

Wakati tukitafakari hiyo inafanyiwa kazi vipi, wanajamii wasisahau kuwa wanafunzi wako kwenye mapumziko na kuna mambo mengi yanafaa kuzingatiwa ili kuwalinda na kuwatunza raia hawa wachanga.

Mojawapo ni kuelewa kuwa watoto wanaishi na jamii muda wote hivyo wanajifunza yote ambayo yanafanywa na watu wanaowazunguka kuanzia nyumbani, ibadani, hadi mtaani hadi kwenye burudani.

Hii ni kwa mazuri au mabaya, kwa hiyo ni muhimu jamii kujitahidi kufanya mambo mema ili kuwa mfano bora kwa watoto wanaoishi nao.

Kwani wao bado ni wanafunzi hivyo, wanajifunza yote kutoka kwenye mazingira waliyopo. Pili, watoto wapo kwenye nafasi ya kuingia katika mtego wa kujihusisha na uhalifu kwa kuwa katika maeneo yasiyofaa kulingana na umri wao.Hivyo ni rahisi zaidi kufanyiwa vitendo visivyofaa kutoka kwa baadhi ya wanajamii.

Mfano wanapokwenda kushinda na kukesha kwenye vibanda umiza kunakoonyeshwa video na tamthilia za ngono au sehemu za kucheza michezo ya kompyuta.

Watu wanao wajibu wa kuwalinda ili kuwa na likizo yenye mafanikio na sio yenye balaa, kwa hivyo kujitahidi kuwa mfano bora wa maisha kwa wanafunzi hawa. Watu wakumbuke watoto bado ni wanafunzi kwa hiyo wanaendelea kujifunza kutoka kwa wanaowazunguka. Hivyo wawape mfano iliyo vizuri na bora.

Jamii isiwe mfano wa vitu visivyofaa kwa watoto kama ulevi wa kupindukia, matusi, ugomvi, kutumia dawa za kulevya, kunyanyasa mabinti mfano madereva wa bodaboda kuwapa lifti n a kuwalaghai wasichana.

Kumbuka mtoto wa mwenzako ni wako pia hivyo umfundishe yaliyo mema. Pili, jamii iwalinde watoto hawa ambao ni wanafunzi dhidi ya matendo yasiyofaa. Mfano wa vitendo hivyo ni ubakaji na ulawiti na aina nyingine zote za unyanyasaji wa kijinsia dhidi yao na kuwafundisha kutumia vilevi.

Ni wajibu pia wa watu wanaowazunguka kuwafuatilia na kuhakikisha watoto hao hawaendi maeneo hatarishi kama vile kwenye vibanda umiza, kujiingiza kwenye michezo ya kompyuta, magenge au vijiwe vya wahalifu na kushiriki mambo hatari zaidi yanayoweza kuwafikisha kwenye kufanyiwa vitendo vya ukatili.



Vibanda vya kuonyesha picha mitaani ni eneo linalopotosha watoto kwa kuwafundisha tabia mbaya kama uhalifu,kutumia dawa za kulevya na unyanyasaji. PICHA: MTANDAO

Na kama watoto hao wakiwepo maeneo hayo hatarishi basi wanaowaona wachukue nafasi ya mzazi au mlezi na kuwaondoa kwenye hatari.

**KUCHUNGUZA JAMII**

Kwa sasa kumekuwa na ushiriki duni wa wanajamii katika kuwalea na kuwalinda watoto hasa wale ambao ni wanafunzi wanapokuwa likizo. Hii inatokana na watu kuwaona kuwa si sehemu muhimu ya malezi ya watoto (wanafunzi) na kufikiria kuwa wazazi na walezi wao pekee ndiyo wanaohusika katika jukumu hilo.

Ni kutokana na kubadilika kwa mifumo na mitazamo ya watu kwenye makuzi na malezi kwa ujumla na hilo limesababisha watu kuona kuwa malezi ni ya mzazi au mlezi wa mtoto na sio jukumu la wote.

Kutokana na kuchenga kazi hiyo baadhi ya wanajamii tena wakiwa wazazi au watu wenye ndoa na familia huwadanganya watoto hao na kuwadhalilisha.Mfano muda mwingine watu wazima hao huwaahidi watoto kuwa wanakwenda nao kuwanunualia vitu au watawalipia vingilio kwenye vibanda vya kuonyesha video au mpira.

Mwisho wa kupewa ofa hiyo ni vitendo vya ulawiti na ubakaji yote hayo ni kinyume na mtazamo chanya wa jamii kuwa watoto wa mwenzako ni mtoto wako hivyo mlee na umlinde kama mtoto wako ili akue na afikie ndoto zake.

Na hiyo ni dalili wazi ya jamii kushindwa kuwalea na kuwalinda watoto kipindi cha likizo na kutamani shule zifunguliwe haraka ili warudi shuleni au vyuoni, kutokana na kuona kuwa hawawawezi.

**UFUMBUZI WA TATIZO**

Kwanza wanajamii lazima wakubali kuwa mfano bora kimatendo na maadili na kimaisha kwa watoto wakiwa likizo na muda wote wa maisha yao.

Hilo litasaidia watoto waone na kujifunza mambo na madili mema kutoka kwa ndugu,jamaa, jirani , walezi na wazazi na kuyafanya wakiwa nyumbani au watakaporudi shuleni au vyuoni baada ya likizo.

Pili, ni wanajamii waanze kuwalea na kuwalinda watoto dhidi ya vitendo visivyofaa kwa kujua nani na wapi ni sehemu salama ya kucheza na kujihusisha nayo na ipi si sehemu salama kwao kucheza au kuwa karibu.

Mfano wawakumbushe na kuwaeleza watoto kuwa vibanda umiza sio sehemu salama kwao, kwani bila kumsaidia mtoto kujua hilo sasa itakuwa ngumu sana kwao kubadilika akiwa mkubwa.

Mfano mtoto aliyeandaliwa mazingira ya kuzurura,kucheza kupitiliza, kushinda na kukesha kwenye vilabu vya kienyyeji na walevi, wavutabangi, wacheza kamari na kusahau kurudi nyumbani au lala hata akiwa mkubwa atakuwa anafanya vitu hivyo hivyo. Kwani tayari alijifunza tangu akiwa mtoto tena mwanafunzi. Ikumbukwe kuwa "mtoto umleavyo ndivyo akuavyo".

Watu iwe kijijini, mtaani au mjini wakumbuke kuwa katika kujiandaa kikamilifu kwa kutimiza jukumu hili muhimu lazima wazingatie misingi yaifuatayo, kuwaandaa vizuri kimaadili watoto wa sasa ni kuwandaa wanajamii bora na wenye maadili wa baadae.

Kila mmoja baba, mama, vijana, walimu, viongozi na walezi wa kiroho wachukue hatua za kurekebisha kasoro kwa Watoto mapema kabla tabia hizo hazijaota mizizi na kukomaa na kusababisha kuwa na wanajamii wasiofaa.

INAENDELEA UK. 18

SAYANSI

KWAHERI 2022

NA MWANDISHI WETU

# Wakati maswali ya GMO yakisumbua, nyama ya maabara sasa ruksa kuliwa

## Ndivyo 2022 unavyoondoka na sekta za mifugo, Amerika, Israel

TEKNOLOJIA inayohusisha masuala ya uzalishaji vyakula pengine katika njia inayohusisha utaalamu wa maabara hata kutumia virutubisho mfano 'dawa busta' ambavyo vinatiliwa mashaka, ni mambo yanayowahofisha walaji hasa kwenye nchi zinazoendelea.

Kwa mfano, Watanzania lakini pengine Waafrika wengi wanahofia kula chochote kilichoelezwa kuwa kimezalishwa na mbegu zilizobadilishwa nasaba -DNA.

Inapotajwa teknolojia ya GMO, inayozalisha mimea na wanyama (viumbe hai) waliobadilishwa nasaba, hofu inazidi kuongezeka mlaji akiamini kuwa akila itakuwaje.

Lakini, wakati watu wengi wakihitaji majibu na kuhakikishiwa usalama wao, maendeleo makubwa na utaalamu unatumiwa kuzalisha vyakula kwa njia za kisayansi bila kuogopa.

Mwaka unavyomalizika wanasayansi wa Marekani wamekuja na kibali cha kuruhusu nyama inayokuzwa au kutengenezwa katika maabara kuliwa na bila hofu.

Wanaidhisha kuliwa na binadamu kwa mara ya kwanza na mhusika mkuu ni Shirika la Usalama wa Chakula na Dawa la Marekani (FDA), linalotoa idhini ya kuliwa kitoweo cha kuku.

Kuku hao ambao ni ruksa kukuzwa na kuuzwa seli zao hukuzwa ndani ya maabara na siyo kulishwa na kufugwa kwenye mabanda kama ilivyozoeleka .

FDA inasema inatoa idhini hiyo baaada ya kufanya ''tathmini ya uangalifu'' na kuridhisha, inaripoti BBC Swahili ikiongeza kuwa kuku hao wanatengenezwa katika matangi ya chuma na kampuni ya Upside Foods, kwa kutumia seli zilizovunwa kutoka kwa wanyama hai.

Baada ya FDA kutoa ruksa sasa hakuna kipingamizi wataweza kuuzwa kwa walaji baada ya ukaguzi wa Wizara ya Kilimo ya Marekani kuridhika.

FDA inasema ilitumia data na taarifa zilizotolewa na kampuni hiyo kufikia uamuazi wake, kwamba "haikuwa na maswali zaidi wakati huu".

Mwanzilishi wa kampuni na mkurugenzi mtendaji Upside Foods, Uma Valeti ananukuliwa na BBC, akisema:"Tulianzisha kampuni ya Upside katika wakati ambapo dunia ilikuwa imejaa watu wenye mashaka na kazi hii, na sasa, tumeweka historia tena kama kampuni ya kwanza kupokea barua ya kutokuwa na maswali' kutoka kwa FDA kwa kuvuna nyama."

**HAMU YA KUVUMBUA**

Kampuni kadhaa za chakula zinazoanza shughuli zake zimekuwa zikijaribu kutengeneza bidhaa zinazofanana na hizo zinazofanyika kwenye maabara.

Mafanikio ya jambo hilo ni kupungua utoaji mkubwa wa hewa chafu ya kaboni kwenye samadi na mifugo na wanyama wengine, lakini pia kupunguza matumizi ya maji, pamoja na ardhi kubwa kwa ajili ya ufugaji ikiwa ni faida kwa siku zijazo.

Wanasayansi wanasema shinikizo la ongezeko la joto duniani kutokana na mabadiliko ya tabianchi linaweza kushuka kwa zaidi ya asilimia 80, iwapo vyakula kama hivyo vinavyozalishwa kwenye maabara vitatumika, ikilinganishwa na mlo wa kawaida wa wakazi wengi huko Ulaya wanaotegemea nyama.



Nyama inayozalishwa ndani ya maabara ikitengenezwa kuanzia, steki, maini na salala. PICHA: MTANDAO

Nyama inayokuzwa kwenye maabara inatarajiwa kuchukua nafasi kubwa katika soko la jumla la nyama katika miaka ijayo.

BBC inaitaja The start-up Eat Just, kampuni ambayo ni mshindani wa Upside Foods, ambayo nayo ilikuwa ya kwanza kupokea idhini ya kutengeneza nyama bandia au "nyama safi" ya maabara, nchini Singapore mwaka 2020.

Nyama hizo zilitengenezwa kutokana na seli za nyama kazi ikifanyika katika maabara na kwamba kampuni mbili kati ya nyingine kubwa katika sekta hiyo ya ukuzaji wa nyama za maabara ni kampuni yenye makao yake Israel-Future Meat Technologies na Impossible Foods.

Aidha, inatengeneza mikate yake ya baga 'burger' mkate unaowekwa nyama katikati inayofahamika kama Impossible Burger iliyozinduliwa mwaka 2016 na umaarufu wake umeongezea zaidi.

Matokeo yake, kampuni ilianzisha ushirikiano na kampuni ya Burger King na sasa Impossible Burgers z inauzwa katika migahawa mingi nchini Marekani

Idhini iliyopewa The Upside Foods na FDA imeelezewa kama hatua kubwa katika sekta na Ernst van Orsouw, Mkurugenzi Mendaji wa Roslin Technologies - kampuni ya teknolojia ya chakula ya Scotland

"Inafurahisha sana kuona mdhibiti wa viwango kote duniani sasa anaafiki kwamba nyama iliyovunwa ndani ya maabara ni salama kuliwa," anasema." FDA imekuwa ikifuata misingi ya hadhari, sayansi na mbinu ya kivitendo kudhibiti chakula hiki, ambacho kinaweza kuwa mwongozo bora kwa maeneo mengine pia."

Anasema hatua hiyo "itachochea uwekezaji zaidi na uvumbuzi " katika sekta ya vyakua vya kukuzwa kwenye maabara.

**CHA KUJIFUNZA**

Maendeleo ya sayansi na teknolojia kwenye kuzalisha vyakula kuanzia wanyama na mimea inaelekea yataweka pembeni kuka, Wanyama na mifugo mingine inazofugwa tena kwa kuhama hama.

Kwa mfano kulisha ng'ombe kutoka Shinyanga hadi Ihefu mkoani Katavi, kishakurudi tena hadi Kigoma yote hayo ni mambo ya kuwatafkarisha wakulim a na wafugaji kuwa kulima na kufuga 'kiuharibifu' sasa kunakishwa na inavyoelekea hakuna anayetaka dunia ikizidi kuharibika.

Inavyoelekea habari ya kuhamasisha wafugaji kufuga itakoma maana, hakutakuwa na mnunuzi wala mlaji wa bidhaa baada ya viwanda vya kusindika nyama kuhamishiwa maabara.



Nyama kutoka kwenye malisho na ufugaji wa kutunza wanyama kwenye mabanda inaelekea kukosa walaji kwenye mataifa yaliyoendelea ambayo ndiyo wanunuzi wakubwa wa kitoweo hicho. PICHA: MTANDAO

ELIMU

NA WAANDISHI WETU

# Ndiyo yaliyotikisa, kung'ara sekta ya elimu mwaka huu

■ Mahafali ya 1 elimu bila michango, Samia Scholarships



Rais Samia Suluhu Hassan na Waziri wa Elimu Profesa Adolf Mkenda , wameng'ara mwaka huu katika kusuka na kutengeneza upya sekta ya elimu. PICHA: MAKTABA

MWAKA 2022 unayoyoma dunia ikielekea kuukaribisha msimu mpya wa 2023, ukiangalia nyuma ni kipindi kilichokuwa na matukio mengi ambayo Watanzania wameyashuhudia.

Iwe kitaifa, kifamilia na hata kimataifa wako walioumia, kusononeshwa na yaliyotokea, kadhalika baadhi wamefurahia na wameandika historia.

Kwa upande wa sekta ya elimu kuna mengi miongoni mwake ni kutangazwa elimu bure kuanzia shule ya msingi hadi kidato cha sita, na mwaka huu wa 2022, imeendelea kuwapunguzia makali wazazi na walezi kwa kutangaza elimu bure hadi kidato cha sita.

Ni Juni 14 mwaka huu jijini Dodoma, Waziri wa Fedha Dk. Mwigulu Nchemba, anasema jambo hilo bungeni wakati akiwasilisha bajeti kuu ya serikali na kufafanua kuwa, kwa sasa wanafunzi wa kidato cha tano ni takriban 90,825 na kidato cha sita ni 56,880 na kwamba mahitaji ya fedha ni Sh. milioni 10.3

Akafafanua kuwa ili kuwapunguzia gharama watoto hao kama Rais Samia Suluhu Hassan, alivyoelekeza wizara hiyo, anapendekeza kufuta ada kwa wanafunzi wa kidato cha tano na sita.

Ada inayolipwa ni Shilingi 70,000 kwa shule za bweni na kutwa kwa mwaka.

Waziri huyo anasema serikali itaendelea kujenga mabweni kwenye maeneo hatari kwa wanafunzi wasichana, kuimarisha elimu ya ufundi hususan katika vyuo vya kati kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kujiajiri au kuajiriwa.

Katika ufafanuzi wake, anasema hadi sasa wilaya 77 zina vyuo vya Ufundi VETA kati ya wilaya 138 zilizopo, huku mikoa 25 ikiwa na vyuo vya ufundi kati ya mikoa 26, huku akiutaja Songwe kuwa hauna chuo cha VETA.

**SAMIA SCHOLARSHIPS**

Katika mwendelezo huo wa elimu bure, Septemba 27 mwaka huu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia imeanzisha programu ya ufadhili wa Samia Scholarship.

Ufadhili huo ni mpya kwa kwenye wanafunzi waliopata ufaulu wa juu katika mitihani ya kidato cha sita mwaka 2022 iliyoendeshwa na Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA) katika Tahasusi za Sayansi (PCB, PCM, PGM, CBG, CBA, PMC na CBN).

Samia Scholarships itagharamia kwa asilimia 100 masomo ya chuo kikuu kwa wanafunzi hao ambao wamepata udahili katika fani za teknolojia, uhandisi, hisabati na tiba, huku ukizingatia sifa kadhaa.

Miongoni mwa sifa hizo, ni mwanafunzi awe Mtanzania, awe na ufaulu wa juu kwenye mitihani ya taifa ya kidato cha sita mwaka 2022 iliyoendeshwa na NECTA katika tahasusi (combination) za sayansi.

Awe amepata udahili katika programu za sayansi katika chuo kikuu kinachotambuliwa na serikali ambacho katika mwongozo

> "Samia Scholarships itagharamia kwa asilimia 100 masomo ya chuo kikuu kwa wanafunzi hao ambao wamepata udahili katika fani za teknolojia, uhandisi, hisabati na tiba, huku ukizingatia sifa kadhaa.

wa utoaji mikopo wa Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kwa mwaka 2022/2023.

Maeneo ya ufadhili yanatajwa kuwa yanazingatia viwango na miongozo ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu kugharamia ada ya mafunzo, posho ya chakula na malazi, posho ya vitabu na viandikwa, mahitaji maalum ya vitivo, mafunzo kwa vitendo, utafiti na vifaa saidizi kwa wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

**WARAKA WA VIBOKO**

Novemba 29, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum Dk. Dorothy Gwajima anaomba Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kusambaza waraka wa adhabu za viboko shuleni wa mwaka 2002.

Lengo la ombi hilo ni kutaka walimu na wanafunzi wauelewe, kwa kuwa ukatili kwa watoto unaendana na kuudhuru mwili ikiwa ni pamoja na vipigo ikijumuisha adhabu ya viboko vilivyopitiliza shuleni.

"Hivyo viboko vilivyopitiliza ni ukatili kwa watoto kwa kuwa tunao Waraka na 24 wa mwaka 2002 unaosimamia adhabu za viboko shuleni ambao unasema wazi ni nani mwenye Mamlaka yakutoa adhabu hiyo na viboko vingapi vinaruhusiwa na kwa utaratibu upi," anasema Dk. Dorothy.

Anaeleza kuwa kuna vikwazo vilivyopo kuwa ni usimamizi wa utekelezaji wa waraka huo, na kwamba baadhi ya walimu hawaufuati wanapotoa adhabu na kuwataka wabadilike vinginevyo washtakiwa kwa sheria ya mtoto iwapo atatoa adhabu hiyo nje ya maelekezo ya waraka huo.

"Inasikitisha kuona baadhi ya watoto wanaacha shule kwa sababu ya kukimbia viboko huku wengine wakipata majeraha makubwa na ulemavu na hata kupoteza maisha eti kwa sababu ya adhabu za viboko, hii haikubaliki kwani hii adhabu ya viboko haikulenga kusababisha mateso kwa watoto na ndiyo maana tunao waraka," anasema.

**KUFUTA MATOKEO LA 7**

Desemba mosi, Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA), lilitangaza matokeo ya darasa la saba kwa mwaka 2022 huku likieleza kufuta matokeo yote ya watahiniwa 2,194 kati ya watahiniwa 1,350,881 waliofanya mtihani ambao walibainika kufanya udanganyifu katika mtihani huo.

Kaimu Katibu Mtendaji wa NECTA, Athuman Amasi, anasema baraza limezifungia shule 24 kuwa vituo vya mitihani ya taifa baada ya kuthibitika kupanga kufanya udanganyifu katika mitihani ya kumaliza elimu ya msingi.

Anataja baadhi ya shule kuwa ni Musabe ya jijini Mwanza na St Anne Marie ya jijini Dar es Salaam na Rweikiza ya mkoani Kagera.

Desemba mosi hiyo pia serikali iliagiza mabasi yote yanayobeba wanafunzi kuwa na kondakta wa kike na pia yafungwe kamera maalum, kwa lengo la kulinda wanaafunzi dhidi ya vitendo vya ukatili. Waziri wa Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wanawake na Makundi Maaalum, Dk. Dorothy Gwajima ndiye aliyetoa agizo hilo akiwa katika Shule ya Star Light ambako mtoto wa miaka sita wa darasa la kwanza alidaiwa kubakwa na kondakta wa gari la shule hiyo.

**FEDHA ZA UHURU**

Desemba 7, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu George Simbachawene anatangaza kuwa fedha zilizokuwa zimetengwa na wizara na taasisi kwa ajili ya maadhimisho ya miaka 61 ya Uhuru wa Tanganyika mwaka huu, zitapelekwe TAMISEMI.

Anasema zitumika kujenga mabweni katika shule nane za msingi za wanafunzi wenye mahitaji maalum na gharama yake ni Shilingi milioni 960.

Waziri anasema zitaelekezwa kujenga Shule ya Msingi Buhangija Shinyanga, Goweko Tabora, Darajani Singida, Mtanga Lindi, Songambele Lindi, Msanzi Rukwa, Idofi Njombe na Longido Arusha.

Kwa mujibu wa Simbachawene, ulikuwa ni uamuzi wa Rais Samia Samia Suluhu Hassan wa kuwajali na kuwajengea mazingira rafiki wanafunzi wenye mahitaji maalum.

INAENDELEA UK. 19

TEKNOLOJIA

NA CHRISTINA MWAKANGALE

# TEHAMA na wanahabari mbinu inayokuza uandishi kidigitali 2023



Kinamama na kompyuta wakifuatilia habari kutoka maeneo mbalimbali duniani. PICHA:WEF

WAKATI dunia ikisonga mbele hususan katika kukua kiteknolojia wanahabari hawajaachwa nyuma, kwa kurahisishiwa mbinu za kisasa kupitia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano-TEHAMA, inayoleta mapinduzi ya maendeleo kwa kuhabarisha kidigitali.

Wanahabari takribani 60 wengi wao wanawake, kutoka mikoa tofauti wanapewa mafunzo ya kukuza ujuzi kidigitali kupitia taaluma yao, ili kubaini na kuchangamkia fursa na namna ya kuandika habari zinazohusisha data.

Ni mafunzo yanayoptolewa kupitia mpango wa Women At WebTZ, unaowezeshwa na Boresha Habari kupitia Shirika la Marekani la USAID Tanzania.

Wakufunzi katika mafunzo hayo, Lily Urio, Zahara Tunda na Ashura Babi ambao kwa namna tofauti wanawasilisha mada tofauti kwa wanahabari ikiwamo kuandika taarifa za kidigitali na mbinu za kubadili fikra na kuegemea uandishi wa kidigitali, wanawaachia waandishi mambo mapya ya kuchangamkia kiteknolojia.

Zahara anasema uandishi wa kidigitali huwa ni wa namna tofauti ikiwamo wa michoro, picha na maumbo tofauti ili kumvutia msomaji katika makala au habari inayochapishwa au kurushwa kwenye mitandao ya kijamii.

"Badala ya kuandika namba kwenye habari yako,mwandishi unatakiwa kuwa mbunifu kwa kutumia vielelezo, michoro, ambavyo vinatafsirika haraka kwa msomaji. Mara nyingi watu huogopa namba zenye tarakimu nyingi, lakini grafu itasaidia kupunguza woga," anasema Zahara.

Mkufunzi Lily anasema kila mwandishi anayetamani kuwa wa kidigitali ni lazima awe na uwezo mzuri wa mawasiliano, fikra pana na kuwa na wazo la kutoa suluhisho la haraka kupitia kazi yake.

"Unaweza kujua namna ya kukusanya taarifa kutoka vyanzo mbalimbali hasa mitandao ya kijamii, kwa kufahamu kinachopendwa kwa wakati gani. Tambua namna bora na mbinu za uandishi wa data na kuhusisha habari zako mtandaoni kwa sababu ulimwengu ni kidigitali zaidi," anasema Lily.

> Anasema mteja anyejiunga na huduma za mtandao ana haki ya kulindwa usalama wake, kupata huduma ya uhakika bila kukatika na iwapo inatokea tatizo la kiufundi, taarifa itolewe kwa mtumiaji.

**MPANGO ULIOPO**

Mpango wa mradi wa Women At Web project unaosimamiwa na Media Convergence, unalenga kuhakikisha wanawake waliopo mijini na nje kidogo ya mji, wananufaika na mabadiliko ya kidigitali,

Nchi zilizotengwa kwenye mradi huo ni Uganda, Kenya, Tanzania na Rwanda kwa lengo la kuwapa ujuzi wa kidigitali hususan wanawake vijana ambao watafanikiwa kukabiliana na ukatili wa kijinsia mtandaoni kwa kutoa taarifa mbalimbali.

Mitandao ya kijamii, hivi sasa ina watumiaji wengi hasa kupitia instagram, facebook, whatsapp, YouTube, na mingineyo huku ikikadiriwa watumiaji wa huduma hiyo wanafikia bilioni 3.8 na kuwa kati ya mbinu mpya inayoifikia dunia kwa haraka Zaidi kufikisha habari.

**WANAWAKE, DIGITALI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Zaina Foundation, Zaituni Njovu akizungumza kwenye moja ya mafunzo ya wanahabari wanawake, yaliyolenga kuwaongezea ujuzi, ikiwamo kulinda vifaa vyao vya kazi pamoja na kuzingatia usahihi wa vyanzo vya habari, anasema wanawake wapo nyuma katika mapinduzi ya kiteknolojia.

Zaituni anasema lengo ni kuwawezesha wanawake kwa kuwapa ujuzi wa namna ya kuhakikisha usalama katika matumizi ya mtandaoni kwenye dunia ya kidigitali, ikizingatiwa kundi ni kubwa la wanawake ambao bado halijajihusisha na Teknolojia Mawasiliano (IT).

"Haki ya kupokea, kutuma, kutoa taarifa ni ya kila mmoja. Lakini tunahitaji kuwepo usalama wa matumizi ya mtandao, kulindwa kwa faragha, kwa kuwa wanawake ni kati ya waathiriwa wakubwa wa picha zisizo na maadili zikisambazwa mitandaoni bila mtu kujua," anasema Zaituni.

Anasema mteja anyejiunga na huduma za mtandao ana haki ya kulindwa usalama wake, kupata huduma ya uhakika bila kukatika na iwapo inatokea tatizo la kiufundi, taarifa itolewe kwa mtumiaji.

"Mtumiaji ameamua kujiunga na kifurushi cha siku au hata wiki, lakini baada ya muda unaambiwa mtanado wa kampuni fulani haupatikani bila taarifa yeyote. Ni haki yako kupata taarifa, wakati

Anafafanua kwamba mafunzo hayo ambayo ni ya awali kutolewa kwa wanahabari, yanawaongezea ujuzi wanahabari, ili kukabiiana na changamoto zilizopo mtandaoni pamoja na kujiongezea fursa za kiuchumi.

"Tunawaelimisha wanawake katika matumizi ya teknolojia na mtandao, wakati matumizi ya teknolojia yakikua ipo haja ya kuwa makini na matumizi ikiwamo kuvamiwa kimtandao na kuvujisha siri zako, ikizingatiwa tunaelekea kwenye uchaguzi mkuu inabidi

**IDADI YA WATUMIAJI**

Zaituni anasema hivi sasa takwimu duniani zinaonyesha watumiaji wa mtandao (intaneti),wameongezeka na kufikia bilioni 4.5 duniani na kati yao watumiaji milioni 23 ni kutoka Tanzania.

"Wakati matumizi yakikua dunia ni muda wa kuongeza usalama ya kimtandao kwa mtumiaji, wadau kwa kuwawezesha namna ya kuweka usiri wa taarifa zao na data zao," anasema Zaituni.

Zaituni anazungumzia changamoto akisema zilizopo katika mtandao ni usalama mdogo huku wanawake kadhaa wakiwa na elimu ndogo.

"Changamoto ni elimu kwa ambao wanatakiwa kufikisha habari kupitia mtandao, ili kutoa taarifa sahihi kuelimisha umma kipindi amcho ulimwengu tunahitaji elimu zaidi," anasema.

Anaeleza kuwa kutokana na watu wengi kuwa na elimu ndogo ya kulinda taarifa, imekuwa ni kawaida kuona picha za kuwadhalilisha hasa wanawake zikisambaa maeneo tofauti bila wao kujua," anaeleza Zaituni.

TEKNOLOJIA

NA MWANDISHI WETU

KWAHERI 2022

# Gari linalopaa, kuendeshwa barabarani laja, litaanza kupatikana sokoni 2025



Gari la kupaa likipewa majina mengi likiwamo la 'hyper drive ' linaweza kuruka juu ili kukwepa foleni linatarajiwa kuingia sokoni kuanzia mwaka 2025. PICHA: BBC

MWISHO wa Oktoba 2022, taarifa zinasambaa kuhusu ujio wa gari linalopaa na kutuma ujumbe kwa nchi zinazoendelea ikiwamo Tanzania kuwa huenda bomoabomoa na kuweka X kwenye majengo sasa kukafikia mwisho.

Japo ni safari ndefu kwa mataifa yanayoendelea lakini huko Marekani wahandisi wanasema mwaka 2025 ni muda mwafaka wa kuanza kuendesha gari linalopaa, ni kwa saa chache 'garindege' linakuwa barabarani lakini ghafla mambo yanabadilika gari linapaa wima.

BBC Swahili inaripoti taarifa hiyo ikianzia katika hafla ya uzinduzi inayofanyika katika Chuo Kikuu cha Draper huko California Marekani, ikijuza kuwa kampuni ya Alef inayotengeneza magari inajinasibu jinsi inavyounda gari lake matata litakalopaa.

Alef itatengeneza 'garindege' ambalo injini yake inatumia umeme likipewa jina la Model A, kama gari la kwanza la ukweli linalopaa.

Mwaka unamalizika kwa kuwapa wateja matumaini kuwa licha ya kuonekana kama gari la umeme lakini linaweza kupaa tena likiwa wima, na linaweza kuruka juu kwa umbali wa kilomita 110 sawa na maili 68.

Pengine ni umbali unaoweza kuwa kutoka Ubungo Dar es Salaam hadi Chalinze kitu kikiwa kinaelea angani. Yote hayo yataondoa foleni, ajali na usumbufu ikiwamo kubomoa nyumba na kuharibu maeneo ili kupisha ujenzi wa barabara.

Kampuni hiyo inatarajia kushindana katika soko linalomilikiwa na wapinzani waliobobea kwenye uzalishaji magari kama vile AirCar na Pal-V gyrocopter ambayo tayari yana magari yanayoendeshwa na kupaa kama ndege.

Lakini Jim Dukhovny, Mtendaji Mkuu wa Alef na mwanzilishi anasema magari mengi yaliyopo sasa sio magari ndege hasa kwa maoni yake.

"Gari linalopaa lazima liwe gari, ambayo ina maana kwamba linaweza kuendeshwa kwenye barabara ya kawaida, kuegesha katika maegesho ya kawaida ya na pia linalopaa wima," anaiambia BBC.

**MUUNDO, KUJIGEUZA**

Gari hilo linaelezwa kuwa sehemu ya juu ya nje ya Model A inafanana na gari la kawaida na inajengwa na wavu ili hewa ipite hadi kwenye 'propela nane' zilizo ndani ambazo husaidia kulinyanyua.

Lakini kuruka umbali wowote kwa kutumia propela peke yake, bila kusaidiwa wa mabawa, kungehitaji nguvu nyingi sana, anasema.

Suluhisho lililopendekezwa la Alef ni kwamba kwa safari ndefu za ndege Model A hubadilika kuwa ndege.

Baada ya kuinuka wima, Model A itageuka na kurudi kawaida, chumba cha marubani cha watu wawili kinazunguka ili dereva abaki akitazama mbele, na gari linakuwa ndege na pande ndefu za gari zikiunda mabawa ya juu na ya chini.

Umbo la kawaida la ndege, lenye mabawa mawili, moja juu ya lingine, ni rahisi kuona katika mfano wa herufi A, ili kuongeza uelewa Alef inatoa video inayoonyesha mabadiliko hayo.

Jarida la Forbes linaandika kwamba namna ndege hiyo itakavyoruka inafanana na 'Opener Blackfly', ambayo ni ndege ya umeme inayopaa wima. Wachambuzi wakihoji ni wazo la busara, lakini linaweza kuwa vitendo?

Kuifanya gari kuruka angani na kupaa lakini pia likibakia kuwa motokaa unaoendeshwa barabarani kwa pamoja huongeza uzito, nguvu ya umeme, pia inamaanisha iwe na betri kubwa yenye nguvu kubwa zaidi wakati wote.

"Muundo huo uko kwenye uwezo wa fizikia na teknolojia kwani vinaweza kufanya na ungetarajia iwe hivyo," asema mhandisi wa anga profesa Steve Wright wa Chuo Kikuu cha West of England cha...

Licha ya nia hiyo suala la vikwazo vya kiufundi vinatajwa kimojawapo ni kuwa na barabara maalumu angani zenye magari mengi yanayoruka. Kama ilivyo kwa ndege kwa sasa.Udhibiti na uidhinishaji wa magari yanayoruka huenda ukawa mkali, unaotumia muda mwingi na wa gharama kubwa, kama ilivyo kwa ndege yoyote.

Ili kurusha gari hili, ambalo linaweza kuendeshwa barabarani, itahitajika leseni ya marubani ingawa Mtendaji Mkuu wa Alef Dukhovny anafikiria kwamba kwa safari fupi za kiwango cha chini juu ya vizuizi kwa kutumia safari ya wima, leseni inayotumiwa kwa waendeshaji wa drone inaweza kutosha.

Anaongeza kuwa mamlaka zinaweza kuweka sheria kali juu ya wapi magari ndege hayo yanaweza kusafirishwa.

> "Gari linalopaa lazima liwe gari, ambayo ina maana kwamba linaweza kuendeshwa kwenye barabara ya kawaida, kuegesha katika maegesho ya kawaida ya na pia linalopaa wima," anaiambia BBC.

**BARABARA HAZITAHITAJIKA**

Profesa Steve Wright wa Chuo Kikuu cha West of England anadhani mustakabali wa magari yanayoruka hautakuwa gari moja ambalo watumiaji wanamiliki, kuendesha na kupaa nalo.

Inagusiwa kuwa katika filamu ya Back to the Future, gari la DeLorean linaloendeshwa na mhusika Doc Brown linaacha njia na kuruka angani.

"Hivyo sivyo usafiri mkubwa wa anga utakavyokuwa, Kwa kweli nataka kuwa na gari langu la DeLorean ya kuruka kweli kama mtu mwingine yeyote angetaka," Prof Wright anasema.

Kwa kweli, kusafiri kwa gari linaloruka, itakuwa kama kukodisha taksii. "Unaliita gari kwa simu yako, na garindege linasogea na linakupeleka mahali pa ukubwa wa bustani ndogo na ndege isiyo na rubani inashuka, inatua chini, unaondoka. Kwa hiyo, kwa maneno mengine, unaiita taksii isiyo na rubani."

Kampuni nyingi zinatengeneza ndege zisizo na rubani za abiria. Hivi karibuni kampuni ya China ya Xpeng ilitoa onyesho lake la kwanza la hadhara la gari lake la X2 huko Dubai.

Lakini Mtendaji Mkuu wa Alef Dukhovny anaamini kwamba wazo la kuwa na gari lenye uwezo wa kuendeshwa na kuruka kwa wakati mmoja ni la kuvutia.

BBC ilipomuuliza nani atakayeweza kulipa bei ya awali ya kununua Model A ya $300,000 (£266,000), anasema "watu wanaopokea mabadiliko mapema".

Anasema watu wamekuwa wakingojea gari linaloruka au kupaa kwa miaka 100. Lengo kuu la Alef ni kuanza kuuza magari hayo mnamo mwaka 2025.

# Uwe kijijini au mjini wakinge watoto na athari za kuangamia

INATOKA UK. 13

Hii itasaidia jamii kuwa na namna nzuri ya kufanya watoto kuona thamani ya muda wa likizo zao katika kujiandaa na maisha yao ya baadae.

Wito wangu ni kuwa lazima kuanza sasa kulitekeleza kikamilifu jukumu la kuwaandaa wanajamii bora wa baadae kwa kuwasaidia watoto kipindi hiki wanapokuwa likizo kuwa na mapumziko mema kiroho na kimwili.

Hili lifanyike na wanajamii kwa njia zote kwa kuwa mfano wa tabia na matendo mema kwa watoto wote kipindi hiki wanapokuwa likizo zinazoambagana na sherehe mbalimbali, burudani, wageni, kusafiri na kukutana na mambo mapya.

Hii inaanza na kijijini au mtaani anapoishi kutumia lugha zenye staha katika kuongea na kuonyesha maadili mazuri katika yale yote wanayoyafanya. Wasomaji tukubuke kama jamii ina tabia ya kuiba vitu hata watoto hawa ambao ni wanafunzi walio likizo wanajifunza kuiba pia.

Kwa mfano kuiba mifugo ya kundi fulani, kuchoma mashamba ya wakulima, kuwahi asubuhi kuiba kuni na mkaa msituni yote hayo ni kioo ambacho Watoto wanajiangalia na kujifunza mabaya.

Ndiyo maana baadhi ya watoto wakirudi shuleni nao wanaanza kudokoa na kuwaibia wenzao na mwisho wakimaliza masomo ndiyo wezi na majambazi wa kwenye jamii kutokana na kujifunza kwa wazazi, walezi na umma unaowazunguka wakati wakiwa likizo.

Pia jamii lazima ihakikishe inafanya lolote liwezekanalo ili kuwalinda watoto hawa dhidi ya vitendo visivyofaa.Wasiruhusiwe kwenda maendeo ya starehe kama baa, disko, ngoma kama kigodoro na mikesha ambayo inahatarisha hatima zao.

Tukumbuke kuwa kwa muda huo wote watoto watakuwa mikononi mwa jamii kwa kipindi kirefu tofauti na muda wa shule wanapokuwa chini ya uangalizi wa walimu. Zaidi utekelezaji kikamilifu wa jukumu hili wa jamii kwa watoto kipindi hiki cha likizo utasaidia kujifunza vitu na maadili yanayofaa kutoka kwa jamii.



Watoto wa Mbagala Kiburugwa jijini Dar es Salaam wakichezea maji sehemu lilipopasuka bomba la DAWASA na kuungwa kienyeji na kusababisha maji mengi kusambaa barabarani. Watoto wasiruhusiwe kuharibu huduma kama maji na miundombinu. PICHA: SELEMANI MPOCHI

Mwandishi ni Mhadhiri Msaidizi Usimamizi, Ufuatiliaji na Tathimini ya Miradi ya Afya MUHAS.

**MAONI: 0757-645746**

## WANENAVYO MALENGA

### NI MWANAFUNZI MMOJA, LALA KITANDA KIMOJA

Kama kuna upungufu, vitanda vya kulalia,
Kwamba shule ni dhoofu, vitanda vya kuchangia,
Amekwishawaarifu, ni vema mkasikia,
Ni mwanafunzi mmoja, lala kitanda kimoja.

Vitanda vya kuchangia, hatutaki kusikia,
Wanafunzi kulalia, ni marufuku sikia,
Hiyo kama yachangia, yale tunayosikia,
Ni mwanafunzi mmoja, lala kitanda kimoja.

Ni Waziri wa Elimu, amekwishawaambia,
Hili jambo la muhimu, vizuri kuzingatia,
Vinginevyo hali ngumu, mbele tutaifikia,
Ni mwanafunzi mmoja, lala kitanda kimoja.

Vitanda viwe pungufu, taarifa tasikia,
Tuujue udhaifu, tuweze kuingilia,
Ifike iwe yakifu, vitanda vya kuchangia,
Ni mwanafunzi mmoja, lala kitanda kimoja.

Hili la shule za bweni, agizo lawafikia,
Liingie akilini, kwenu tusijesikia,
Kwamba watoto bwenini, vitanda wanachangia,
Ni mwanafunzi mmoja, lala kitanda kimoja.

Mabaya ya kusikia, tusipate yasikia,
Malezi twayatakia, ni mazuri kubakia,
Tabia chafu fukia, zinapaswa kufukia,
Ni mwanafunzi mmoja, lala kitanda kimoja.

Magonjwa pia sikia, njia kuambukizia,
Vitanda vya kuchangia, hatutaki kusikia,
Hiyo itasaidia, tusije kuangamia,
Ni mwanafunzi mmoja, lala kitanda kimoja.

Enyi wakuu wa shule, agizo mmesikia?
Ziko vipi zenu shule, hali zenu zavutia?
Vitanda mnavyo tele, au vyawapungukia?
Ni mwanafunzi mmoja, lala kitanda kimoja.

Malezi bora watoto, ni hata pa kulalia,
Wazazi twatoa wito, tafadhali saidia,
Malezi yawe mvuto, mema tuzidi sikia,
Ni mwanafunzi mmoja, lala kitanda kimoja.

Inavyosemwa shuleni, na hata nyumbani pia,
Wazazi tuwe makini, wana wanapolalia,
Tusijeumwa moyoni, kuona waangamia,
Ni mwanafunzi mmoja, lala kitanda kimoja.

**Na Lwaga Mwambande (KiMPAB)**
**lwagha@gmail.com 0767223602**

ELIMU

# Ndiyo yaliyotikisa, kung'ara sekta ya elimu mwaka huu



Wanafunzi takribani 42,000 waliokuwa na vigezo lakini waliokosa mikopo waliruhusiwa kujisajili vyuoni wakati serikali inashughulikia tatizo lao. Pichani miundombinu ya kisasa ya maktaba ya chuo kikuu cha Dar es Salaam,Mlimani. PICHA: UDSM.

INATOKA UK. 15

**MARUFUKU YA KITANDA**

Desemba 15 Waziri wa Elimu, Sayansi na Tekinolojia, Profesa Adolf Mkenda, anapiga marufuku wanafunzi wa bweni wawili kulala kitanda kimoja na kuwataka wakuu wa shule kutoa taarifa kwa wakurugenzi wa halmashauri iwapo vitanda ni pungufu.

Anapiga marufuku kwenye Mkutano Mkuu wa Umoja wa Wakuu wa Shule za Sekondari Tanzania (TAHOSA) jijini Dodoma. Katika kufanikisha marufuku hiyo, anaahidi kufuatilia kama itatekelezwa.

Waziri huyo akasema mkurugenzi atakayekuwa anatumia fedha za utengenezaji wa vitenda sehemu nyingine na kulaza watoto wawili wa wazazi na walezi wenzake kitanda kimoja hafai kubaki ofisini.

**TIJA ELIMU MBADALA**

Utekelezaji wa Programu ya Elimu ya Sekondari kwa Njia Mbadala, umewarejesha shuleni wasichana 3,333 kwa mwaka 2022, tena kwa kuvuka lengo , hapo awali ilikusudiwa kurejesha wasichana 3,000 walioacha shule kwa sababu mbalimbali.

Ni taarifa inayotolewa bungeni wakati wa kujadili bajeti ya serikali ya mwaka 2022/23 Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

Waliokwama kusoma kwa sababu mbalimbali kuanzia ujauzito, utoro, magonjwa na kipato cha familia walianza safari ya kurejea darsani kwa kuripoti kwa viongozi wa serikali iwe kijijini, ofisi za elimu kata na vyuo vilivyotengwa mahsusi kwa ajili yao.

**KUFUMUA MTAALA**

Mwaka 2022 serikali imekusanya maoni ya wadau mbalimbali kuhusu mitaala inayotumika katika ngazi ya elimu ya awali, msingi, sekondari na katika vyuo vya ualimu.

Wadau wa elimu ambao wametoa maoni ni wengi wakati wa kuwasilishwa hotuba ya bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia watu na taasisi zilizowasilisha maoni na mitazamo walifikia zaidi ya 103,210.

Baadhi ya waliotoa maoni yao ni pamoja na wabunge, Kamati ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, taasisi za kidini, binafsi, wataalamu mbalimbali wa elimu na asasi za kiraia kutoka Zanzibar na Bara.

Lengo la kukusanya maoni hayo ni kuboresha mtaala kwa wanafunzi wa Bara na Zanzibar na maoni yatazingatiwa kwenye kuandaa mitaala mipya itakayowajengea wanafunzi ujuzi na maarifa yanayoendana na mahitaji ya jamii katika nchi, kikanda na kimataifa.

Vilevile, mitaala hiyo inatarajiwa kuwezesha kuwaandaa wanafunzi kuendelea na ngazi ya elimu inayofuata.

**MIKOPO KWA MAELFU**

Kwa mara ya kwanza wanafunzi wa vyuo vikuu waliruhusiwa kutangulia vyuoni na kuendelea na masomo wakati serikali inawaandalia fedha za mikopo kupitia Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu.

Baada ya kufanyika mjadala mzito bungeni kuhusu wanafunzi wenye sifa kukosa mikopo ya kuanza masomo mwaka wa kwanza 2022/23 Waziri Mkuu Kassimu Majaliwa, wakati akiahirisha Bunge la Bajeti, anatangaza kuwa wanafunzi wenye sifa lakini walikuwa hawajapata mikopo ya bodi waripoti vyuoni kuendelea na masomo wakati serikali inawatafutia fedha hizo.

Mwaka huu bodi ya mikopo ilitarajia kutoa mikopo ya takribani bilioni 570 kwa ajili ya wanafunzi 71, 000 waliokuwa wapate fedha hizo, lakini wengine 42,000 walikuwa na vigezo walikosa fursa.

Hatua hiyo, ilihitimishwa kwa serikali kuwaruhusu wanafunzi hao kujisajili wakati serikali inawatafutia mkopo huo.

**WAHITIMU ELIMU BURE**

Elimu bila michango ya wazazi na walezi maarufu Sera ya Elimubure, mwaka huu imetoa wahitimu wa darasa la saba. Ni wale walioanza la kwanza mwaka 2016 baada ya serikali ya awamu ya tano kuingia madarakani.

Ni mwaka huu Baraza la Mitihani la Taifa (NECTA) linatangaza watahiniwa 1,350,881 sawa na asilimia 97.59 ya waliojiandikisha walifanya mtihani huo.

Linasema baraza kuwa kati yao, wasichana walikuwa 709,556 sawa na asilimia 98.14, wakati wavulana walikuwa 641,325 ambao ni asilimia 97.00.

Watahiniwa 33,305 sawa na asilimia 2.41 hawakufanya mtihani huo kutokana na sababu mbalimbali zikiwamo za utoro na magonjwa ambapo wasichana walikuwa 13,471 na wavulana 19,834,inabainisha NECTA.

Awamu ya tano ya Rais John Magufuli, alipoingia madarakani Novemba 2015 alianza kutekeleza sera hiyo ya elimu bila michango.

Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 ndiyo iliyotamka kuwa serikali itafanikisha elimu msingi ,elimu ya awali hadi kidato cha nne, inakuwa ya lazima na inayotolewa bure kwenye shule za umma.

**Imeandaliwa na Sabato Kasika na Gaudensia Mngumi.**

## HABARI PICHANI



Watoto takribani 47 waliopata Kipaimara katika kanisa la KKKT Usharika wa Muheza mkoani Tanga katika sherehe ya pili ya Krismasi wakiimba kwa furaha jana ambapo watoto hao walibarikiwa na Mchungaji Kiongozi wa kanisa hilo, John Ndimbo akisaidiwa na Mchungaji Msaidizi, Jonathan Mwamboza. PICHA:STEVEN WILLIAM



Madereva wa bodaboda wakijaribu kuvuka taa za kuongozea magari kwenye Barabara ya Sam Nujoma eneo la Mawasiliano, Dar es Salaam jana, kabla ya kuruhusiwa na taa hizo, kitendo ambacho kinaweza kusababisha ajali. PICHA: SABATO KASIKA




Mjumbe wa Halmshauri Kuu ya CCM Taifa, Ramadhan Mlao (kushoto), akisalimiana na Mwenyekiti wa UVCCM Mkoa wa Lindi, Twaib Mpako juzi, alipomtembelea nyumbani kwake mjini Liwale kumpa pole ya kufiwa na watoto wake wawili mapacha. PICHA: MPIGAPICHA WETU

## CHEMSHABONGO NA -00 36 00-

Na Felix Magezi
felixmagezi@gmail.com

Dondoo: Kulia
1. kitu chenye madhara mwilini
5. mdudu aenezaye malaria
7. alikuwa Rais mweusi Marekani
9. kikundi cha watu kuchunguza jambo fulani
11.kifungu cha maneno yaliyo kamili 12.unyambi
14.aina ya madini
16.Kaka yake Mama
18.sala 19.chakula cha Israeli jangwani 20.Msafiri


Chini:
1. kabumbu
2. kinyume cha wema
3. jamii ya wanyama wenye kuzaa viumbe na kunyonyesha
4. ng'ata
6. pata maradhi
8. zawadi
10.mtungo
13.Mrithi wa kiti cha Ufalme Uingereza aliyekufa kwa ajali Ufaransa 15.kero 17.toa uhai
19.makazi ya watu wengi



Kamilisha jedwali kwa kujaza maneno yafuatayo:

MWANZA
MOTA
AMBIA
ZAKA, KIU, UJI
ADA, JUA, NZI
KAMBA
ADHA, UZA
TABAKA
AFYA, ASILI
AFISA, YAI
LULU, ULNA
ULEZI, ZULIA
KILELE, URAIA

maoni SMS: 0787 00 97 94




Majibu toleo lililopita

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| M | I | M | I | | A | M | U |
| O | M | A | N | I | | A | |
| L | A | M | A | | | L | |
| A | R | A | M | A | I | K | I |
| | I | | I | S | H | I | |
| | K | I | S | A | S | A | |
| U | A | | H | | A | | B |
| F | | M | W | A | N | Z | A |
| A | U | | A | | I | | A |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| P | A | N | Y | A | | U | |
| U | | Y | | Z | I | B | A |
| N | Y | A | M | A | | W | |
| D | | T | A | N | G | A | |
| A | M | A | N | I | | B | |
| | B | | D | A | K | W | A |
| P | E | T | E | | W | A | A |
| | Y | | L | | A | | L |
| K | A | R | A | B | A | T | I |



# Wazee washauri uwapo shule nyingi kidato cha tano, sita

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAZEE mkoani Mbeya wameshauri Serikali ya Mkoa kuzielekeza halmshauri zote kuanzisha shule nyingi za sekondari za kidato cha tano na sita ili watoto wote wanaofaulu kidato cha nne wanufaike na elimu bila malipo.

Pia walipendekeza kila halmashauri kujenga shule hizo zisizopungua 10 kufikia mwaka 2025 ili kukabiliana na ongezeko la wanafunzi wanaojiunga na ngazi mbalimbali za elimu baada ya serikali kuanzisha sera ya elimu bila malipo.

Walitoa ushauri huo juzi walipozungumza na Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya, Dk. Steven Mwakajumilo ambaye walimtembelea ofisini kwake kwa lengo la kumshauri kuhusu mbambo mbalimbali ya maendeleo.

Mwenyekiti wa wazee hao, Mwaiseje Polisya alisema kuanzishwa kwa shule hizo kutasaidia wanafunzi wote wanaohitimu kidato cha nne na kufaulu kupata nafasi ya kuendelea na masomo ya elimu ya juu kama ilivyo lengo la serikali.

Alisema umoja wa wazee unaamini kwamba mwenyekiti huyo ana uwezo mkubwa wa kuisimamia serikali na kuibua miradi ya maendeleo.

"Lakini pia tunashauri vijengwe vyuo vingi vya ufundi stadi ndani ya mkoa wetu ili wale vijana wanaoshindwa kuendelea na masomo ya elimu ya juu wapate ujuzi wa kuwawezesha kujiajiri, hii itatusaidia kupunguza tatizo la ajira kwa vijana wetu," alisema Polisya.

Dk. Mwakajumilo aliwashukuru wazee hao kwa ushauri walioutoa kwa maelezo kuwa utasaidia kuboresha baadhi ya maeneo ambayo yalikuwa hayatekelezwi vizuri.

Alisema uwepo wa wazee hao unawaongezea maarifa viongozi huku akisisitiza kuwa ushauri waliotoa utazingatiwa na chama hicho .

Hivyo aliwataka wazee hao kuendelea kushirikiana na chama ili kuuletea maendeleo ya mkoa huo na taifa kwa ujumla.




Kamishna Msaidizi wa Polisi Mkoa wa Mbeya ACP, Benjamini Kuzaga akionyesha baadhi ya nyara za Serikali ambazo ni pembe za Ndovu zilizokamatwa kati ya Desemba mosi mpaka 23 mwaka huu wilayani Chunya baada ya kufanya opareshenі maeneo mbalimbali ya mkoa wa Mbeya. **PICHA:GRACE MWAKALINGA**

# Dk. Tulia awataka wanachama CCM kuacha majungu

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

Mbunge wa Mbeya, Dk. Tulia Ackson amewataka wanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), mkoani Mbeya kuacha majungu na badala yake wafanye kazi ya kukijenga chama hicho ili kiendelee kukubalika.

Aidha, amewataka wananchi wanaobeza michango ya baadhi ya wadau kuacha tabia hiyo kwa maelezo kuwa vitendo hivyo vinawakatisha tamaa wenye moyo wa kujitolea.

Alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki wakati wa Mkutano Mkuu Maalumu wa chama hicho Wilaya ya Mbeya Mjini ambao ulilenga kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya uchaguzi ya chama hicho.

Alisema baadhi ya wanachama wa chama hicho wamekuwa wakikosoa na kubeza hata shughuli za maendeleo zinazotekelezwa na viongozi wa kitaifa hali ambayo alisema inaleta sintofahamu miongoni mwa wananchi.

Vilevile alisema ukosoaji huo unasababisha wananchi kutokiamini chama pamoja na viongozi wake jambo ambalo alisema halina tija yoyote kwa taifa.

"Nawaomba wananchi wa Mbeya Mjini muendelee kuniunga mkono kwenye shughuli mbalimbali za ujenzi wa taifa, tunaendelea na ujenzi wa miundombinu mbalimbali ikiwamo vyumba vya madarasa, barabara na vituo vya afya," alisema Dk. Tulia.

Vilevile aliwataka wananchi hao kuendelea kumuunga mkono Rais Samia katika shughuli mbalimbali za maendeleo ambazo anazifanya kwa taifa.

Pia aliwataka viongozi wa chama na Serikali katika mkoa huo kuhakikisha wanamsaidia Rais Samia Suluhu Hassan kuelezea miradi ya maendeleo inayotekelezwa ili wananchi waifahamu.

Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Mbeya Mjini, Afrey Nsomba alimpongeza Dk. Tulia kwa kuwakilisha vizuri chama hicho kwa maelezo kuwa amekuwa akifanya kazi nzuri ya kuliongoza Bunge.

Alisema mbali na kuliongoza Bunge pia amekuwa akifanya shughuli mbalimbali za maendeleo ndani ya jimbo hilo ikiwamo uboreshaji wa miundombinu ya elimu na afya.

Nsomba alisema Dk. Tulia amekuwa akitumia fedha zake kujenga miundombinu ya elimu na afya kupitia fedha anazokusanya kwenye mashindano ya mbio yanayoandaliwa na taasisi yake ya Tulia Trust.

Naibu Waziri wa Maji, Maryprisca Mahundi ambaye pia ni Mbunge wa viti maalumu wa Mkoa wa Mbeya alisema Dk. Tulia amekuwa kiongozi ambaye amekuwa akivumilia mambo mbalimbali.

Alisema baadhi ya wananchi wamekuwa wakimbeza na kumkosoa bila staha lakini amekuwa akiwavumilia kwa sababu yeye nia yake ni kuleta maendeleo kwa wananchi na siyo kupambana na watu.

Alisema yeye kama mmoja wa wabunge wanaotoka ataendelea kumpambania ili kuhakikisha anafanikiwa katika jitihada zake za kuleta maendeleo.

# Wawili mbaroni kwa kukutwa na silaha za kienyeji

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya linawashikilia watu wawili akiwamo dereva bodaboda kwa tuhuma za kumiliki silaha za moto zilizotengenezwa kienyeji.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi wa Polisi Benjamin Kuzaga aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Tizo Nelson (34) dereva bodaboda na mkazi wa Makongolosi wilayani Chunya na Damian Thomas (40) ambaye pia ni mkazi wa Makongolosi.

Alisema watuhumiwa hao walikamatwa wakati wa msako maalumu uliofanywa na makachero wa Jeshi la Polisi kuanzia Desemba mosi hadi Desemba 25 mwaka huu katika maeneo mbalimbali ya mkoa huo.

Alisema watuhumiwa hao walikutwa wakimiliki bunduki tatu aina ya gobore yaliyotengenezwa kienyeji, risasi 50 pamoja na mafataki 32 ambayo pia huwa yanatumika kwenye silaha hizo.

"Watuhumiwa wanaendelea kuhojiwa ili kufahamu silaha hizo walikuwa wanazitumia kwenye matukio gani, tuliwakamata baada ya kupata taarifa za siri kutoka kwa wasamalia wema, hawa ni lazima tuwafikishe mahakamani kwa hatua zaidi," alisema Kamanda Kuzaga.

Katika hatua nyingine Kamanda Kuzaga alisema katika kipindi hicho cha siku 25 Jeshi la Polisi liliwakamata watu 12 wa matukio mbalimbali ya mauaji yaliyotokea mkoani humo.

Alisema kati ya watuhumiwa hao waliokamatwa watano wameshafikishwa mahakamani kwa hatua zaidi za kisheria huku watuhumiwa wengine wakiwa wanaendelea kuhojiwa kwa ajili ya kukusanya ushahidi kabla ya kupelekwa mahakamani.

Kamanda Kuzaga alisema kuwakamata watuhumiwa wa matukio hayo ni sehemu ya mafanikio ya Jeshi la Polisi katika harakati za kudhibiti uhalifu katika kipindi hiki cha sikukuu za mwisho wa mwaka.

Hata hivyo Kamanda Kuzaga alisema katika kipindi cha kuanzia Desemba mosi mpaka Desemba 23 mwaka huu zilifunguliwa kesi 219 zilizokuwa zinahusisha makosa mbalimbali.

Alisema baadhi ya kesi hizo zilikuwa zinahusu mauaji na zingine zilikuwa zinahusu kupatikana na nyara za serikali ambazo zilikuwa zimepatikana kutokana na uwindaji haramu.

Alisema kati ya kesi hizo 219, 56 Jeshi la Polisi lilipata mafanikio kwa kushinda ambapo wahusika walihukumiwa kwenda jela miaka 30 na zingine zipo katika hatua mbalimbali za kisheria.

Katika tukio lingine, Kamanda Kuzaga alisema Jeshi la Polisi linawashikilia watu wanne kwa tuhuma za kukutwa na nyara za serikali ambazo ni nyama ya tandala, nyama ya swala na mifupa ya mbuni. Aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Fikiri Shega, Lucas Balton, Christopher Mwankina na Gelvas Kinyaga ambao wote walifikishwa mahakamani na kuhukumiwa kwenda jela miaka 20.

Aliwataka wananchi wa mkoa huo kuendelea kutoa taarifa za siri wanapowaona wahalifu ili wadhibitiwe kabla hawajatekeleza uhalifu wao.

Kamanda Kuzaga alisema Jeshi la Polisi litaendelea kufanya doria katika maeneo mbalimbali katika kipindi hiki cha sikukuu za mwisho wa mwaka ili kuzuia wahalifu kutekeleza uhalifu wao.



HABARI DODOMA

## TAG yawakumbuka yatima, wajane Sikukuu Krismasi

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

KANISA la TAG Upendo Revival Christian Center Area 'D' Dodoma limetoa msaada wa zaidi ya Sh. milioni 30 kwa ajili ya kuwapatia zawadi watoto yatima, waishio katika mazingira magumu, na wajane kwa ajili ya Sikukuu ya Krismasi.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kukabidhi misaada hiyo, Askofu wa kanisa hilo, Dk. Vangast Salumu, alisema misaada hiyo imetolewa kwa makundi hayo ikiwa ni sehemu ya kutimiza maandiko matakatifu yanayoeleza kuwa dini iliyo safi ni ile inayojali yatima, wajane na wenye uhitaji.

Dk. Vangast alisema kanisa licha ya kuwalinda watu kiroho, lakini pia wana wajibu wa kuwalinda kimwili kwa kuwawezesha wenye uhitaji wa mambo mbalimbali ili nao wajione kuwa sawa na watu wengine wenye familia zinazojiweza.

"Leo ni sikukuu ya kumbukizi ya kuzaliwa kwa Yesu Kristo na familia nyingi zinasherehekea, lakini kuna familia zisizo na uwezo wa kujumuika na kufanya sherehe.

"Kutokana na hali hiyo kanisa la mahali pamoja la (URCC) wameandaa chakula cha pamoja na watoto yatima, wajane, wagane na watoto waishio katika mazingira magumu huku wakiwa wamenunua jozi 400 za viatu, mabegi 400 kwa ajili ya wanafunzi pamoja na doti 100 za vitenge kwa ajili ya wahitaji.

"Vifaa hivyo vitawafanya wahitaji hao kujisikia wapo salama na wenye furaha ya kusherehekea sikukuu ya kumbukizi ya kuzaliwa kwa Yesu Kristo na pindi shule zitakapofunguliwa watoto watakwenda shule bila kuwa na wasiwasi," alisema Dk. Vangasti.

Akizungumzia 2023, alisema ni mwaka wa ujasiri na kuwezesha mataifa mengine kwa kuhakikisha taifa linakuwa na ujasiri katika utafutaji na kuandaa malighafi ambazo zinazalishwa nchini badala ya kutegemea misaada kutoka nje ya nchi.

Naibu Katibu Mkuu wa kanisa la Pentecostal Holiness Association Mission Tanzania (PHAM (T) Julius Bundala, aliwashauri watumishi wa serikali na washauri wa Rais kufanya kazi kwa mazingira ya haki na uwazi badala ya kuwa waongo na wabinafsi.

"Tumeona kipindi ambacho Rais Samia Suluhu Hassan alipoingia madarakani amekutana na changamoto mbalimbali, lakini ameweza kuzitatua na nyingine bado anaendelea nazo, kinachotakiwa ni kuwa wasaidizi wake wanatakiwa kuhakikisha wanamlinda na kumshauri katika kweli ili aweze kutatua matatizo ambayo yanaendelea kulikabili taifa ikiwa ni pamoja na kuimarisha uchumi wa Watanzania," alisema.

# Dodoma yaweka mikakati kukabiliana utoro wanafunzi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKOA wa Dodoma umeweka mikakati ya kukabiliana na utoro wa wanafunzi shuleni kupitia azimio waliloweka kwa mwaka 2023 kwenye kikao cha pili cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa (RCC), kilichofanyika chini ya Mwenyekiti wake Rosemary Senyamule, Mkuu wa mkoa huo.

Katika kikao hicho, agenda nane zilijadiliwa ikiwamo masuala mbalimbali ya maendeleo, bajeti ya mkoa, elimu, afya, kilimo, maji na mazingira.

Mkoa wa Dodoma unakabiliwa na kero kubwa ya utoro kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari huku sababu kubwa zikitajwa kuwa ni ukosefu wa chakula shuleni.

Pia, wazazi na walezi kutoipa thamani elimu na kutowajibika kwa malezi ya watoto wao, viongozi wa vijiji kushindwa kutimiza wajibu wao wa kudhibiti utoro shuleni na umbali mrefu wa kwenda na kurudi.

Akizungumza katika kikao hicho, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, alisema licha ya kero hizo katika sekta ya elimu, wilaya ya Bahi imefanikiwa kushika nafasi ya 10 kitaifa katika matokeo ya darasa la saba mwaka 2022.

"Naipongeza sana Halmashauri ya Bahi kwa kushika nafasi ya 10 kwa mpangilio wa ufaulu wa halmashauri kitaifa kwani wameufaharisha mkoa mzima wa Dodoma.

"Natoa shime kwa halmashauri nyingine kwenda kujifunza Bahi namna walivyofanya na kufanikiwa kuingia kwenye kumi bora za kitaifa. Pia tukafanye kazi kubwa kuhakikisha watoro wanarudi shuleni mwaka 2023," alisema Senyamule.

Katibu Tawala mkoa, Dk. Fatuma Mganga, alitoa rai kwa wakurugenzi wa halmashauri za Mkoa wa Dodoma kutoa msukumo kwa walimu kufundisha kwa bidii kwa lengo la kuongeza kiwango cha ufaulu.

Pia, katika kikao hicho Senyamule aliziagiza halmashauri kuongeza kasi ya kukusanya mapato na kutoa asilimia 10.

"Naziagiza halmashauri zote kwa kushirikiana na wadau kuendelea kutengeneza madawati ili kupunguza upungufu uliopo, halmashauri zikamilishe usimamizi wa sheria ndogo ndogo za upatikanaji wa chakula shuleni pamoja na kudhibiti utoro, kila shule itenge eneo la kuzalishia chakula kwa wanafunzi, vyuo vya ufundi viimarishwe," alisisitiza Senyamule.

Akitoa maoni ya azimio la mwaka 2023, Ofisa Elimu Mkoa Gift Kyando, alisema mwaka ujao wameazimia wanafunzi wote watakaomaliza elimu ya msingi kurudi mapema shuleni kwa ajili ya kujiandaa na masomo ya kidato cha kwanza tofauti na ilivyokua mwaka huu.

"Mwaka huu mitihani ilichelewa badala ya kufanyika mwezi Septemba imefanyika mwezi Oktoba ila mwakani itafanyika kama kawaida mwezi Septemba," alisema.



Baadhi ya watoto pamoja na walezi wao wakiwa viwanja vya Nyerere Square jijini Dodoma ikiwa ni shamrashamra ya Sikukuu ya Krismasi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Tisa wazaliwa mkesha wa Sikukuu ya Krismasi

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

WATOTO tisa wamezaliwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma kwenye mkesha wa Sikukuu ya Krismasi.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma, Dk. Ernest Ibenzi, alisema idadi ya watoto waliozaliwa usiku wa kuamkia Sikukuu ya Krismasi kati yao wa kiume ni wanne na wakike watano huku afya zao zikiendelea vizuri.

Alisema kati ya watoto hao, mapacha wote ni wa kiume.

Kadhalika, alisema hospitali hiyo imejipanga vizuri kutoa huduma bora kwa wagonjwa wanaofika ikiwa ni pamoja na kinamama kupata huduma za kujifungua.

Muuguzi wa zamu wodi ya watoto jengo la Mama na Mtoto, Furaha Mbwilo, alisema kinamama watano walijifungua kwa njia ya kawaida na watatu kwa upasuaji.

Pia, alisema yupo mama aliyejifungua mapacha na afya zao zinaendelea vizuri.

Alisema afya za kinamama waliojifungua kwa njia ya kawaida na upasuaji zinaendelea vizuri na wataruhusiwa kuondoka baada ya madaktari kuwaruhusu.

Alisema utaratibu wa kutoa chanjo kwa watoto waliozaliwa hospitalini ulifanyika na wote wamepata kinga zao za magonjwa mbalimbali.

Mmoja wa kinamama waliojifungua hospitalini hapo, Abigael Muhoya, mkazi wa Chang'ombe, alieleza furaha ya kumpata mtoto wake wa kiume kwenye sikukuu hiyo.

Abigael alisema alihudumiwa vizuri na madaktari pamoja na wauguzi waliokuwa zamu na kuwashukuru.

"Kwakweli nimefurahi kupata mtoto wangu wa kiume salama, sikupata kikwazo chochote na ninawashukuru sana watu wa afya kwa kutuhudumia kinamama tunaofika kupata huduma hapa," alisema.





# 'Zanzibar inakabiliwa na janga la ukosefu wa maadili'

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema Zanzibar imekabiliwa na janga kubwa la ukosefu wa maadili hali inayosababisha baadhi ya watumishi kufanya vitendo vya kifisadi kupitia dhamana zao za kazi.

Aliyasema hayo jana Kiembesamaki Wilaya ya Magharib Unguja wakati akifungua mkutano mkuu wa tano wa mwaka wa Madrasat Hayaatul Atfaal ya Baghani Wete Pemba.

Othman alisema watu wanaofanya vitendo vya kuiba mali za serikali siyo wale walioishia darasa dogo la elimu lakini wengi wao ni wasomi wenye elimu ya juu na wanafanya hivyo kutokana na kutolelewa katika maadili mema yanayotokana na muongozo wa dini.

Hivyo aliitaka jamii kuhakikisha kwamba wanawaandaa vijana katika maadili kwa kuwafundisha tabia njema za kumcha Mungu ili kuwa watu wema.

Alisema jukumu la malezi bora yenye maadili ni wajibu wa wazazi wenyewe na siyo busara jambo hilo kuachwa kwa walimu pekee ama kuonekana kwamba ni jukumu la serikali.

Othman alisema kwamba Zanzibar inahistoria katika kufuata mila na tabia njema zinazotokana na muongozo wa dini na kwamba bila jamii kujitahidi kuwalea vyema vijana upo uwezekano wa maadili ya Zanzibar kupotea.

Naibu Kadhi Mkuu wa Zanzibar, Shekhe Othman Ame Chum, alisema kwamba Zanzibar inavipaji vingi vya watoto na kwamba walimu wanaendelea na kazi kubwa ya kuvilea na kuvikuza vipaji hivyo.

Alisema matatizo ya ukosefu wa maadili iliyopo Zanzibar kwa vijana kujiingiza kwenye vitendo viovu kama vile vya utumiaji wa dawa za kulevya, udhalilishaji dawa yake siyo kuwapo kwa sheria kali bali ni kuwajenga watoto na jamii katika maadili mema.

Akisoma risala, Rashid Sinan alisema kwamba pamoja na madrasa kutoa mashekhe na walimu lakini imekabiliwa na matatizo mbalimbali ikiwamo viti, vifaa vya kufundishia kwa mfumo wa kisasa.



Baadhi ya wanachama wa Klabu ya Waandishi wa Habari Zanzibar wakimsikiliza Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Tabia Maulid wakati akifungua mkutano mkuu wa chama hicho jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Muswada Sheria ya Habari Zanzibar wakamilika

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, Tabia Maulid Mwita, amesema kuwa kikao kijacho cha Baraza la Wawakilishi kinatarajia kupokea Muswada wa Sheria ya Habari ambao utasomwa kwa mara ya kwanza.

Aliyasema hayo jana wakati akifungua mkutano mkuu maalum wa Klabu ya Waandishi wa Habari Zanzibar (ZPC).

Alisema maoni yote ya wadau wa habari waliyoyatoa wakati wa uandaaji wa muswaada huyo yatafanyiwa kazi, kwamba kukamilika kwa sheria hiyo itawasaidia waandishi wa habari katika kutekeleza majukumu yao vizuri.

Alisema serikali imejiandaa kuhakikisha kwamba uandishi wa habari unakwenda kutambulika kama kada inayojitegemea na kuheshimika, siyo kwa sababu ya umuhimu wake pekee bali mchango wake katika maendeleo ya nchi na ustawi wa jamii kwa ukubwa wake.

Tabia alisema waandishi wa habari hasa wa sekta binafsi wanakabiliwa na matatizo mengi ikiwamo kufanya kazi bila ya mikataba.

Alisema ni lazima vyombo vya habari vitambue na kuthamini kazi ngumu zinazofanywa na waandishi wa habari.

"Kukamilika kwa sheria hii kutawabana na kuwawajibisha wamiliki wa vyombo habari ambao wanawatumia waandishi wa habari bila ya mikataba ya kazi wala stahiki zingine ikiwamo mishahara kwa ajili ya kujikimu kimaisha,"alisema.

Pia, aliitaka ZPC kuzitumia fursa zilizopo katika kuimarisha ujuzi, taaluma na weledi wa waandishi wa habari.

Alisema hatua hiyo itaimarisha uhuru wa kujieleza na kupata habari mambo ambayo Serikali ya Zanzibar na Tanzania imeitambua kisheria na kikatiba.

"Niwaombe wanahabari kutumia vyema fursa ya uwapo kwa taasisi hii kwa kujiunga nayo ili fursa za mafunzo na nyingine za kuimarisha ujuzi kazi na maarifa zisiwapite,"alisema.

Alisema wizara yake itaimarisha uchumi wa vyombo vya habari ili kuajiri watu wengi na kuchangia katika ahadi ya ajira laki tatu zilizoahidiwa kwenye ilani ya uchaguzi ya CCM.

Mwenyekiti wa ZPC, Abdallah Abrahman Mfaume aliwataka waandishi wa habari kuendelea kufanya kazi zao kwa kuzingatia maadili ya taaluma yao na kufuata sheria zikizopo.

Aidha, aliwataka waandishi kuendelea na majukumu yao ili kuendelea kuwa daraja na kukosoa pale penye kasoro na serikali kuzifanyia kazi kasoro hizo.

# Watu wenye ulemavu bado wanahitaji vifaa visaidizi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

Katibu Mkuu Wizara ya Maendeleo Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Abeida Rashid Abdalla amesema msaada wa vifaa saidizi kwa watu wenye ulemavu ni muhimu katika kuwasaidia kwenye maisha yao ya kila siku.

Aliyasema hayo jana wakati akimkabidhi vifaa visaidizi, Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Khamis Abdallah Said, uliotolewa na Ubalozi wa Falme za Kiarabu, hafla iliyofanyika katika Ofisi ya Wizara ya Afya.


Alisema visaidizi hivyo vimetolewa kwa ajili ya kuwasaidia wanafunzi wenye ulemavu wa kuona, wenye ulemavu wa Ngozi, pamoja na magari ya magurudumu mawili.

Aidha, alisema kuwa msaada huo utawasaidia katika Maisha yao ya kila siku, huku akiwaomba watu wengine wenye uwezo kujitokeza kuwasaidia watu wenye ulemavu ili nao waishi kama watu wengine.

Naye Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Khamis Abdallah Said aliishukuru Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kwa kuwapatia visaidizi hivyo ambavyo vitawasaidia wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wasioona Zanzibar, Fatma Jinjaa Chesa aliishukuru wizara hiyo kwa kuendelea kuiunga mkono katika kuhakikisha inapata visaidizi.

Alisema watu wenye ulemavu wanakabiliwa na matatizo mengi ikiwemo visaidizi ambavyo ni muhimu kwa sababu miundombinu siyo rafiki kwao.





Dampo lililopo katika mtaa wa Majanimapana kata ya Nguvumali, jijini Tanga likiwa na taka zilizorundikana na kuleta adha ya harufu kali kwa wakazi wa mtaa huo na wapita njia kama lilivyokutwa jana. **PICHA: DEGE MASOLI**

# FPCT latoa msaada kwa wafungwa Gereza la Geita

**Na Alphonce Kabilondo,** GEITA

KANISA la Free Pentekoste Church Tanzania (FPCT) Jimbo la Geita limetoa msaada wa vitu mbalimbali kwa wafungwa wa Gereza la Wilaya ya Geita ili kuwawezesha kusherehekea Sikukuu ya Krismasi na Mwakampya.

Msaada huo ni sabuni, sukari, mafuta ya kupikia ,mchele pamoja na ng'ombe.

Askofu wa FPCT, David Nzumbi akikabidhi msaada huo alisema kuwa kanisa hilo limeamua kutoa msaada wa vitu hivyo vikiwa na thamani ya Sh. milioni 100.

Askofu Nzumbi alisema msaada huo umetokana na michango ya waumini wa kanisa hilo uliotokana na utaratibu wa kanisa hilo kila mwaka kuwatembelea wafungwa waliopo gerezani na kufanya nao ibada, kuwajulia hali na kuwatia moyo pamoja na kuwasaidia mahitaji mbalimbali.

"Tumetimiza maandiko matakatifu kutoka Kitabu cha Mathayo 26:36 tunaamini kuwa nao ni sehemu ya jamii wamo pia watumishi wanamtumikia Mungu,"alisema Askofu Nzumbi .

Katibu wa wanawake wa kanisa Jimbo la Geita, Justina John alisema katika kusherehekea Sikukuu ya Krisimasi wanaungana na waumini wenzetu kuwajulia hali wafungwa na kuwapatia mahitaji mbalimbali .

Mkuu wa Gereza la Wilaya ya Geita, Mrakibu Mwandamizi wa Jeshi la Magereza, SSP Jovin Bujwina alilipongeza kanisa hilo kwa msaada huo na kuyaomba madhebu mbalimbali ya dini kuiga mfano wa kanisa hilo.

Alisema waumini wa kanisa hilo wamefanya jambo jema la kuwasadia wafungwa hao kwa sababu nao wanastahili huduma sawa na wengine na siyo kuwatenga kwa kuwa nao bado ni sehemu ya jamii.

## Watoto 11 wazaliwa mkesha wa Krismasi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WATOTO 11 wamezaliwa katika Kituo cha Afya Kambarage kilichopo katika Manispaa ya Shinyanga wakati wa mkesha wa Sikukuu ya Krismasi.

Kati ya watoto hao wakike ni wanne na wakiume ni saba na wote wamezaliwa wakiwa na afya njema.

Akizungumza na waandishi wa habari, Muunguzi Wodi ya Wazazi katika kituo hicho, Onesmo Godwin, alisema siku hiyo ya mkesha wa Sikukuu ya Krismasi walizaliwa idadi ya watoto hao na wote wana afya nzuri.

"Natoa wito kwa kinamama wajawazito wapende kujifungulia kwenye vituo vya afya sehemu ambayo ni salama kabisa, pamoja na kuhudhulia kliniki ili kujua maendeleo ya mtoto ili kupunguza vifo vya mama na mtoto vitokanavyo na uzazi,"alisema Godwin.

Mganga Mkuu wa Manispaa ya Shinyanga Dk. Elisha Robert, alisema, Kituo cha Afya Kambarage kwa sasa huduma zake zimeboreshwa na kinatoa huduma ya upasuaji.

Aidha, alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutoa fedha na kuboresha huduma za afya hapa nchini ili wananchi waweze kupata matibabu na kuimarisha afya zao pamoja na kupunguza vifo vya uzazi.

Baadhi ya wazazi ambao wamejifungua watoto wao walifurahi kupata watoto siku moja na maadhimisho ya kuzaliwa kwa Yesu Kristo.

Pia waliwapongeza wahudumu pamoja na huduma nzuri walizopata kabla ya kujifungua na baada ya kujifungua.

# Wazazi, walezi watajwa chanzo utoro kwa wanafunzi

**Na Shaban Njia,** KAHAMA.

BAADHI ya wazazi na walezi katika Halmashauri ya Msalala mkoani Shinyanga wametajwa kuwa chanzo cha utoro kwa wanafunzi shuleni kutokana na kutumia sababu ya kuwaombea ruhusa na kwenda kuwatumikisha katika shughuli za kilimo na ufugaji wa mifugo kipindi cha masomo.

Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Shilela, Daniel Paul aliyabainisha hayo juzi katika mdahalo wa ushiriki wa wanaume na vijana katika kupambana na ukatili wa kijinsia kutoka Kata ya Lunguya na Shilela, uliondaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) kwa ushirikiana na Shirika la Kimataifa la UNFPA.

Alisema wazazi wamekuwa wakifika shuleni kwa nyakati tofauti hasa katika kipindi cha mvua za masika na kutoa sababu za ugonjwa juu ya watoto wao.

Alisema wanapofuatilia juu ya taarifa hizo wanabaini watoto hao wako shambani na wengine wakiendelea kuchunga mifugo.

Aidha, alisema baada ya kuona hali hiyo imekithiri waliamua kuweka makubaliano ambayo yatakuwa yakiwabana wazazi wasio wadilifu wanaokatisha ndoto za watoto wao kwa kuwaripoti katika uongozi wa Serikali ya Kijiji kwa hatua za kisheria.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Ndola, Charles Shabani alikili kuwapo kwa baadhi ya wazazi wasiokuwa wadilifu wanaowachukua wanafunzi kipindi cha masomo na kuwapeleka shambani na pale anapopata taarifa anawawajibisha kisheria na kuhakikisha mtoto anarejea shuleni kuendelea na masomo yake.

Alisema sababu ngingine inayochochea kuwapo kwa vitendo vya kikatili ni mila na desturi potofu ya mfumo wa mwanaume wa kutoa mahali na kuoa baada ya ndoa huwatumikisha wake zao katika kilimo kama vibarua bila kupumzika na wanapovuna mazao mwanamke hana sauti yoyote juu ya kilichopatikana.

"Ili kuondoa unyanyasaji huu ni vema elimu ikatolewa kwa wingi katika maeneo ya vijijini ambapo ndipo ukatili unafanyika zaidi, familia nyingi hazijaelimika na pale zinapofanyiwa ukatili hazifahamu mifumo sahihi ya kutoa taarifa kwa ajili ya msaada wa kisheria,"alisema Shabani.

Ofisa Mradi wa TGNP, Jackson Malangalila, alisema lengo la kufanya mdahalo huo ni kuhakikisha ukatili wa kijinsia unaisha ndani ya familia na jamii kwa kushirikisha kundi la wanaume na vijana ambalo ndilo linatajwa kwa wingi kushiriki katika vitendo vya unyanyasaji kwa wanawake na watoto hususani vijijini.

Alisema kwa kushirikina na serikali wataendelea kutoa elimu ya ukatili wa kijinsia na madhara yake katika vijiji vyote vilivyopo katika kata za Shilela na Lunguya na kuwataka vijana hao kuwa mabalozi wazuri wa kutoa taarifa pale wanapoona vitendo hivyo vikifanyika.

## Namna Rais Zelensky alivyofika Washington

**WASHINGTON,** MAREKANI

HATUA za ajabu zilizochukuliwa kumsafirisha Rais wa Ukraine Volodymyr Zelensky kutoka Ukraine hadi Mji Mkuu wa Marekani ni ishara ya jinsi uhusiano huo ulivyo muhimu kwa nchi zote mbili.

Baada ya kuzuru eneo la vita mashariki mwa Ukraine, safari ya Zelensky kuelekea Washington DC ilianza kwa treni ya usiku kuelekea Poland kabla ya kupanda ndege ya Jeshi la Wanahewa la Marekani, ikiripotiwa kuungwa mkono na ndege ya kijasusi ya Nato na ya kivita ya F-15.

Taarifa za ziara hiyo ya Washington zilianza kusambaa mapema wiki iliyopita, lakini haikuthibitishwa, huku maofisa wa Marekani wakihisi kuwa kiongozi wa Ukraine alikuwa njiani salama kuelekea mji mkuu wa Marekani.

Inaelezwa kuwa kilichoshanganza ni kwamba hakuna taarifa rasmi iliyotolewa kuhusu safari.

Ilibainishwa kuwa kutokana na tishio la makombora ya Russia kufanya safari ya anga nchini Ukraine kumekuwa hatari, jambo lililosababisha Zelensky kufanya safari ya siri ya treni kutoka Ukraine hadi Poland, ikiwa ni safari yake ya kwanza tangu kuanza kwa vita.

Muda mfupi baadaye, data ya ndege ilionyesha ndege ya Jeshi la Anga la Marekani Boeing C-40B - inayodhaniwa kumsafirisha Zelensky, ikipaa kutoka uwanja wa ndege wa Rzeszow umbali wa kilomita 80 kuelekea magharibi.

Ndege hiyo ilielekea kaskazini magharibi kuelekea Uingereza, lakini kabla haijaingia kwenye anga ya juu ya Bahari ya Kaskazini, ndege ya kijasusi ya Nato ilichunguza eneo hilo. Bahari inajulikana kusimamiwa na manowari za Russia.

Vile vile inaelezwa kuwa ndege ya kivita ya Marekani F-15, iliyopaa kutoka kambi moja nchini Uingereza, ilisindikiza ndege ya Zelensky katika sehemu ya safari yake.

Baada ya takriban saa 10 ndege inayodhaniwa kumbeba kiongozi huyo ilitua saa sita mchana karibu na Washington.

Inaelezwa kwamba alipofika, alipewa ulinzi wa siri kama ilivyo kwa wakuu wote wa nchi wanaomtembelea lakini hali ya Zelensky kama kiongozi wa nchi iliyopigana na Russia ilimaanisha maofisa wa usalama walikuwa waangalifu zaidi.

Ofisa mmoja mkuu aliiambia ABC News "Tunafahamu sana kwamba Russia ina mali katika nchi hii na inaweza kujaribu kufanya kitu".

Licha ya wasiwasi huo, ziara hiyo ilionekana kupita vizuri, na kwamba Alhamisi alisimama kwa muda nchini Poland alipokuwa akielekea nyumbani kukutana na mwenzake, Andrzej Duda.

Na kufikia Ijumaa alikuwa amerejea kwenye dawati lake mjini Kyiv, akichapisha video fupi kwenye Telegram. "Tunajitahidi kupata ushindi," alisema.

**BBC**

# China: Tutaimarisha ushirikiano na Russia

**BEIJING,** CHINA

WAZIRI wa Mambo ya Nje wa China Wang Yi amesisitiza msimamo wa nchi yake wa kutofungamana na upande wowote katika vita vya Ukraine, akieleza kwamba taifa hilo litaimarisha uhusiano na Russia 2023.

Wang, aliyazungumza hayo jana katika mkutano uliofanyika kwa njia ya video jijini Beijing, huku akiilaumu Marekani kutokana na kuzorota kwa uhusiano kati ya mataifa hayo mawili makubwa kiuchumi duniani.

Pia Wang alisisitiza kuwa China itazingatia mikakati ya kuaminiana na ushirikiano na Russia kwa manufaa ya pande zote mbili.

Inabainishwa kuwa meli za kivita kutoka kwa nchi hizo mbili zilifanya mazoezi ya pamoja ya majeshi yao ya wanamaji katika Bahari ya Mashariki ya China wiki iliyopita.

Alisema China inapinga sera mbaya ya Marekani dhidi yake, huku akitaja shinikizo la nchi za magharibi dhidi ya nchi hiyo.

China inataja shinikizo kubwa katika maswala ya biashara, teknolojia, haki za binadamu na kupinga hatua ya nchi hiyo kutangaza kulidhibiti eneo zaidi la magharibi mwa bahari ya Pasifiki ni hatua za uonevu za Marekani kutokana na China kukataa kulaani uvamizi wa Russia nchini Ukraine na hatua yake ya kukataa kuungana na nchi nyingine katika kuiwekea Russia vikwazo.

"Sababu hizo zimechochea mivutano inayoendelea kujitokeza kati ya China na sehemu kubwa ya nchi za Ulaya," alisema.

Inatajwa kuwa Wang alizungumza na mwenzake wa Marekani, Antony Blinken kwa njia ya simu mwishoni mwa juma.

Wizara ya Mambo ya Nje ya Marekani ilisema Blinken amezungumzia juu ya kusimamia uhusiano baina ya mataifa hayo kwa kuwajibika na alielezea wasiwasi wake juu ya uvamizi wa Russia nchini Ukraine unaoathiri vibaya usalama na utulivu wa uchumi wa dunia.

Kwa mujibu wa taarifa ya Wizara ya Mambo ya Nje ya China, Wang aliilaumu Marekani kwa kupendelea upande mmoja, na kwamba China itaendelea kuchukua jukumu muhimu la kuutatua mgogoro wa Ukraine kwa njia yake yenyewe.

**DW**



Papa Francis akiwabariki waumini kwenye Uwanja wa Mtakatifu Petro. **PICHA: DW**

# Papa Francis ataka vita vya Ukraine vikomeshwe

**VATICAN CITY,** VATICAN

MKUU wa Kanisa Katoliki Duniani, Papa Francis, ametoa wito wa kukomeshwa kile alichokiita vita visivyo maana nchini Ukraine.

Papa Francis aliyasema hayo juzi katika ujumbe wake wa Krismasi alioutoa akiwa katika Kanisa Kuu la Mtakatifu Petro mjini Vatican.

"Mungu atupe ufunuo wa kutoa ishara za dhati za mshikamano kuwasaidia wale wanaoteseka, na azitie nuru nafsi za wale wenye nguvu wanyamazishe mirindimo ya silaha na wakomeshe vita hivi visivyo maana haraka sana," alisema. Pia alitumia hotuba hiyo kutaka pakomeshwe mbinu ya kutumia chakula kama silaha, akitaja jinsi vita nchini Ukraine vilivyowatia kwenye hatari ya njaa watu wote ulimwenguni.

"Tunajua kuwa kila vita husababisha njaa na hutumia silaha kama chakula... natuanze na wale wenye nafasi za kisiasa kwa kuwataka wajitolee kukifanya chakula kuwa nyenzo ya amani na sio vita," alisema.

Hata hivyo, inatajwa kuwa amekuwa akikosolewa na baadhi ya watu kwa kutokujitokeza waziwazi kumkosoa Rais wa Russia, Vladimir Putin kwa kuanzisha vita hivyo, badala yake amejikita tu kwenye kuzungumzia madhara yanayotokana na vita hivyo.

Kwenye mahojiano yaliyochapishwa mwishoni mwa Novemba katika gazeti la Jesuit la Marekani, Papa aliulaani ukatili wa vikosi vya Russia nchini Ukraine, kauli ambayo ilisababisha Russia itoe malalamiko rasmi dhidi yake.Aidha, kiongozi huyo alitoa wito kwa watu kuachana na pumbazo la kilimwengu na kugundua maana halisi ya Krismasi katika zama hizi za matumizi ya anasa, akitetea kuwepo kwa Kanisa linalowahudumia watu masikini. **DW**

# HABARI PICHA





Wakazi wa Dar es Salaam wakisherehekea Krismasi katika ufukwe wa Coco jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**











# LULU DIVA: NAPENDA KUPENDWA, KUPEWA PESA

**Na Mwandishi Wetu**

MMOJA wa mastaa wa kike wa muziki wa Bongo Fleva, Lulu Diva, amebainisha kuwa katika mahusiano yake yeye anapenda sana kupendwa kupitiliza, kudekezwa na kupewa pesa.

Lulu ambaye kwa sasa ana ngoma yake mpya nikupe yenye wiki mbili tu iliyo kwenye mfumo wa 'audio', amesema kupewa pesa haimaanishi kwamba yeye anapenda sana pesa, bali amesisitiza bila pesa mapenzi hayanogi.

"Yaani mimi napenda kupendwa sana, napenda kupendwa kupitiliza, napenda kupewa pesa," akaangua kicheko halafu akaendelea.

"Haimaanishi kama napenda sana pesa, ni kunihudumia, najua mapenzi si pesa, bila pesa mapenzi yanaenda, lakini pesa ikiwamo ndani yake mapenzi yananoga, ni sawa na gari haiwezi kwenda bila mafuta, lakini hata kama gari haina maji nayo kuna tatizo pia lazima yawapo, sasa kusudi vitu vinoge lazima mpunga uwapo hata kama siyo sana, lakini kusiwe pangu pakavu kabisa," alisema staa

# TID akumbusha Januari inakuja

**Na Mwandishi Wetu**

MSANII mkongwe nchini wa muziki wa Bongo Fleva, Khalid Mohamed maarufu TID, amewatahadharisha mastaa wenzake na wananchi wote kwa ujumla kutumia pesa kwa kiasi kwani mwezi unaokuja Januari nao unahitaji pesa nyingi kuliko hata ilivyo kwa Desemba hiii.

TID ambaye mashabiki wake walimpachika jina la Top in Dar amesema baadhi ya watu wanajisahau sana na kufanya matanuzi sana Desemba na kujisahau kama Januari ndiyo mwisho wa matatizo.

"Januari ndiyo mpango mzima, najua umenunua mbuzi, umeenda wapi sijui umefanya kila kitu, mwezi Desemba ni wa kukamua, sasa msijisahau, Januari kuna ada, kodi na vitu vingi. Msinipigie simu, ooh niazime milioni moja nimlipie mtoto ada sitaki kabisa stresi, jipangeni Januari inakuja, jipangeni Januari hiyo baba," alisisitiza TID.





# *Diamond alazwa, mashabiki wahaha*

**Na Mwandishi Wetu**

SIKUKUU ya Krismasi ya mwaka 2022 haijamuendea vizuri, staa wa muziki Tanzania na Afrika kwa ujumla, Diamond Platnumz, kwani kwenye intastori yake, ameshea video akiwa kitandani hospitalini amelazwa akipatiwa matibabu mbalimbali, ikiwamo kuchomwa sindano na kutundikiwa dripu.

Kwenye video ambazo ameziishea mwenyewe kwenye ukurasa wake wa Instagram, akieleza hayo kuwa mwaka huu haukuwa mzuri kwake kwenye sikukuu hii ya Noeli kwani amesherehekea akiwa kitandani.

Video hiyo tangu juzi jioni sikukuu ya Krismasi imekuwa 'ikitrendi', ikizua gumzo na taharuki pia kwa mashabiki wake na muziki wa Bongo Fleva kwa ujumla.

Hata hivyo, Bongo hakukosekani maneno, kwani baadhi ya mashabiki wanadai inawezekana ikawa ni mpango uliotengenezwa kimkakati kwa ajili ya kuzuia kuongelewa au kufuatiliwa kwa shoo ya hasimu wake kimuziki, Harmonize aliyekuwa akiifanya siku hiyo maeneo ya Masaki, Dar es Salaam.

# KICHUYA ATOA SOMO KWA WAZAWA SIMBA, YANGA

Na Adam Fungamwango

MCHEZAJI Shiza Kichuya wa Namungo amewashauri wachezaji wa Kitanzania kutoogopa kusajiliwa na timu kubwa kama Simba, Yanga na Azam kwa sababu eti hawatopata namba, akidai hata Watanzania nao wana uwezo wa kuwaweka nje mapro.

Kichuya ambaye ameshawahi kuichezea Simba mara mbili kwa nyakati tofauti alionyeshwa kushangazwa na baadhi ya watu waliowakatisha tamaa wachezaji vijana wanaotaka kusajiliwa na timu kubwa wakiwatisha kuwa hawatokwenda kucheza kwani zina wachezaji wengi kutoka nje ya nchi.

"Tusiogope kusajiliwa eti kwa sababu tutakaa nje hapana, kuna wazawa wanacheza na wanawaweka nje wageni, tunaona wazawa wanakwenda Simba na Yanga wanakutana na changamoto wa moto wa wageni, nao baadhi ya wageni pia wanakutana na Watanzania ambao wamekomaa kwenye nafasi zao. Jitihada zako zitamfanya mchezaji wa nje naye akae akutazame wewe, na hilo linawezekana, naamini sisi Watanzania tunajua soka," alisema Kichuya.


**Alisema hata yeye alipokwenda Simba kutoka Mtibwa Sugar alikutana na wachezaji wakigeni, lakini kutokana na jitihada zake aliwaweka benchi.**

"Ukiona mchezaji anasajiliwa kwenye timu kubwa ujue wamemuona ana kitu, timu hizi Simba, Yanga na Azam hazisajili mchezaji hivi hivi, zikikusajili ujue una kitu, ila wachezaji wanapokwenda kule wanatakiwa waongeze juhudi zaidi ili kupata nafasi ya kumshawishi mwalimu kucheza.

"Mimi sioni cha ajabu, naona mpaka mtu anakwenda kusajiwa na timu hizo ana uwezo, kinachotakiwa wewe uendelee kuwa na kitu kilekile walichokiona au uongeze mara mbili yake, sisi tupo wengi? Kwa nini wamekusajili wewe, wameona kitu, sasa nenda kawaonyeshe hicho na kingine zaidi ambacho unacho, nenda utawaweka wagen benchi tu, ukibweteka hilo ni kosa lako sasa," alisema.

Kwenye kipindi hiki cha usajili kumekuwa na tahadhari kwa baadhi ya wachezaji wakiepuka kujiunga na klabu kubwa kwa madai kuwa zinaua viwango vyao walivyotoka nayo walikokuwa.

HAPA HUPITI...




Mshambuliaji wa Yanga, Fiston Mayele, akidhibitiwa na beki wa Azam FC, Lusajo Mwaikenda (kulia), kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa katika Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi na kumalizika kwa Yanga kushinda 3-2. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Ihefu kupoteza nyota wawili

Na Hadija Mngwai

NYOTA wawili wa Ihefu FC, Evarist Myauki na Ramadhani wapo mbioni kutimka katika klabu hiyo kutokana na ofa iliyowekwa mezani huku baadhi ya timu zikiwataka kwa mkopo.

Dirisha dogo la usajili kwa timu za Ligi Kuu Bara, Championship na First League, lipo wazi tangu Desemba 16, mwaka huu na linatarajiwa kufungwa Januari 15, mwakani, ambapo timu za ligi hizo zina nafasi ya kufanya maboresho katika vikosi vyao.

Akizungumza na Nipashe, Kocha Mkuu wa Ihefu, Juma Mwambusi, amesema kuna ofa imeshuka klabuni hapo ya wachezaji wao kutakiwa na timu nyingine huku akiahidi kukifanyia maboresho kikosi chake baada ya kupungua wachezaji.

"Wachezaji wangu Evarist na Ramadhani wamepata ofa kuna timu zimejitokeza zikitaka kuwachukua katika dirisha hili dogo linaloendelea, bado tunaendelea na mazungumzo na timu husika mpango ukikamilika ndipo tutakapoziweka wazi timu hizo.

"Pia, nahitaji kuongeza nguvu katika kikosi changu kwa kusajili wachezaji eneo la kati na ushambuliaji sehemu ambayo ndiyo nimepaangalia na kutakiwa maboresho.

"Dirisha dogo mara nyingi ni gumu kuweza kupata wachezaji kwa kuwa wengi hawapo huru wana mikataba yao, hivyo ni ngumu kumpata mchezaji yule unayemhitaji.

"Wachezaji wanaopatikana sasa hivi ni kwa ugumu sana, hivyo tunafanya maboresho kulingana na wachezaji tutakaowapata," alisema Mwambusi.

# Ntibazonkiza kuzibwa na wawili Geita Gold

Na Shufaa Lyimo

BENCHI la ufundi la Klabu ya Geita Gold, limesema linatarajia kuongeza wachezaji wawili katika msimu huu wa usajili wa dirisha dogo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Fred Minziro, alisema baada ya nyota wao, Saido Ntibazonkiza kutimkia Klabu ya Simba, pengo lake limeonekana hivyo linapaswa kuzibwa.

"Natarajia kuongeza wachezaji wawili au watatu kwa ajili ya kuziba nafasi ambazo zina mapungufu," alisema Minziro.

Kocha huyo alisema endapo mipango yake itakaa sawa, atasajili wachezaji wenye viwango ambao wataleta ushindani kwenye kikosi chake hicho.

Wakati huo huo aliwapongeza wachezaji wake baada ya kupata pointi moja katika mchezo wao wa juzi dhidi ya timu ya Kagera Sugar.

"Ninawapongeza wachezaji wangu, wameonyesha uwezo mkubwa katika mchezo wetu wa jana( juzi), tunashukuru tumepata pointi moja tukiwa ugenini," alisema kocha huyo.

Alisema baada ya mchezo huo kwa sasa wanajipanga kuelekea katika michezo yao ijayo na kudai malengo yake ni kushika nafasi za juu katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Geita Gold kwa sasa inashika nafasi ya saba kwenye msimamo wa ligi hiyo ikiwa na alama 24 baada ya kushuka dimbani mara 18 hadi sasa.



## ZISIKUPITE

### ARSENAL, MUDRYK WAKUBALIANA

Arsenal imekubaliana dili kimsingi na winga wa Ukraine, Mykhaylo Mudryk, 21, wakati huu mazungumzo kuhusu ada ya uhamisho yakiendelea na klabu ya Shakhtar Donetsk. (***Nicolo Schira)***

### GVARDIOL AGOMBEWA ULAYA

Real Madrid, Chelsea na Manchester City, zote zimemfanya beki wa RB Leipzig na Croatia, Josko Gvardiol, 20, kuwa kipaumbele chao cha kwanza katika dirisha la usajili. (***Sport - in Spanish***)

### LIVER SPURS KWA SKRINIAR

Tottenham na Liverpool ni miongoni mwa klabu za Ligi Kuu England ambazo zipo tayari kuanza mbio za kuwania saini ya beki wa Slovakia, Milan Skriniar, 27, ambaye mkataba wake Inter Milan unamalizika mwishoni mwa msimu. (***Teamtalk***)

### MARTINELLI, ARSENAL KUMALIZANA

Arsenal inakaribia kukubaliana mkabata mpya na mshambuliaji wa Brazil, Gabriel Martinelli. (***Fabrizio Romano***)

### UGARTE ATEGWA NA SPURS

Tottenham inafuatilia mustakabali wa Manuel Ugarte ndani ya Sporting Lisbon, wakati huu beki huyo raia wa Uruguay mwenye umri wa miaka 21 akiwa hajakubali kupewa mkataba mpya. (***Record)***

### KANTE AWINDWA AL NASSR

KLABU ya Saudi Arabia, Al Nassr, inavutiwa kupata huduma ya kiungo wa Ufaransa N'Golo Kante, mwenye umri wa miaka 31, wakati huu mkataba wake na Chelsea ukimalizika mwishoni mwa msimu. (***Footmercato - in French***)

### FRESNEDA AIVUTIA JUVE

Newcastle, Juventus na Borussia Dortmund ni miongoni mwa klabu zinataka kumfukuzia beki kinda Mhispania wa Real Valladolid, Ivan Fresneda, 18. (Fabrizio Romano)

### SA KULETEWA MPINZANI WOLVES

Wolves inawinda kipa mpya katika dirisha la Januari ili kutoa ushindani kwa mlinda mlango wa kimataifa wa Ureno, Jose Sa, 29. (***Express and Star***)

### VILLA YAMTAKA DANJUMA

Aston Villa imefungua meza ya mazungumzo na Villarreal kuhusu uwezekano wa kumpata winga Mholanzi Arnaut Danjuma, 25. (***Todofichajes - in Spanish***)

### SMALLING AMULIKWA INTER

Inter Milan inafikiria majira ya joto kufuata huduma ya beki wa Roma na England, Chris Smalling, 33. (***Calciomercato - in Italian***)

### FRANCA AGEUKIWA NEWCASTLE

Newcastle imefungua mazungumzo na kiungo wa Flamengo, Mbrazil Matheus Franca, mwenye umri wa miaka 18. (***Globo - in Portuguese)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# ZIDANE APIGIWA DEBE NA NYOTA BRAZIL KUINOA

**Kumbuka wachezaji kama Vinicius Jr, Casemiro na Eder Militao walicheza chini yake...**

**PARIS, Ufaransa**

KOCHA wa zamani wa Real Madrid, Zinedine Zidane, ameibuka kuwa mmoja wa makocha anayepewa nafasi kubwa ya kurithi mikoba ya Kocha wa Brazil, Tite, kwa mujibu wa gazeti la kila siku la Ufaransa la L'Equipe [via Foot01.com].

**Zidane aliiongoza Real Madrid kutwaa mataji 11, ikiwa ni pamoja na matatu ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, katika kipindi chake cha uongozi klabuni hapo. Hata hivyo, amekuwa hana klabu anayoinoa tangu 2021.**

Kocha huyo mwenye umri wa miaka 50, kwa kiasi kikubwa alitarajiwa kwenda kuchukua nafasi ya Didier Deschamps kama Kocha Mkuu wa Ufaransa baada ya fainali za Kombe la Dunia la FIFA 2022 nchini Qatar. Hata aliripotiwa kukataa nafasi ya kwenda kuinoa Paris Saint-Germain (PSG) akisubiri majukumu hayo ya 'Les Bleus'.

Sasa ingawa, inaonekana kuna mashaka juu ya nafasi ya mtaalamu huyo wa Ufaransa kuchukua mikoba ya kuinoa timu ya taifa. Kuna maoni kwamba Deschamps anaweza kuendelea na jukumu lake kama kocha wao.

Deschamps alipendekezwa kuachana na Timu ya Taifa ya Ufaransa mkataba wake utakapomalizika mwishoni mwa mwaka. Noel Le Graet, rais wa Shirikisho la Soka la Ufaransa, anasemekana kutamani kuona kocha huyo mwenye umri wa miaka 54, akiendelea na timu ya taifa.

Meneja huyo wa zamani wa Marseille, anatarajiwa kufanya uamuzi kuhusu mustakabali wake hivi karibuni. Zidane atafikiriwa kushika nafasi hiyo iwapo Deschamps ataamua kuachia ngazi, lakini hakuna uhakika kwamba atakabidhiwa kazi hiyo.

Ingawa kuna sintofahamu kuhusu nafasi yake ya kujiunga na timu ya taifa, hakika hana chaguo. Kulingana na chanzo kilichotajwa hapo juu, wasifu wake ni wa kuvutia Brazil, ambao kwa sasa hawana kocha.

'Selecao' wanawinda kocha mpya baada ya Tite kujiuzulu nafasi hiyo mwishoni mwa Kombe la Dunia la FIFA Qatar. Inaonekana Zidane ana mashabiki kadhaa katika nchi hiyo ya Amerika Kusini licha ya unyanyasaji wake kisoka dhidi yao wakati akiwa mchezaji.

Wachezaji kadhaa wa Brazil wanashinikiza kocha huyo wa zamani wa Real Madrid kuteuliwa kuwa kocha wao mpya, kulingana na ripoti. Inafaa kukumbuka kuwa wachezaji kama Vinicius Jr., Casemiro, na Eder Militao walicheza chini yake huko Santiago Bernabeu.

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 429,

MECHI KALI
MANCHESTER UTD
VERSUS
NOTTINGHAM
1 | 1.35
X | 4.76
2 | 7.88

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# MARTINELLI AKARIBIA KUJIFUNGA ARSENAL




**LONDON,** England

NYOTA wa Arsenal, Gabriel Martinelli, anakaribia kukubali mkataba mpya wa muda mrefu na klabu hiyo baada ya mazungumzo sasa kuwa katika hatua ya mwisho, kulingana na mchambuzi wa masuala ya uhamisho, Fabrizio Romano. Mkataba wa Mbrazil huyo unamalizika Juni 2024, lakini 'The Gunners' wanataka kumbakisha klabuni zaidi ya hapo.

Martinelli aliwasili katika kikosi hicho cha London Kaskazini mwaka 2019 akitokea Ituano ya Brazil na amekuwa mchezaji muhimu tangu wakati huo, akicheza mechi 104 na kuchangia mabao 38. Alishinda Kombe la FA katika msimu wake wa kwanza.

Kupanda kwa kiwango kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 hadi kujulikana hivi majuzi bado kumeonekana katika medani za kimataifa. Kocha wa zamani wa Brazil, Tite alimwita kwenye kikosi mara sita mwaka huu.

Bado haijakamilika au kukubaliwa kikamilifu, pia hakuna kilichosainiwa - lakini inakaribia.

Hiyo inajumuisha kucheza mechi tatu Kombe la Dunia la Fifa 2022 nchini Qatar. Alicheza dakika 111 pekee, ingawa, alianza mechi moja wakati wakipoteza kwa bao 1-0 dhidi ya Cameroon katika mchezo wa mwisho wa hatua ya makundi.

Romano alisema mkataba huo mpya haujakamilika au kukubaliwa bado, na hakuna chochote ambacho kimetiwa saini, lakini pande zote mbili zinakaribia kumalizana. Aliongeza kuwa Bukayo Saka na William Saliba ni vipaumbele kwa Arsenal pia katika suala la kusaini mkataba mpya, na wachezaji wote wawili walivutia msimu huu.

Akiwa na mabao manne na asisti sita, Saka amekuwa na mabao mengi zaidi kikosini nyuma ya Gabriel Jesus pekee huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21, akiibuka kinara katika safu ya ushambuliaji ya Arsenal.

# Barca kumuuza Raphinha



**BARCELONA,** Hispania

KWA mujibu wa Toni Juanmarti, Barcelona inataka kumuuza Raphinha mwishoni mwa msimu, ambaye alitua klabuni hapo majira ya joto kwa kitita cha Euro milioni 65 akitokea Leeds United.

Klabu hiyo ya Katalunya, iliipiku Chelsea katika mpango wa kumsajili Mbrazil huyo. Pia Barca iliongeza mkataba na Ousmane Dembele wiki chake baadaye ambapo wawili hao wamekuwa wakiwania namba katika winga ya kulia chini ya Xavi Hernandez. Hata hivyo, Xavi amekuwa akipenda kutoa nafasi kwa Dembele na kumtumia Raphinha kama mtokea benchi ama winga ya kushoto kwa kipindi kirefu cha msimu.

Kiwango cha Raphinha hata hivyo kimekuwa kidogo pia. Katika mechi 18, amefunga mabao mawili pekee na kutoa pasi za mwisho nne tu. Ni 10 tu kati ya hizo ambazo Mbrazil huyo ameanza.

Kambi ya mchezaji huyo inataka kuishawishi klabu hiyo kwamba itachukua muda kidogo kwa Raphinha kuweza kuzoea matakwa ya mbinu za klabu hiyo ya Katalunya. Wamewatolea mfano wapinzani wakubwa wa 'Blaugrana', Vinicius Jr wa Real Madrid.

Baada ya kuhaha kwa misimu michache, hatimaye winga huyo aliibuka msimu wake wa mwisho. Raphinha yupo tayari kubaki Katalunya na kambi yake inaamini kuwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, anaweza kubadilisha bahati yake.

## HABARI MICHEZO


,669,290

JACKPOT
MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 28/12/22 | 17:00 | Troyes vs Nantes | 2.34 | 3.48 | 2.78 |
| 02. 28/12/22 | 17:00 | Istanbulspor vs Kasimpasa | 2.78 | 3.53 | 2.31 |
| 03. 28/12/22 | 22:00 | Portimonense vs Casa Pia Atletico | 2.36 | 3.14 | 2.99 |
| 04. 28/12/22 | 22:45 | St Johnstone vs Hearts | 2.85 | 3.15 | 2.46 |
| 05. 28/12/22 | 22:45 | Livingston vs St Mirren | 2.32 | 3.38 | 2.88 |
| 06. 29/12/22 | 17:00 | Giresunspor vs Gaziantep BB | 2.47 | 3.34 | 2.69 |
| 07. 29/12/22 | 19:00 | Girona vs Rayo Vallecano | 2.36 | 3.15 | 3.05 |
| 08. 29/12/22 | 21:15 | Betis vs Athletic Bilbao | 2.70 | 3.25 | 2.55 |
| 09. 29/12/22 | 22:00 | GD Estoril vs Boavista | 2.27 | 3.13 | 3.18 |
| 10. 29/12/22 | 22:45 | Blackburn vs Middlesbrough | 2.53 | 3.22 | 2.68 |
| 11. 29/12/22 | 22:45 | Wigan vs Sunderland | 2.69 | 3.19 | 2.54 |
| 12. 29/12/22 | 23:00 | Nice vs Lens | 3.14 | 2.89 | 2.43 |
| 13. 30/12/22 | 11:45 | Western United vs Brisbane Roar | 2.49 | 3.24 | 2.74 |

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMANNE - 27/12/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 12:15 | 3033 | Adelaide United vs Newcastle Jets | 1.80 | 3.73 | 3.98 |
| 12:15 | 5526 | Melbourne City FC W vs Perth Glory W | 1.36 | 4.87 | 6.23 |
| 15:00 | 2849 | Wuhan Three Towns FC vs Hangzhou NG | 1.48 | 4.28 | 5.25 |
| 15:20 | 4387 | AL Arabi (SA) vs Al Ahli Jeddah | 2.82 | 2.92 | 2.48 |
| 15:30 | 1950 | Leyton Orient vs Stevenage | 2.19 | 3.12 | 3.31 |
| 15:30 | 5620 | Vietnam vs Malaysia | 1.35 | 4.67 | 6.81 |
| 15:35 | 4174 | AL Akhdood vs AL Khlood | 2.27 | 2.83 | 3.27 |
| 16:00 | 1507 | Coalville Town vs Barwell | 1.56 | 4.28 | 4.47 |
| 16:00 | 2096 | US Souf vs MO Constantine | 1.67 | 3.29 | 5.03 |
| 16:00 | 3061 | ASM Oran vs SC Mecheria | 2.88 | 2.78 | 2.54 |
| 16:00 | 3161 | AS Khroub vs Ib Khemis El Khechna | 1.48 | 3.85 | 7.20 |
| 16:00 | 4999 | MC Saida vs Skaf Khemis Miliana | 2.04 | 2.92 | 3.75 |
| 16:00 | 5174 | ES Mostaganem vs GC Mascara | 1.21 | 5.06 | 13.62 |
| 16:00 | 5969 | Corinthian Casuals vs Aveley FC | 3.07 | 3.46 | 2.06 |
| 16:30 | 5536 | Porthmadog FC vs Conwy Borough | 1.81 | 3.70 | 3.60 |
| 17:00 | 1634 | Gresford Athletic vs Buckley Town | 2.32 | 3.55 | 2.58 |
| 17:00 | 1791 | Pontardawe Town FC vs Swansea University FC | 2.13 | 3.55 | 2.87 |
| 17:00 | 1993 | Ittifaq Marrakech vs Rapide Oued Zem | 1.96 | 2.95 | 4.50 |
| 17:00 | 2309 | Ethiopian Medhin vs Adama City FC | 2.63 | 2.83 | 2.73 |
| 17:00 | 2417 | Ankaragucu vs Umraniyespor | 1.82 | 3.64 | 3.99 |
| 17:00 | 3198 | Racing Athletique vs Club Jeunesse Ben Guerir | 1.91 | 2.85 | 5.00 |
| 17:00 | 3738 | Basaksehir vs Antalyaspor | 1.79 | 3.62 | 4.17 |
| 17:00 | 3952 | Chirk AAA vs Llandudno FC | 5.24 | 4.08 | 1.51 |
| 17:00 | 5352 | IZK Itihad Z Khemisset vs Raja Beni Mellal | 2.55 | 2.70 | 3.30 |
| 17:00 | 5781 | Prestatyn Town vs Holyhead Hotspur | 1.41 | 4.67 | 5.64 |
| 17:30 | 1404 | Penrhyncoch vs Cefn Druids | 2.67 | 3.88 | 2.14 |
| 17:30 | 2223 | Briton Ferry vs Goytre United | 1.24 | 6.03 | 7.98 |
| 17:30 | 2725 | Ruthin Town vs Colwyn Bay | 5.25 | 4.38 | 1.47 |
| 17:30 | 3319 | Llanelli AFC vs Taffs Well | 2.07 | 3.45 | 3.06 |
| 17:30 | 5035 | Abergavenny Town vs Cwmbran Celtic | 2.30 | 3.80 | 2.49 |
| 17:30 | 5331 | Ammanford vs Carmarthen Town AFC | 3.22 | 3.91 | 1.87 |
| 17:30 | 5343 | Barry Town FC vs Llantwit Major | 1.35 | 4.75 | 6.79 |
| 17:45 | 4089 | AL Badii vs Al Ahli Manama | 4.86 | 3.98 | 1.55 |
| 18:00 | 1126 | Pyramids vs El Ittihad Alexandria | 1.60 | 3.72 | 5.56 |
| 18:00 | 1967 | Bolton vs Derby | 2.34 | 3.27 | 2.88 |
| 18:00 | 4235 | Dundela FC vs H and W Welders | 1.56 | 4.09 | 4.68 |
| 18:25 | 2575 | Jeddah Club vs AL Qaisoma | 2.44 | 2.88 | 2.92 |
| 20:00 | 1298 | Afan Lido vs Trefelin FC | 2.16 | 3.65 | 3.05 |
| 20:00 | 3554 | Fenerbahce vs Hatayspor | 1.28 | 5.58 | 8.97 |
| 20:15 | 4184 | Reading vs Swansea | 2.86 | 3.21 | 2.39 |
| 20:15 | 4362 | Raja Casablanca vs MAS Maghrib A Fes | 1.84 | 3.15 | 4.70 |
| 20:30 | 4752 | Chelsea vs Bournemouth | 1.31 | 5.13 | 8.09 |
| 20:45 | 1953 | Sitra Club vs Bahrain Club | 2.06 | 3.16 | 3.35 |
| 22:00 | 1482 | KVC Westerlo vs Royal Antwerp | 3.03 | 3.53 | 2.17 |
| 22:00 | 5355 | St Truiden vs Zulte Waregem | 1.62 | 3.88 | 4.98 |
| 22:30 | 4097 | RS Berkane vs Ittihad Tanger | 1.83 | 3.20 | 4.70 |
| 22:45 | 1547 | Beaconsfield Sycob vs Bracknell Town | 2.77 | 3.69 | 2.14 |
| 23:00 | 2074 | Burnley vs Birmingham | 1.61 | 3.66 | 5.35 |
| 23:00 | 3682 | Manchester Utd vs Nottingham | 1.35 | 4.76 | 7.88 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# AZAM: BAHATI IMEIBEBA YANGA

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa Klabu ya Azam FC, Kally Ongala, amesema kikosi chake kilipambana vizuri dhidi ya Yanga, lakini bahati ndiyo iliyowabeba wapinzani wao hao na kufanikiwa kushinda mabao 3-2 kwenye mechi hiyo ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa juzi usiku katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Akizungunza baada ya mchezo huo, alisema wachezaji wake walipambana isipokuwa bahati haikuwa upande wao.

> **"Tulicheza mpira mzuri wenzetu waliweza kutumia udhaifu wetu wakatufunga japokuwa tulipambana ba hati haikuwa ya kwetu," alisema Ongala.**

Alisema Yanga ni miongoni mwa timu bora, yenye uzoefu wa kumiliki mpira, lakini Azam ilimiliki mchezo kwa asilimia kubwa licha ya kupoteza. Ongala alisema makosa ambayo wameyafanya katika mchezo huo atayafanyia kazi yasijirudie kwenye michezo ijayo.

"Wachezaji wangu wameonyesha uwezo mkubwa licha ya kuwa wamefanya makosa ambayo tutayafanyia marekebisho, tunaomba mashabiki wetu wasikatishwe tamaa na matokeo hayo," alisema.

Alisema wanatarajia kufanya usajili wa kishindo kwa kuongeza wachezaji ambao wataifikisha mbali zaidi timu yao.



Kali Ongala - Kocha Azam FC

# Chama azidi kunoga Simba ikiirarua KMC

INATOKA UK 32

Ilikuwa ni kama imechokoza nyuki, kwani baada ya bao hilo, wachezaji wa Simba walicharuka na kufanya mashambulizi mfululizo na ya hatari, kiasi cha kupachika bao la pili dakika tatu tu baada ya wapinzani wao kusawazisha.

Ulikuwa ni kama msako, krosi na mashuti makali yaliyokuwa yakipigwa langoni mwa KMC yakiwababatiza mabeki na kuokolewa na kipa.

Mwishowe, krosi ya Sakho ilimkuta Sadio Kanoute aliyeachia shuti kali lililotemwa na kipa Kisu aliyefanya kazi kubwa jana, mpira ukatua kwenye mguu wa Okrah ambaye naye alichia shuti kali la chini chini lililotinga wavuni.

Chama alifikisha 'assist' ya 10 msimu huu akiendelea kuwa kinara wa pasi za mwisho, alipopiga faulo nje ya eneo la hatari na Inonga aliruka juu akaupiga kichwa kuukwamisha wavuni likiwa ni bao la tatu dakika ya 73.

Ni bao la pili mfululizo kwa mchezaji huyo na msimu huu kwani Jumatano iliyopita alifunga bao la kusawazisha lililoipa sare ya bao 1-1 dhidi ya Kagera Sugar kwenye Uwanja wa Kaitaba, Bukoba, mkoani Kagera.

Lilikuwa ni bao lake la kwanza baada ya kuongezwa tena mkataba wa miaka miwili na klabu yake hiyo. Pamoja na mabadiliko ya pande zote mbili, ambayo yaliongeza kasi ya mchezo, lakini matokeo yalibaki kama yalivyo.

KMC imebaki na pointi zake 22 ikiwa kwenye nafasi ya tisa ya msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo iko kwenye mzunguko wa pili.

# Nabi aanika tatizo Yanga

INATOKA UK 32

shatoka huko," alisema Ongala.

Alisema ubingwa kwa sasa wanajiandoa kwa sababu tofauti ya pointi 10 hadi 11 ni jambo ambalo ni ngumu sana kuzifikia hivyo sasa wanapigania kumaliza katika nafasi ya juu.

Michezo

Nipashe Jumanne Desemba 27, 2022



## Zidane apigiwa debe Brazil

UKURASA 29

# Chama azidi kunoga Simba ikiirarua KMC

## ●●● Bocco taratibu anakuja kwa mabao, huku Inonga naye akizidi kutupia...

**Na Adam Fungamwango**

NAHODHA wa Simba, John Bocco, jana alifikisha bao la sita kwenye orodha ya wafungaji wa Ligi Kuu Tanzania Bara, beki Henock Inonga akifunga bao la pili mfululizo huku Clatous Chama akifikisha 'asisti' ya 10, wakati timu yao ikiibuka na ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya KMC FC.

Katika mechi hiyo iliyopigwa Uwanja wa CCM Kirumba, huo ni ushindi ambao umeifanya Simba kufikisha pointi 41 ikiendelea kukamata nafasi ya pili sasa kwa nafasi zaidi baada ya juzi Azam kuchapwa mabao 3-0 dhidi ya Yanga kwenye Dimba la Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Simba sasa imeizidi Azam pointi nne baada ya kulingana nayo kwa muda mrefu, huku ikiendelea na kampeni yake ya kuifukuza Yanga inayong'ang'ania kileleni kwa pointi 47.

Kama ingekuwa makini, Simba ingeweza kupata mabao 5-0 hadi mapumziko, lakini wachezaji wake walikosa utulivu wa kutumia nafasi nyingi ilizozipata.

Dakika ya 11 tu, Bocco alipiga kichwa dhaifu na mpira ukadakwa na kipa David Kisu, akiwa katikati ya mabeki wa KMC, akiunganisha mpira wa krosi kutoka kwa Shomari Kapombe na kukosesha timu yao bao.

Dakika mbili baadaye Pape Sakho alitaka kufunga kwa kisigino mpira uliorudishwa ndani na Mohamed Hussein 'Tshabalala' baada ya kipa Kisu kutoka golini, lakini mpira uliokolewa kabla haujavuka mstari na Kelvin Kijili.

Bocco alikosa tena bao, dakika moja baadaye, alipotanguliziwa mpira na Chama, lakini akiwa peke yake na Kisu, alishindwa kumlamba chenga kipa huyo, akauwahi na kuuweka kwenye himaya yake.

Hatimaye dakika ya 15, ikiwa ni dakika moja tu baada ya kukosa bao hilo, alisawazisha makosa yake alipokwamisha mpira wavuni, akiunganishwa kwa mguu mpira wa krosi kutoka kwa Kapombe.

Mpira ulianzia kwa Chama ambaye alimpenyezea Kapombe aliyemimina krosi iliyomkuta mfungaji likiwa ni bao lake la sita msimu huu na la kwanza kwenye mechi hiyo.

Kapombe ambaye alikuwa kwenye kiwango bora jana, aliweka tena krosi nyingine ambayo haikutendewa haki na Augustine Okrah, ambaye aliutoa nje.

Shambulizi pekee la KMC dakika 45 za mwanzo lilikuwa ni dakika ya 40, wakati kona ya Awesu Awesu ikiunganishwa kwa kichwa na George Makang'a, lakini Aishi Manula alikuwa macho akaudaka mpira huo.

KMC ilianza kipindi cha pili kwa kasi na kufanya mashambulizi kadhaa langoni mwa Simba na haikushangaza ilipofanikiwa kusawazisha bao dakika ya 51.

Alikuwa ni Sadallah Kipangile aliyekwamisha mpira wavuni mbele akiwa katikati ya mabeki wa Simba, baada kupokea krosi fupi safi kutoka kwa Ken Mwambungu aliyemuacha Joash Onyango na kumuwekea mfungaji.

INAENDELEA UK 31



Chama

# Nabi aanika tatizo Yanga

**Na Saada Akida**

LICHA ya kuibuka na ushindi wa mabao 3-2 dhidi ya Azam FC juzi, Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, ameweka wazi bado kuna tatizo katika safu yake ya kiungo.

Katika mchezo huo uliopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Azam iliumiliki mpira kwa asilimia kubwa, lakini ilijikuta ikishindwa kupata matokeo dhidi ya mabingwa watetezi hao.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nabi alisema kipindi cha kwanza Azam FC walitawala mpira katika safu ya kiungo na kuwatumia vizuri mawinga wao hivyo kupata bao la kuongoza kabla ya wao kusawazisha na kuongeza la pili baada ya dakika chache.

Alisema baada ya kufunga bao la pili na Azam FC kuingia kipindi cha pili wakiwa imara waliendelea kutawala mpira hali iliyosababisha kufanya mabadiliko kwa kumuingiza Tuisila Kisinda na Farid Mussa.

"Tuliona mechi inaenda sare, lakini tulipofanya mabadiliko yalitusaidia kuweza kupata ushindi, Azam katikati walikuwa wazuri zaidi, waliweza kutengeneza nafasi kwa sababu wana wachezaji wazuri kati na mawinga.

Alisema ubora wa Azam FC ulifanya wachezaji wake kushindwa kukaba, kwa sababu mpira ni mchezo hautabiriki na bahati haikuwa kwao ndio maana walipata pointi tatu, kwani kwa jinsi walivyocheza wangeondoka na pointi moja," alisema Nabi.

Kaimu Kocha Mkuu wa Azam FC, Kali Ongala, alisema walianza vizuri mchezo na kuutawala dakika ya 45 za kipindi cha kwanza na baada ya kupata bao la kuongoza wachezaji walijisahau na kuwapa nafasi wapinzani kusawazisha.

Alisema bao la pili walifungwa kizembe baada ya mabeki wake kutokuwa na mawasiliano, lakini pia waliporejea kipindi cha pili waliendelea kutawala mpira na kusawazisha.

"Kwa sasa tunaangalia mechi zilizopo mbele yetu, kuhakikisha tunapata matokeo mazuri kwa ajili ya kujiweka katika mahali pazuri ili kumaliza nafasi ya juu, suala la ubingwa tayari tume-

INAENDELEA UK 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >